Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA KUMI NA MBILI – TAREHE 22 JUNI, 2005

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika ( Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 109

**Kasoro Katika Chaguzi Mbalimbali**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa ni azma ya Serikali kufanya uchaguzi ulio huru na haki; na kwa kuwa uchanguzi uliofanyika Zanzibar uliharibika mara zote mbili hasa kutokana na utendaji mbovu wa Watendaji wa Tume ya Uchaguzi uliosababisha hata kurudiwa kwa uchaguzi katika Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 1995:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba kasoro zilizojitkeza katika chaguzi zilizopita hazitokei tena katika chaguzi za vitongoji, vijiji na mitaa za mwaka 2004 pamoja na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2005?

(b) Je, ni hatua gani zitachukuliwa kwa Maafisa wa Tume watakaobainika kuharibu chaguzi hizo kwa njia moja au nyininge?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMED SEIF KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazotumika kusimamia uendeshaji wa chaguzi za Vitongoji, Vijiji na Mitaa ni tofauti na zile zinazotumika kwa chaguzi za Rais, Wabunge na Madiwani. Hali kadhalika, naomba ieleweke kuwa Mamlaka zinazosimamia uendeshaji wa chaguzi hizo nazo ni tofauti.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ali Salim, Lenye sehemu ya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali imekuwa na itaendelea kuwa kuhakikisha chaguzi zote hapa nchini zinaendeshwa katika mazingira yaliyo huru, ya amani na haki na kwamba uzoefu wa chaguzi zilizopita za Rais, Wabunge na Madiwani unatumika kuboresha zaidi na kuandaa vema chaguzi zinazofuata ukiwemo huu wa Oktoba, mwaka 2005. Aidha kasoro chache zilizojitokeza katika chaguzi za vitongoji, vijiji na mitaa mwaka jana zitaepukwa katika chaguzi zijazo.

(b) Aidha, hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa Sheria kwa Maofisa wa Tume watakaobainika kuharibu chaguzi zikiwemo faini au kifungo au vyote viwili kwa pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Said swali la nyongeza.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Hivi majuzi palitokea utata hasa katika kutabulisha Wagombea jambo ambalo lilipelekea baadhi ya Vyama vya Upinzani kulalamikia hatua ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumtangaza mgombea wake wakidai kwamba ni kuanza kampeni.

Je, Serikali inaweza kutueleza nini tofauti mambo gani ukifanya yatajulikana kwamba ni kampeni na yapi si kampeni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - MHE. MUHAMED SEIF KHATIBU:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, kama ifuatavyo:-

Nafikiri tumesikia tamko la Tume ya Uchaguzi kwamba imetoa maelekezo na jambo linalofanywa na CCM sasa hivi ni utambulisho wa Mgombea wao ndani ya chama chao. Kwa hiyo si makosa, lakini ningependa niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba

chama chako Mheshimiwa Salim kimewatangaza Wagombea pale Jangwani hadharani na si makosa pia.

Na. 110

**Ujenzi wa Barabra ya Marangu – Kilema Maua Seminari**

**MHE. MAJOR JESSE MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara toka Marangu Mtoni hadi kwenye hoteli ya Kitalii ya *Kibo Hotel* ilijengwa kwa kiwango cha Lami na Watalii wengi waliipenda sana hoteli ya Kibo kwenye miaka michache iliyopita; na kwa kuwa, barabara hiyo imeharibika vibaya mno kiasi cha kusababisha watalii kukataa kuingia kwenye hoteli hiyo maarufu na kulikosesha Taifa fedha za kigeni; na kwa kuwa, kuna mapipa mengi ya lami yaliyoko katika viwanja vya hoteli hiyo na nyingine iko pale Marangu Kyala *KNCU* kwa miaka mingi sasa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutafuta mkandarasi wa kuitengeneza barabara hiyo kuanzia Marangu Mtoni hadi Kilema Maua Seminari kwa mkataba nafuu wa kutumia lami iliyopo japo kwa kiwango cha *Otta seal*?

(b) Je, utengenezaji wa barabara hiyo unaweza kukamilika katika awamu hii ya uongozi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye Sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali la Bunge Na. 181 tarehe 5/2/2001 nilishauri Halmashauri ya Wilaya ya Moshi vijiji kufanya yafuatayo ili lami hiyo isiharibike kwa sababu ya kukaa muda mrefu.

Kwanza, Halmashauri iangalie uwezekano wa kutumia mapato yake ya kila mwaka pamoja na mgao wake wa fedha za Mfuko wa Barabra zinazotolewa kwa halmashauri zote nchini kupitia Ofisi yetu kutengeneza barabara hizo.

Pili, Halmashauri iongeze juhudi za kutafuta Wahisani watakaoweza kusasidia ujenzi wa barabara hiyo.

Tatu, Halmashauri iuze lami hiyo na fedha zitakazopatikana zijenge barabara hizo kwa kiwango cha changarawe.

Aidha, niliwaomba Waheshimwa Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini na Major Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, kwa kuwa wote ni wajumbe wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini watusaidie kuiwezesha Halmashauri hiyo kufikia maamuzi yake haraka iwezekanavyo kabla ya lami hiyo kuharibika.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mtoni – Kilema – Maua Seminari ambayo inapendekezwa na Mheshimiwa Mbunge kuwekewa lami aina ya *Otta Seal*, ni barabara ya wilaya na hali ni nzuri kwa wastani. Barabara hii ina kipande cha urefu wa km. 1.40 ambacho kilikuwa na lami na sasa kimeharibika kabisa. Aidha, majadiliano yaliyofanywa kwenye vikao vya Halmashauri kujadili ushauri uliotolewa na Serikali baada ya kujibu Swali Na. 181 haukuzaa matunda yoyote. Wananchi wanaendelea na msimamo wao wa kutotaka lami iuzwe ili zipatikane fedha za kujenga barabara kwa kiwango cha changarawe, pia hawajachanga fedha zozote kwa ajili ya kusaidia katika ujenzi wa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, lami inayoelezwa na Mheshimiwa Mbunge iko katika mapipa 1,000 ambayo yanaweza kutengeneza km 4.5 kwa kiwango cha "*Otta Seal*". Makadirio ya awali *(preliminary estimates)* ya kazi hiyo inakisiwa kugharimu shilingi milioni mia mbili hamsini (Shs. 250 milioni)

Kwa kuwa, lami hiyo inaendelea kuwa katika hatari ya kuendelea kuharibika kwa kukaa muda mrefu bila kutumika na kutohifadhiwa vizuri na kwa kuwa Halmashauri imeshindwa kuchangia fedha au kupata wafadhili na wananchi hawataki lami iuzwe. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaelekeza yafuatayo:-

(i) Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ikapime lami hiyo ili kuona yote ina ubora unaostahili kwa kazi ya ujenzi.

(ii) Kwa kuwa, Mradi wa *NRTP* ambao utajihusisha na matumizi ya lami nafuu (*low cost seals*), Halmashauri iwasiliane na Ofisi yangu baada ya kutambua kiasi cha lami kinachofaa kwa kazi za ujenzi baada ya hapo ndiyo tutaamua namna ya kusaidiana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ni wakati muafaka wa kumtafuta Mkandarasi kwa ajili ya kutenganea barabara ya Mtoni – Kilema – Maua Seminari kwa kiwango cha *Otta Seal* hadi hapo kiwango cha lami inayoweza kutumika kitakapo julikana na hivyo kujua urefu wa barabara unaoweza kutengenezwa na gharama yake. Kwa hali hiyo barabara hii kwa sasa haita kamilika katika awamu hii ya uongozi.

**MHE. MAJOR JESSE MAKUNDI**: Mheshimwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimia Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri pia na maelekezo yake aliyoyatoa ambayo hakika ni sahihi.

Je, katika kipindi hiki cha Bajeti anaweza kutenga kiasi kidogo cha kunyanyua kipato cha Halmashauri ya Moshi ili iweze kumtafuta Mandarasi na Mkandarasi huyo aweze kuendelea na kazi yake japo kwa kilimita moja ya kuanzia kufanya majaribio?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Major Makundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, najua shauku aliyonayo Mheshimiwa Mbunge hasa wakati wa kipindi kama hiki na nina uhakika tungekuwa na fedha tungejaribu kufanya hilo ombi likakamilika lakini kama nilivyosema kwa hali tuliyonayo hata kwenye Bajeti ya mwaka huu ambayo inamalizika hivi sasa hilo halitawezekana na kwa Bajeti inayokuja kwa bahati mbaya tayari tumekwishaweka mipango yote kulingana na mipango mliyowasilisha kutoka kwenye Halmashauri yetu kwa hiyo narudia rai yangu ileile tuombe Halmashauri ifanye kazi ya kupima lami kwanza kisha tushirikiane namna ya tunavyoweza kujaribu kuingiza utaratibu huo katika *NRTP*.

Na. 111

**Ubovu wa Barabara Katika Kata**

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya kutoka Changarawe hadi Mbamba; na ile ya kutoa uwanja wa Ndege hadi kijiji cha Malangali hazijafanyiwa matengenezo kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano (5):-

Je, ni lini barabara hizo zitaanza kutengenezwa ili zifae kupitika kwa urahisi bila usumbufu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa barabara ya Changarawe – Mbamba haijafanyiwa matengenezo kwa zaidi ya miaka mitano kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Lakini nasikitika kusema kwamba barabara hii iko katika daraja la barabara za Vijiji na kwa kuwa sheria yetu ya sasa ya Mfuko wa barabara fedha zake hazitumiki kwenye barabara za aina hiyo haipangiwi bajeti za matengenezo kwa hivi sasa kupitia Mfuko wa barabara. Kwa hiyo wenye jukumu la kutengeneza barabara hizi ni wanavijiji wanaohudumiwa na barabara hizo na hasahasa kwa kushirikiana na Halmashauri husika ambayo inatakiwa itenge fedha kutokana na mapato yake. Hivyo nashauri Halmashauri hiyo pamoja na wanavijiji na pamoja na Mheshimiwa Mbunge mkae pamoja mjaribu

kuona ni namna gani tunaweza tukatatua tatizo hilo kwa kuwa barabara hiyo kwa sasa si moja ya barabara zilizoainishwa chini ya mfuko wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Uwanja wa Ndege – Malangali, barabara hiyo haipo katika ramani ya mtandao wa barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Ila kuna barabara ya kuanzia Tende (Uwanja wa Ndege) hadi Kilangali kupitia katika kijiji cha Kivungu ambayo pia hali yake ni mbaya. Barabara hii pia kwa bahati mbaya ni barabara ya daraja la Barabara za Vijijini hivyo wenye jukumu la kuitengneza ni Halmashauri yenywe kupitia vyanzo vyake kwa kushirikiana na wanavijiji wanaohudumiwa na barabara hiyo.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu vizuri.

Lakini kwa kuwa amekubali na nimwongezee tu kwamba barabara hiyo ndiyo kwenye uchumi mkubwa kuondoa umaskini kwa maana ya sera hii ya MKUKUTA ndiyo tuna Shamba kubwa la Kilangali la kutengeneza mbegu.

La kwanza, Sasa haoni sasa wakati umefika kuacha kuiachia Halmashauri barabara hizi zote mbili washirikiane wao na Wizara ya Kilimo pamoja na TAMISEMI wakatenga fedha?

La pili, kwa kuwa barabara sasa kwa muda mrefu imebaki kwenye ngazi ya vijiji hawaoni sasa imefikia hatua iende kwenye ngazi ya TAMISEMI?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Wegga maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi yetu inatambua umuhimu wa barabara hiyo na kama alivyosema Mbunge ni kweli kabisa kwamba inakwenda katika eneo la Kilimo kikubwa sana katika eneo hilo lakini kama nilivyosema tufanye nini katika hali kama hii hakuna mwenye jibu la moja kwa moja. Ninachoweza kusema hapa ni kwamba Halmashauri yake ya Kilosa ikikaa kwa ushirikiano mzuri na Mbunge, uwezo wa kutenga fedha kidogo kidogo na matengenezo yakawa yanafanyika upo si kwamba haupo, upo. Kwa hiyo tunachoweza kusaidia hapa ni kutoa msukumo kwa Mkurugenzi ili ahakikishe kwa kweli barabara hii inafanyiwa matengenezo.

Kuhusu swali la pili, ni kweli kwamba barabara hizi nyingi kuziacha kuwa zinasimamiwa na vijiji na hata Halmashauri zao kwa kiasi Fulani ni mzigo mkubwa sana. Lakini bahati mbaya kwa sasa hatuwezi kusema kwamba tunaweza tukazihamishia barabara hizo zote TAMISEMI kwa sababu Mfuko uleule wa asilimia 30 ndiyo bado tunaulalamikia kwamba hautosho, kwa hiyo kwa sasa itabidi tuende na programu mbalimbali tulizonazo *NRTP* ikiwa mojawapo tukiitumia vizuri inaweza ikatupunguzia tatizo hili.

Na. 112

**Uwekezaji Kwenye Maeneo Mbalimali Nchini**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (K.n.y. MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwelekeo wa sera ya uchumi sasa inalenga katika uwekezaji; na kwa kuwa, wawekezaji wote wanafuata zaidi maeneo yenye miundombinu iliyokamilika kama vile barabara za uhakika, umeme, maji ya kutosha, mawasiliano ya simu na viwanja vya ndege;

(a) Je, Serikali haioni kwamba, yale maeneo ambayo hayana miundombinu, uchumi wake utaendelea kudumaa na yale yenye miundombinu yatakuwa na maendeleo makubwa zaidi?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, kutofautiana kwa kiwango kikubwa cha uchumi katika nchi moja kunaweza kuleta hisia mbaya kwa wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu mwelekeo wa sera ya uchumi kwamba inalenga kupanua uwekezaji. Ni kweli kuwa miundombinu kama vile barabara, maji, nishati, mawasiliano ya simu, viwanja vya ndege n.k ni moja ya mahitaji ambayo yanachochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kuliko sehemu ambazo hazina miundombinu na huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, mbali na huduma nzuri ya miundombinu, uwepo wa raslimali na maendeleo ya sekta nyinginezo kunachochea zaidi uwekezaji kwa ujumla. Kwa mfano sehemu ya kitalii (zenye mbuga za wanyama na Ndege) zinachochea uwekezaji katika viwanja vya ndege na barabara.

Mheshimiwa Spika, kutofautiana kwa kiwango cha kukua kwa uchumi baina ya maeneo mbalimbali nchini hutokana na kasi ya uwekezaji katika miundombinu; rasilimali zilizopo katika eneo na hali ya kijiografia kiuzalishaji bidhaa mbalimbali za biashara. Kwa hiyo, haitakuwa sahihi kufikiria kuwatofauti za kiuchumi kati ya eneo moja na jingine ni lazima zitokane na kuwepo miundombinu peke. Hivyo kwa kuwaelimisha wananchi juu ya vichocheo vya maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi, wataweza

kuondoa hisia mbaya kama vile kupendelea maeneo fulani na kubagua mengine juu ya Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, mikakati iliyopo na inayoendelezwa na Serikali ni: Ujenzi wa barabra unaoendelea nchini kama vile mradi wa ujenzi wa Daraja la Mkapa uliokamilika mwaka jana na ujenzi unaoendelea wa barabara ya Kibiti Lindi, ni mojawapo ya juhudi za Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya miundombinu muhimu. Vile vile Serikali imeendelea kubuni mikakati mbalimbali itakayosaidia kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuboresha mipango yamaendeleo nautekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mbali na mikakati iliyopo, Serikali imeruhusu na inahamasisha wawekezaji wengine hususan sekta binafsi ili nao kuwekeza kwenye miradi na miundombinu. Aidha, Serikali kupitia mpango wa kanda za maendeleo (*Development Corridors),* miradi itakayoshughulikiwa ni pamoja na ile ya kuendeleza miundombinu kwa mfano chini ya program ya *Mtwara Development Corridor* ambayo inasimamiwa na Shirika la Maendeleo la taifa *(NDC),* Mkoa wa Mtwara utanufaika na miradi ya uendelezaji wa miundombinu iliyomo katika programu hiyo. Programu za maendeleo za jumuia mbalimbali kama vile Jumuia ya Afrika Mashariki, *SADC* na *NAEPAD* ambazo Tanzania ni mwananchama.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mikakati ya kisera iliyopo, katika kipindi cha miaka michache ijayo, maeneo yote ya nchi yatakuwa na miundombinu ya uhakika na huduma za kutosha. Namwomba Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kusaidiana na Serikali katika kuwaelimisha wananchi na Taasisi mbalimbali ili waweze kushiriki vema katika utekelezaji wa kuharakisha maendeleo ya sekta ya miundombinu nchini.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini ningeomba kuuliza kwamba kwa kuwa, Serikali kwa hivi sasa na hasa katika bajeti hii lengo na nia kubwa ni kukuza huu mradi mkubwa wa MKUKUTA. Je, mikakati gani maalumu ambayo Serikali imeweka ili kulenga matatizo ya mikoa ile ambayo iko nyuma na maana yangu katika hili ni kwamba katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Kigoma, Rukwa, Musoma na kadhalika tunaomba tupewe msimamo maalum wa Serikali na jinsi itakavyoshughulikia matatizo ya maeneo haya. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrope kama ifuatavyo:

Mpango wa MKUKUTA kama ilivyo tofauti na mpango wetu wa mwanzo, mpango huu sasa umechukua maeneo katika sekta zote. Maeneo ya kukuza uchumi, maeneo ya kuendeleza huduma za jamii na maeneo ya kuendeleza utawala bora. Lakini katika mpango huu vilevile suala moja la muhimu lililowekwa ni kuangalia kwamba

mipango hii inajaribu kuondoa tatizo la uwekezaji tofauti baina ya mikoa nchini kwa maana ya *Investment Desparities,* sasa kutokana na miradi ambayo imewekwa katika mpango huu nina hakika sasa pamoja na miundombinu itakayojengwa itaondoa tatizo la kuacha mikoa mingine iwe nyuma ikilinganishwa na mikoa ambayo iko mbele. (*Makofi*)

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niongeze angalau swali moja.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukilalamika juu ya uwezekano wa kuvifanya viwanda vya korosho vilivyopo katika maeneo ya kule vifanye kazi kwa muda mrefu sana tumelalamika hilo. Tunashukuru sasa imejitokeza kwamba amepatikana mwekezaji, sasa kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ametaja miundombinu kwamba ni kichocheo kikubwa cha maendeleo yoyote yale.

Na kwa kuwa, sasa anataja kwamba uko mpango wa *Mtwara Corridor* nilikua nataka niulize kwamba viwanda vile vya korosho amepewa mtu kufanya kazi kule hakuna maji ya kutosha, hakuna umeme wa kutosha na hata ilipopatikana fursa hii ya kupata hii *Mtwara Corridor* kutengeneza barabara na barabara inayotajwa haitoki.

**SPIKA:** Uliza swali, maelezo hayatakiwi.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, Je, kama barabara inayotajwa kwenye *Mtwara Corridor* haipiti Mtwara, Nanyamba, Tandahimba, Newala mpaka Masasi hata viwanda hivi vikiambiwa sasa vianze kufanya kazi na vinahitaji kwenda bandarini kwenda kupeleka bidhaa shughuli hii itafanyikaje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mhehimiwa Lutavi kama ifuatavyo:-

Kwanza ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Lutavi kwa jitihada kubwa aliyoiweka ya kuhakikisha kuwa viwanda vya kubangulia korosho vya mikoa yote ya Kusini sasa vimepata wawekezaji baada ya ubinafsishaji na vitaanza kufanya kazi kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika., suala la kuboresha miundombinu kama nilivyosema katika suala langu la msingi tunalichukulia ni kama ni mchakato ambalo lazima lichukue muda na miminimeweza kutembelea viwanda vyote hivi vya korosho na nikaviona kwamba vinafikika kwa sababu barabara za kule zinatengenezwa.

Sasa kuhusu suala la upungufu wa miundombinu kwa mfano nishati ya umeme, mimi nina uhakika kabisa kwamba baada ya kukamilisha mradi wetu wa *gas* ya *Mnazi Bay* haya yatakuwa ni matatizo ya kihistoria na eneo lile liataamka kwa juhudi zaidi na kuchangia maendeleo ya uchumi wetu. *(Makofi)*

Na. 113

**Athari za Ukame 2004/2005**

**MHE. LEONARD M. SHANGO (K.n.y. MHE. RAPHAEL N. MLOLWA)** aliuliza:

Kwa kuwa, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2004/2005 kumekuwa na ukame wa muda mrefu katika maeneo mengi nchini na kusababisha mazao mengi mashambani kukauka hata katika wilaya zinazosemekana kwamba huwa mara nyingi hazipungukiwi na chakula kama Kahama na Bukombe:-

Je, Serikali imeliona tatizo hili na imeliona, imeandaa mkakati gani wa makusudi wa kuhaskikisha kuwa wananchi wote, wakiwemo wale wa Jimbo la Kahama wanahakikishiwa upatikanaji wa chakula cha kutosha wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Nkuli Mlolwa, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2004/2005, ukame ulijitokea mwezi wa Januari na Februari, 2005, hususan katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Shinyanga. Ukame huo uliathiri mazao yaliyokuwa mashambani hasa zao la mahindi, ambalo lilikuwa katika hatua za kuchanua na kubeba. Mvua zilizonyesha mwezi wa Machi 2005, zilisaidia kukua kwa mazao mengine ya mtama, uwele, muhogo, viazi vitamu na mpunga.

Serikali inatambua kwamba kulitokea ukame ambao utasababisha upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya katikati ya nchi katika mwaka wa 2005/2006. Aidha, upungufu huo usingekuwepo iwapo wananchi katika maeneo yanayokabiliwa na ukame wa mara kwa mara wangezingatia ushauri wa serikali wa kulima mazao yanayostahimili ukame. Aidha, wananchi walipaswa kujiwekea akiba ya chakula kutokana na mavuno mazuri ya msimu uliotangulia.

Tathmini iliyofanywa na Wizara ya Kilimo na Chakula katika Mkoa wa Shinyanga imebaini kamba Wilaya za Maswa, Meatu, Kishapu, Shinyanga Vijijini, Bariadi na Kahama zitakuwa na upungufu wa chakula kwa viwango tofauti wakati Wilaya ya Bukombe itakuwa na ziada ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua tahadhari ya kujikinga na njaa kwa nchi nzima. Hadi tarehe 15 Mei, 2005 Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilikuwa na tani 114,635 za mahindi. Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilikuwa na tani 4,917 za mahindi katika maghala yake yaliyoko Shinyanga. Chakula hicho kitasaidia kuhudumia wananchi watakaobainika kuathirika na upungufu wa chakula, wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji endelevu wa chakula kwa wakati wote, nachukua fursa hii kurudia wito wa serikali wa kuhimiza wananchi kulima mazao kulingana na mazingira ya maeneo yao. Kwa mfano, mikoa ya kati itoe kipaumbele katika kilimo cha mazao ya chakula yanayostahimili ukame, kwa mfano uwele, mtama, mhogo viazi vitamu na kadhalika.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Je, kwa kuwa Janga la ukame linaendelea kulikumba Taifa hili mara kwa mara. Ufumbuzi wa kudumu kwa tatizo hili ni kuvuna maji ya mvua kwa kuendeleza kilimo cha kumwagilia. Je, Serikali inatoa tamko gani au kauli gani kuhusu kukubali sera ya kuvuna maji kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji?

Pili, kwa kuwa kuna miradi mingi ambayo inaonekana imeandaliwa katika Wilaya mbali mbali pamoja na Wilaya ya Kahama ya kuvuna maji au kuchimba mabwawa kwa ajili ya kilimo cha kumwagilia.

Je Serikali sasa kwa kuanzia bajeti hii itaanza mipango maalumu ya kuanza kuvuma maji katika miradi ambayo iko katika Wilaya ya Kahama pamoja ile miradi ambayo ipo wilaya ya Iramba kwa mfano mradi wa kuvuma maji katika milima ya Sekenke ambayo unaainisha kata kama saba hivi kuanzia Urugu mpaka Kidaru. Je, Serikali itaanza kutekeleza kwa matendo siyo kwa kuzungumza na kuwa na kigugumizi cha mara kwa mara? (*Makofi*)

**NAIBU WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Shango kama ifuatavyo:

(a) Kuhusu kuvuna maji, Serikali inatoa tamko gani. Tamko rasmi ni kuwa hatukuanza leo tumenza nyuma kushughulikia suala la kuvuna maji, kuna malambo na kuna mifereji ya kuchepusha maji ya mvua kwa manufaa au shughuli hizo hizo. Mimi mwenyewe nimewahi kufika katika Jimbo la Mheshimiwa Shango kushughulikia masuala hayo, tunaendelea.

(c) Miradi mingi ya Wilaya kuchimba mabwawa. Mabwawa tunayo sana na kwa taarifa hapahapa Mjini Dodoma tuna Ofisi maalum ya kushughulikia masuala ya Visima na Mabwawa. Narudia tunaendelea na tutaendelea kuhudumia umma kupambana na tatizo hili. Ahsante.

**SPIKA:** Kuna nafasi ya maswali mawili ya nyongeza, Mheshimiwa Said Juma Nkumba na Mheshimiwa nani sasa, aah! Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Dr. Slaa. Namwita Mheshimiwa Nkumba.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kwenye majibu yake ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ametumia lugha ya mazao

yanayostahimili mazao na kwa kuwa lugha ya mazao yanayostahimili ukame imekuwa inawachanganya wananchi. Je, Waziri anaweza kunitajia mazao yanayokua bila maji kwa maana ya ukame na yale yanayokua kwa maji ili wananchi waelewe? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tunaposema mazao yanayostahimili ukame tuna maana kwamba mazao ambayo hayahitaji mvua nyingi. Tunajua mazao yote yanahitaji maji, lakini mengine yakipata maji kidogo tu yanashamiri. Hiyo ndio tafsiri, kwa mfano, mihogo, viazi havihitaji mvua nyingi kama mahindi au mpunga unavyohitaji. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linauliza mkakati kwa watu ambao sasa hivi wana njaa na kwa kuwa suala la njaa linahusiana na uhai wa binadamu na kwa kuwa masuala yote aliyoeleza Mheshimiwa Waziri kuhusu mazao ya kudumu ni ya miaka ijayo.

Je, kwa mwaka huu kwa kuwa mvua imewadanganya wananchi wengi na maeneo mengi yamekuwa na ukame, Serikali katika Bajeti hii imetenga kiasi gani kuhakikisha wananchi hawa ambao hawana chakula sasa hawataathirika? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza pesa zitakazotengwa kwenye Bajeti hii sio hizo zitakazowapa wananchi chakula sasa hivi. Wananchi wenye upungufu wa chakula watakipata kutoka kwenye hifadhi ya Chakula ya Taifa na tumeeleza katika jibu la msingi kwamba tuna tani 114,000 kwenye maghala yetu ili kushughulikia dharura hizi za upungufu wa chakula.

Pale Shinyanga tuna tani karibu elfu tano, Arusha tuna tani karibu elfu tatu, halafu kule Rukwa kuna tani thelathini na mbili elfu na kadhalika. Kwa hiyo, tuna hakika kwamba tuna uwezo wa kumudu upungufu wa chakula ulipo sasa hivi.

Na. 114

**Kilimo cha Mahindi na Alizeti**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Sumbawanga hususan Jimbo la Kalambo ni maarufu kwa kilimo cha mahindi na alizeti na wananchi wa Kata za Matai Mkowe, Msanzi, Mwazye Mwimbi, Sopa na Mambwe kipato chao chote karibu asilimia themanini hutokana na mazao hayo mawili:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Jimbo hilo na Wilaya husika kwa ujumla kupata mwekezaji katika mazao hayo ili kuongeza thamani yake na kuinua pato la wakulima wa mazao hayo?

(b) Kwa kuwa, mipango ya kupata mbolea katika mwaka 2003/2004, haikuwa na ufanisi: Je, katika mwaka 2004/2005, Serikali iliandaa mpango gani wa kuondokana na aibu iliyojitokeza katika mwaka uliotangulia ili wananchi waridhike na mipango ya Serikali kwenye Wizara husika?

(c) Je, Serikali imeandaa vipi usimamizi wa usambazaji wa mbolea katika Mkoa wa Rukwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Ili kuwavutia wawekezaji kuwekeza kwenye Jimbo la Kalambo, Wilaya ya Sumbawanga na Mkoa wa Rukwa, Serikali inatekeleza mipango ya kuboresha miundombinu, hususan ujenzi na ukarabati wa barabara za Vijijini na barabara kuu na madaraja ili kurahisisha usafiri ndani ya Mkoa na kuunganisha Mkoa wa Rukwa na Mikoa inayopakana nao na pia na nchi za jirani. Mkoa wa Rukwa unaandaa kitabu kinachoeleza fursa za uwekezaji zilizoko katika Wilaya za Mkoa huo. Wananchi wa Jimbo la Kalambo na Wilaya ya Sumbawanga, wanashauriwa kuunda vikundi vya uzalishaji na usindikaji wa mazao ili waweze kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha ya kuwawezesha kuwekeza kwenye shughuli hizo.

(b)Mheshimiwa Spika, sikubaliani na Mheshimiwa Mwananzila kwamba usambazaji wa mbolea ya ruzuku katika mwaka wa 2003/2004 haukuwa na ufanisi na ulikuwa wa aibu. Kwanza, tunapaswa kuipongeza Serikali ya CCM ya Awamu ya Tatu kwa kuamua kurudisha tena utaratibu wa kutoa ruzuku kwa mbolea ili kumwezesha mkulima kupata mbolea kwa bei nafuu na kwa hiyo kuitumia kwa wingi. Pili, mpango wa ruzuku uliwezesha wakulima kutumia mbolea kwa wingi kuliko ilivyokuwa bila ruzuku. Matumizi ya mbolea katika Mkoa wa Rukwa yaliongezeka kutoka tani 1,003 iliyotumika mwaka wa 2002/2003 hadi tani 3,732.65, ongezeko la karibu mara nne. Ruzuku ilipunguza bei ya mbolea Sumbawanga Mjini kutoka sh. 23,000/= hadi sh. 14,0000/=. Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mbolea tija katika uzalishaji wa mahindi iliongezeka kutoka tani moja hadi tani 1.8 kwa hekta.

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa. Tukiri mafanikio hayo na kama kuna mapungufu yaliyotokea tuyashughulikie. Usambazaji wa mbolea wa msimu wa mwaka 2004/2005 umeshafanyika. Kwa maoni ya Wizara yangu ulifanyika kwa ufanisi na mafanikio makubwa kwenye Mkoa wa Rukwa. Katika kikao cha Mheshimiwa Rais na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Mikoa walisifu utaratibu wa kutoa ruzuku kwa mbolea na manufaa ya utaratibu huo kwa wakulima. Kamati za Mkoa na Wilaya ambazo Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe ndizo zilizokuwa na jukumu la kusimamia usambazaji wa mbolea hizo na Kamati hizo zinastahili pongezi kwa mafanikio yaliyopatikana.

(c)Usimamizi wa usambazaji wa mbolea ya ruzuku katika msimu wa 2004/05, unazingatia maelekezo yaliyotolewa katika Tamko la Serikali kuhusu Fidia ya sehemu ya Gharama ya Usafirishaji wa Mbolea kwa ajili ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika msimu wa Kilimo wa 2003/04, lililotolewa katika Bunge lako tukufu tarehe 13 Novemba, 2003. Tamko hilo linaainisha majukumu ya Kamati za Taifa, Mikoa na Wilaya.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa mahitaji ya mbolea katika Mkoa wa Rukwa ni zaidi ya tani 23,000, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri anazungumza ugawaji wa mbolea tani 3,000 kama ni mafanikio makubwa. Je, haya ndio mafanikio ambayo tunaweza kuyafurahia wakati tungeweza kuzalisha zaidi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa swali la msingi nimeuliza suala la uwekezaji ili kuongeza thamani ya mazao. Nchi jirani ya Zambia wanatumia sana unga wa mahindi ambao umeshaandaliwa tayari. Je, Wizara hii ya Kilimo inaweza kusaidia Mkoa wa Rukwa kuwa na kinu kikubwa cha kukoboa na kusaga unga kwa ajili ya kuuza nchi jirani ili tuweze kuwapatia bei nzuri wakulima wa Mkoa wa Rukwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mbolea ya ruzuku tuliyopeleka Mkoa huo zilikuwa tani 3,000, lakini bado tunasema ni mafanikio kwa sababu kama nilivyosema katika jibu la msingi, kabla mbolea hizi za ruzuku matumizi yalikuwa tani elfu moja tu. Sasa kutoka elfu moja mpaka elfu tatu na ushekhe ni sawasawa na mara nne zaidi. Sisi tunafikiri haya ni mafanikio. Aidha, huko Mkoani kuna Kamati ya kusimamia iliyoratibu shughuli hizo na kila tulipopata ombi la kuongeza mbolea tulijitahidi kufanya hivyo. Nakumbuka mimi mwenyewe niliwahi kwenda Sumbawanga mwaka jana kushughulikia suala hili. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, tutafikia huko anakotaka Mheshimiwa Mbunge tutakaposhirikiana Makao Makuu na hizo Kamati za Mkoa na Wilaya husika. Lakini pamoja na haya mafanikio yamekuwepo.

Pili, haya mahitaji anayosema Mheshimiwa Mbunge ambayo yapo Zambia, tunaomba ayalete katika utaratibu unaostahili. Hata hivyo, suala la shughuli hizo ni la *private sector*. Kwa hiyo, tunahamasisha tena Mkoa ujaribu kushughulikia suala hili kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali langu ni kwamba mwuliza swali ametaja mazao mawili, mahindi na alizeti. Sasa hivi karibuni viwanda vingi vya kusindika mafuta ya mbegu za alizeti, pamba na karanga vimejengwa huko Dar es Salaam na Wabunge hapa mara nyingi wamesema kwamba tungependa viwanda hivi vitumie mbegu kutoka hapa hapa katika kuzalisha. Je, *program* ya uzalishaji wa mbegu za mafuta kama vile alizeti kwa kuzingatia kwamba viwanda vimejengwa hapa hapa nchini ikoje?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, suala hili ni sawasawa na lile la kusindika mahindi ni suala la *private sector*, Serikali imejiondoa moja kwa moja katika shughuli hizo. Tunachofanya ni kuzalisha mbegu bora zenye mafuta kwa wingi na kuhamasisha wananchi wazizalishe kwa wingi na hapa tunatoa mwito *private sector* iwekeze katika shughuli hii na tutafanya kila iwezekanavyo, kama ikibidi kufanya mipango mingine basi mjadili huko kwenye Wilaya, ije Wizarani kama mradi wa *BAP DADAP,* hapo Serikali itaona nini kinaweza kufanyika, lakini mawazo yatoke huko katika maeneo husika.

Na. 115

**Kampuni/Asasi Kujiandikisha katika Soko la Hisa**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA** aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na hali halisi ya Kampuni/Asasi yoyote kujiandikisha katika soko la hisa na ili kuondoa uwezekano wa wananchi kutapeliwa fedha zao kunakoweza kufanyika kutokana na kampuni husika kughushi hesabu zao na kuonekana inafanya vizuri kibiashara na kupata faida:-

(a) Je, ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa kwa kampuni inayotoa/iliyotoa mwelekeo (*prospects*) wa uongo ili iorodheshwe kwenye soko la hisa?

(b) Serikali inafanya nini ili kuhakikisha kuwa wizi huo ambao umetokea katika kampuni ya kuzalisha gesi ya *TOL* na kuwaibia maelfu ya wananchi walionunua hisa hautokei tena kwa kampuni zenye nia kama hiyo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa wanahisa wa *TOL* na hatma ya *TOL* kwa ujumla katika biashara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uuzaji wa hisa wa makampuni kwa umma unaratibiwa chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 kama ilivyorekebishwa mwaka 1997 ambayo inaainisha kwamba, ni kinyume cha sheria kwa mtu au kampuni yoyote kuuza kwa umma wa Watanzania hisa zake bila kupata kibali cha Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA).*

Mheshimiwa Spika, Kampuni huorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE)* baada ya kutimiza masharti yafuatayo kwa mujibu wa sheria hiyo na Sheria ya *Dar es Salaam Stock of Exchange*:-

(a)Iwe imesajiliwa kama kampuni ya umma yaani *public limited liabitlity company* na iwe na wanahisa wasiopungua saba na wasiopungua hamsini baada ya uuzaji;

(b)Iandae na kuwasilisha kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Waraka wa Matarajio (*prospectus*) ambao unatoa taarifa za kina za kampuni kwa uwazi na zitakazomwezesha mwekezaji pamoja na washauri wake kuwekeza au la. Sharti hili linahusu pia Makampuni yaliyokwishauza hisa kwa umma;

(c)Iwe na historia ya utendaji mzuri inayoambatana na hesabu zilizokaguliwa na kipindi kisichopungua miaka miwili au mitatu kutegemea ngazi ipi ya soko kampuni inataka kuorodheshwa;

(d)Kuwepo na menejimenti yenye wataalam wenye uzoefu wa kusimamia shughuli za uendeshaji wa biashara ambayo Kampuni ile inafanya.

(e)Iwe na mtaji uliolipwa (*paid up capital*) usiopungua shilingi milioni hamsini (50,000,000);

(f)Wanahisa wasipungue elfu moja na wawe wanamiliki si pungufu ya asilimia ishirini na tano ya mtaji wote wa kampuni;

(g)Kuwa na historia ya kupata faida na kulipa gawio.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hakuna hatua zozote za kisheria zilizokwishachukuliwa na Serikali au Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kampuni yoyote iliyoorodheshwa kwenye soko la hisa kutokana na kutoa mwelekeo (*prospectus*) wa uwongo kwa kuwa hakuna kampuni hata moja iliyobainika kufanya hivyo.

(b)Mheshimiwa Spika, hakuna wizi wa fedha za wananchi, uliotokea katika kununua hisa za kampuni ya *TOL*. Kilichotokea ni upande wa pili wa taswira ya masoko ya hisa na dhamana. Makampuni yanayoorodheshwa katika Soko la Hisa yanaweza kupata hasara licha ya matarajio yao kuonyesha yatapata faida. Hali hii inapotokea wanahisa kama wamiliki halali hubeba hasara iliyotokea.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua kadhaa kuisaidia kampuni ya *TOL* ikiwa ni pamoja na:-

- Serikali kushiriki kikamilifu katika toleo la hisa za upendeleo kwa wanahisa waliopo na kununua jumla ya hisa 18,153,107 kati ya hisa 20,765,445 zilizotolewa.

Fedha hizo zilitumika kupunguza deni la kampuni kwa mabenki na hivyo kuzuia hatari ya kampuni hiyo kufilisiwa.

-Serikali ilishiriki katika juhudi za kumtafuta mwekezaji mhimili (*strategic investor*) ili aweze kuwekeza na kuendesha Kampuni kitaalam. Mnamo Januari, 2005, Serikali ilisaini Mkataba wa kuuza asilimia 60 ya hisa za *TOL* kwa kikundi cha Watanzania kinachoshirikiana na *SweedFund International AB* ambaye sasa ndiye mwanahisa mwenye hisa nyingi katika kampuni. Hivyo sasa hivi umiliki wa hisa katika Kampuni hiyo ni kama ifuatavyo:-

- *SAAMI Holdings Ltd & SweedFund* 60% Serikali ya Tanzania 11.14% Wanahisa wengine 28.86%

- Hadi kufikia Machi, 2005, ilikuwa imelipa madeni yote ya ya *East African Development Bank* na *PTA* na hivyo kusafisha mizania ya *TOL*.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri hasa kwa kuzingatia jinsi Serikali ilivyoingilia na kusaidia. Lakini walionunua hisa zaidi ya miaka karibu kumi mpaka sasa hivi hawajapata gawio na Serikali imekiri kwamba kumekuwa na hasara. Je, wale kama watu ambao kulikuwa na sheria iliyoweka na Mikataba kwa maana ilivunjika, wale watu wanasaidiwaje kwa sababu Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu kulipa madeni ya benki peke yake, wale waliweka hisa wanasaidiwaje?

Mheshimiwa Spika, la pili, nilikuwa nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri hiyo kampuni kwa sasa baada ya kusaidiwa je, ina uwezo wa kuanza sasa kutoa gawio kwa watu waliowekeza hisa zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba matarajio kwa kila mwekezaji siku zote ni kwamba watapata faida na watoe gawio na ile ni *risk* ambayo yule mwenye hisa amechukua. Kwa hiyo hapa hakuna suala la kwamba watasaidiwaje, Serikali imeshatoa msaada kwa kuhakikisha kwamba imeuza asilimia sitini na kulipa madeni ya benki yaliyokuwepo ili hii Kampuni ya TOL iweze kujirekebisha na kwenda kwa mwendo unaostahili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni baada ya hapo utakapofika wakati kwamba wame-*take off,* kampuni hiyo italipa gawio kwa mujibu wa taratibu za utoaji wa gawio wa kampuni zilizoandikishwa *DSE.*

Na. 116

**Ujenzi wa Barabara ya Kyaka**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI** aliuliza:-

Kwa kuwa matokeo ya sensa ya watu ya mwaka 2002 imeonyesha Wilaya ya Karagwe inaongoza kuwa na idadi kubwa ya watu katika Mkoa wa Kagera na kwa kuwa Wilaya hiyo inaongoza pia kwa uzalishaji wa kahawa, ndizi, mahindi na maharage; na kwa kuwa moja ya vigezo katika kupanga fedha za miradi ya maendeleo ni pamoja na wingi wa idadi ya watu na shughuli za kiuchumi:-

(a)Je, Serikali ipo tayari kujenga barabara ya Kyaka hadi Bugene yenye urefu wa kilomita hamsini kwa kiwango cha lami?

(b)Kama Serikali iko tayari kufanya hivyo: Je, ni lini ujenzi huo utaanza?

(c) Kama haiko tayari kujenga barabara hiyo, ni kwa sababu gani hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya ya Karagwe ndiyo Wilaya pekee Mkoani Kagera ambayo ardhi yake haijaguswa na lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa barabara ya kutoka Kyaka hadi Bugene yenye urefu wa kilomita 59. Wizara inatambua pia umuhimu wa Wilaya ya Karagwe katika kuzalisha mazao mbalimbali ya chakula na biashara. Barabara ya Kyaka –Bugene ndiyo kiungo pekee cha kusafirisha mazao haya toka Karagwe hadi barabara kuu ya Mutukula-Bukoba na baadaye katika bandari ya Bukoba na Kemondo. Kwa kuzingatia haya, Serikali imekuwa inatilia mkazo matengenezo ya barabara hii. Barabara hii katika mwaka 1998, ilifanyiwa ukarabati mkubwa sana kupitia mradi wa *Core Rural Roads Rehabilitation Programme* (CRRP) kwa gharama ya sh. 791,639,205.50, baada ya hapo barabara inaendelea kupata matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya muda maalum. Katika mwaka wa fedha 2004/05, sehemu ya barabara hii kuanzia Kayanga-Omurushaka yenye urefu wa kilomita 10 inajengwa kwa kiwango cha lami nyepesi (*Otta Seal*), hivyo si kweli kuwa Wilaya ya Karagwe haijaona lami.Aidha, ujenzi wa barabara yote kwa kiwango cha lami utategemea uwezo wa Serikali utakaotokana na ukuaji wa uchumi. Kwa sasa hivi mpango huo haupo.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Wilaya hiyo inazalisha na kwa mujibu wa idadi ya watu ni wengi na kwa kuwa anakiri kwamba hawajaweka lami na hapa anataja lami nyepesi ambayo haipo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Wilaya ile ambayo inazalisha zaidi ya milioni hamsini za fedha za kigeni kwa kupitia kahawa inawekewa lami na wala sio maneno ya kusema walitengeneza kwa kiwango cha changarawe?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa kuna usemi watu wanaozunguka huko Jimboni Kyerwa wanasema kwamba, barabara za Karagwe hazitengenezwi kwa sababu kuna Mbunge kutoka Upinzani. Je, Mheshimiwa Waziri anataka kusema kwamba barabara inayoanzia kwenye Jimbo la *Sir* George haitengenezwi kwa lami kwa sababu kuna mimi kule Kyerwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua. Wakati Mheshimiwa Mutungirehi anazungumzia Jimbo lake halina lami, pia kuna Mikoa kadhaa katika nchi hii haina lami kabisa. Kwa hiyo mpango wa Wizara ya Ujenzi ambao ni mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba inapofika mwaka 2012, Makao Makuu ya Mikoa yote yawe yameunganishwa kwa lami kwanza kabla hatujakwenda kwenye Wilaya.

Zile Wilaya ambazo kwa bahati zimepata lami basi ni bahati yao, lakini tunaomba zile ambazo bado pamoja na yangu zistahilimi ili tuweze kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote kwa lami. Kwa hiyo kusema kwamba sasa hivi tutoe tamko kwamba barabara hii itatengenezwa kwa lami tamko hilo halipo kama nilivyosema katika jibu langu la awali.

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba barabara hii haitengenezwi kwa lami sababu kuna Mpinzani sidhani kama huo ndio msimamo wa Serikali na sio msimamo wa Wizara ya Ujenzi, kwani ukisema hivyo basi huko Tabora na Sumbawanga kote kuna Wapinzani tupu maana yake hakuna lami kabisa hata Makao Makuu ya Mikoa.

Lakini mimi nafikiri ni suala la kupanga ni kuchagua tu, wapi tutafanya nini kwanza.

Na. 117

**Mizani ya Kupima Uzito wa Magari Makubwa**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mizani ya kupima uzito wa magari makubwa Kibaha imewekwa ili kudhibiti magari yanayobeba mizigo kuliko uwezo wa barabara zeti ili kuzinusuru barabara hizo zisiharibike na kwa kuwa kituo hicho sasa kinasababisha msongamano mkubwa na misafara ya magari yote (ya mizigo na ya kawaida) kuendelea na safari zake; na kwa kuwa, msongamano huo hutokea nyakati za usiku kuanzia saa mbili hadi saa nne usiku kwa sababu mbalimbali kama vile njia nyembamba, watumishi wa mizani kuchukua muda mrefu kupima gari moja, baadhi ya madereva kutofuata utaratibu, askari wanaopangiwa kazi sehemu hizo huzidiwa na kazi au wanabaki kwenye mizani tu na kadhalika:-

(a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kumaliza kabisa kero hiyo?

(b) Je, kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuwazuia wenye magari (*owners*) kufika kwenye mizani kabla ya magari yao kuifikia mizani ili kupunguza vurugu ambazo sasa zimekuwa kero za kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mizani iliyopo katika barabara zetu hutumika kudhibiti uzito wa magari ili kulinda barabara zetu kutokana na uharibifu unaosababishwa na magari yanayobeba mizigo mizito kinyume na inavyoruhusiwa kisheria. Magari yanayostahili kupima hupimwa kadri yanavyofika kwani mizani hufanya kazi kwa masaa 24 na kila gari huchukua muda wa kati ya dakika moja na dakika tatu kulingana na ukubwa wa gari hilo katika upimaji.

Katika kudhibiti mapato yanayotokana na mizigo inayopita katika Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi za jirani, Mamlaka ya Mapato *(TRA,* imejiweka utaratibu maalum wa kufuatilia mwenendo wa magari yanayobeba mizigo hiyo yakiwa humu nchini ili kuhakikisha kwamba mizigo hiyo inapita katika vituo muda uliopangwa inapokwenda nchi husika ili kudhibiti ukwepaji wa kodi.

Kwa kupitia kitengo chake cha *Transit Goods Control Unit*, Mamlaka hiyo imeweka muda maalum wa magari hayo kuondoka Dar es Salaam na kutoa taarifa katika vituo vya Chalinze, Makambako na vituo vinginevyo vilivyowekwa maalum kwa kazi hiyo. Magari yote yanapaswa kuwa yameondoka Dar es Salaam ifikapo saa moja jioni. Kutokana na utaratibu huu magari mengi yanafika Kibaha kati ya saa mbili na saa nne usiku na hivyo kusababisha msongamano katika mizani ya Kibaha.Baada ya maelezo hayo juu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imeishaliona tatizo hilo na imeanza kulifanyia kazi kama ifuatavyo:-

•Wizara yangu kupitia kwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* inawasiliana na Mamlaka ya Mapato kuona kama magari yanayosafirisha mizigo ya nje yakamilishe taratibu muhimu kama inavyotakiwa kisheria na hivyo kuanza safari na kufika mizani ya Kibaha mapema.

•Ikiwa itashindikana kubadilisha muda ili magari yanayokwenda nje kuondoka Bandarini mapema, Wizara itafanya mpango wa kuongeza urefu wa njia *approaches* za kuingia kwenye mizani ili kutenganisha magari yanayotakiwa kupimwa na yasiyotakiwa kupimwa na/au kununua mizani ya kupima na kuchambua magari yakiwa kwenye mwendo *Weigh in Motion* ili magari yaliyozidisha uzito tu ndiyo yapite na kupimwa kwenye mizani iliyopo kwa hivi sasa.

(b)Utaratibu umeshafanywa wa kuzuia wenye magari kusogelea kwenye mizani kabla ya magari hayo hayajafika kwenye mizani. Hii ni pamoja na kuweka walinzi ambao wanazuia wenye magari na wafanyabiashara ndogo ndogo kusogelea eneo la mizani.

Pia Ofisi ya Mizani ya Kibaha imefanya matengenezo yenye lengo la kurekebisha utaratibu uliokuwepo wa wenye magari kuingia ndani ya ofisi. Kwa sasa taratibu zote zinafanyika nje ya jengo la ofisi ili kuondoa msongamano wa wenye magari ndani ya ofisi hiyo, ofisi yenyewe bado ni ndogo.

**SPIKA:** Muda uliobaki unatosha swali moja tu, kwa hiyo nampa Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa.

Na. 118

**Hospitali ya Muhimbili**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Muhimbili ni Hospitali pekee ya Rufaa nchini:-

(a)Je, hospitali hiyo ina wataalam wangaqpi wenye sifa ya upasuaji *surgeons*?

(b)Je, hospitali hiyo ina utaratibu gani wa kuwatibu wagonjwa mahututi hasa waliopata ajali huku wakiwa hawana wadhamini?

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimwia Mossy Mussa, Mbunge wa Mfenesini, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Muhimbili siyo hospitali pekee ya Rufaa hapa nchini. Pamoja Hospitali ya Taifa Muhimbili ziko pia hospitali nyingine za Rufaa tatu na hospitali nne maalum.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Mussa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Hospitali ya Muhimbili ina jumla ya Madaktari wapasuaji 20 kati ya hao 12 ni Walimu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Jamii na waliobaki ndiyo wanafanya kazi muda wote pale Muhimbili.

(b)Wagonjwa mahututi hasa wanaopata ajali hupata huduma kutoka kwa Madaktari wa Idara ya Upasuaji au Madaktari wa mifupa na mishipa ya fahamu ambao wako katika Taasisi ya MOI au Madaktari Bingwa wa Idara nyingine yeyote kufuatana na sehemu za miwili alizoumia mgonjwa. Mgonjwa mmoja huweza kupata huduma

kutoka kwa Madaktari Bingwa zaidi ya mmoja wa Idara moja au zaidi kwa ushirikiano kufuatana na majeraha ya mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, mgonjwa huwa chini ya uangalizi wa Daktari Bingwa mmoja ambaye anakuwa zamu siku mgonjwa anapolazwa. Wagonjwa wote mahututi na waliopata ajali hupata huduma za kitaalam hata kama hawana wadhamini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mossy Mussa samahani, muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, sasa tunaendelea na ajenda nyingine na kwa leo hakuna matangazo ya vikao vilivyoandaliwa. Kwa hiyo, tunaendelea moja kwa moja na *Order Paper,* Katibu endelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006
### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii niwe mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaamu za rambirambi zangu kwa msiba ambao ulitokea hivi karibuni wa Mheshimiwa Mbunge wa Kilombero, Mungu ailaze roho ya marehemu Abu Kiwanga mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya salaamu za rambirambi hizo. Napenda pia niendelee kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kuchangia.

Kwa vile leo ni mara yangu ya kwanza kuchangia toka Bunge hili la Bajeti la mwaka huu limeanza. Naomba na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wa Urais kupitia tiketi ya CCM na Mungu atasaidia atapata kura za kishindo na atakuwa Rais wa nchi hii.

Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuteuliwa kwake kuwa mgombea mwenza. Nimpongeza Mheshimiwa Rais Amani Abeid Karume kwa kusimamishwa kuwa mgombea kupitia tiketi ya CCM katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, *Inshallah* Mungu atamsaidia ushindi wa kishindo tutaupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa hotuba yake nzuri na hotuba yenye mwelekeo wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ambazo huwa zina maswali mengi ni Wizara hii ya TAMISEMI haipiti siku tatu ama wiki bila kupata hoja ama swali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Ni Wizara yenye mambo mengi na ni Wizara inayogusa wananchi. Lakini kutokana na busara za Mheshimiwa Waziri wakishirikiana na Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kweli wamekuwa wakitusaidia sana kuweza kutatua matatizo mbalimbali ambayo tumekuwa tukiwapelekea. Kwa hiyo, mimi nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa na kuwatia moyo waendelee na kazi hiyo ili kuinua nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo na kwa vile nimesema kwamba kazi nzuri imefanywa. Mimi nina mambo matatu tu ya kuzungumza. Kwanza, nitazungumzia suala la barabara, lakini pia nitazungumzia suala la hospitali na nitamalizia na suala la mikopo hususan mikopo ya akinamama na vijana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri ambayo nimesema kwamba yamefanywa na Wizara ya TAMISEMI. Mimi nichukue nafasi hii kuipongeza sana Halmashauri yangu ya Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi ambacho mimi nimekuwa Mbunge kwa kweli Halmashauri ya Temeke imekuwa ikifanya kazi nzuri chini ya uongozi wa Mkurugenzi Ndugu yetu Iddi Nyundo, wamefanya kazi nzuri sana na maendeleo mengi yamepatikana. Isingekuwa vyema nianze kurudia ambayo nilikwishayazungumza kwamba sisi katika mambo ya kihistoria ambayo tumeweza kuyajenga ni jengo kubwa la Halmashauri yetu ambalo kwa nchi nzima Halmashauri ya Temeke imeonyesha mfano. Kwa hiyo, hiyo ni mojawapo na yapo mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nitazungumzia suala la barabara. Wilaya ya Temeke ina tatizo kubwa la barabara. Tuna barabara chache tu ambazo zimeweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Lakini barabara nyingi hazijatengenezwa na kwa kweli ni mbaya sana sana. Sasa kutokana na mapato ya Halmashauri yetu tumejitahidi kwa kiasi fulani tumeweza kutengeneza barabara, kwa kipindi cha miaka mitano tunayo barabara angalau ya lami tumeitengeneza kwa kutumia mapato yetu. Katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 tuliweza kutenga fedha tukatengeneza barabara ya lami ambayo inatokea *Veterinary* kupitia Mwembeyanga hadi Tandika.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi kuipongeza sana Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, chini ya uongozi wake Mheshimiwa Waziri Hassan Ngwilizi, waliweza kuchangia kiasi kikubwa cha fedha ili ziweze kuongezewa na zile za kwetu tukaweza kuitengeneza barabara hiyo. Hili kwa kweli tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini tunayo matatizo makubwa kwenye barabara sasa zinazokwenda kwenye Kata zetu mbalimbali. Barabara ambayo nimelenga kuizungumzia ni hii barabara inayotokea Devis Kona kupitia Yombodovya kuelekea Makangarawe.

Mheshimiwa Spika, barabara hii toka nimekuwa Mbunge nimeikuta iko kwenye hali mbaya sana. Lakini kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo hayo tuliweza kuishawishi Halmashauri na tukatenga fedha ili angalau tuweze kuitengeneza kwa kiwango cha moram kwa sababu mapato yetu ni kidogo na Wilaya ni kubwa kwa hiyo tunagawanagawana. Sasa kwa Bajeti ya mwaka jana 2004 tuliweza kuitengeneza barabara ile kwa kiwango cha moram.

Mheshimiwa Spika, kiwango kile tulichotengeneza barabara ile ukifika sasa hivi utakuta barabara hii kana kwamba haikuwa imefanyiwa chochote imeharibika kwa haraka sana sana kutokana na mvua ambazo zimekuwa zikinyesha mfululizo.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwamba fedha ambazo tulikuwa tumetenga zililenga kutengeneza barabara tu, sasa hatukuwa tumefikiria kutenga fedha kwa ajili ya kutengeneza mifereji. Kwa sababu wataalam wa ujenzi wataweza kunisahihisha, tunapotengeneza barabara bila kuitengenezea mifereji ambapo maji yatakuwa yakipita na kumwagwa pembeni kwa kweli uimara wa barabara hiyo utakuwa siyo mzuri.

Sasa hili ndilo ambalo limetukuta sisi, tumetumia fedha kutengeneza barabara, lakini haikuchukua muda ambao tulitarajia na bado imeharibika vibaya sana sana.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilikuwa naomba ili kuweza kutusaidia nguvu zetu za Halmashauri tulizowekeza pale zisipotee bure. Nilikuwa naiomba Wizara ya TAMISEMI angalau sasa itusaidie kutuongezea fedha ili barabara hii tuitengeneze kwa kiwango cha lami na ikiwezekana basi niliwahi kuzungumza kwenye mkutano wa Mheshimiwa Makamba katika mkutano wake wa barabara kwamba pale wanapoamua kwamba wanachukua barabara hii kuitengeneza, basi sisi tutoe mapendekezo yetu kwamba ni barabara ipi. Kwa hiyo, Mfuko ule wa Barabara wa Mkoa niliwaomba sana wao waichukue barabara ile ili waweze kuitengeneza mifereji ambayo sisi Halmashauri hatukuwa na uwezo wa kuitengeneza. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba pia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itusaidie sasa sisi tuliitengeneza kwa kiwango cha *moraine* lakini na Wizara nayo itusaidie ili angalau tuweze kuiwekea lami katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo lingine katika barabara ile ile tumetengeneza baadhi ya sehemu tu, sehemu nyingine ilishindikana kwa sababu kulihitajika fedha nyingi kwa ajili ya kutengeneza mifereji. Lakini lilikuwepo tatizo la wananchi kuwepo pale nyumba karibu nane walikataa kuhama kwa sababu walikuwa wameahidiwa huko nyuma kwamba watalipwa.Nichukue nafasi hii kuipongeza Halmashauri yangu ya Temeke tumetenga fedha kwa ajili ya kuwalipa ili waweze kutoa nafasi na tutatengeneza mfereji ambao uko *Devis* kona ambao umekuwa ukisumbua na unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni ndefu kuanzia *Devis* kona inaelekea Makangarawe, lakini ile barabara tulitengeneza nusu tu baadhi ya sehemu tuliibakisha. Sasa sehemu ile iliyobaki bado mimi ninaomba Serikali itusaidie ili tuweze kuimalizia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kulizungumzia hili. Sasa naomba nizungumzie suala la pili ambalo ni suala nzima la mikopo ya akinamama. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwenye ukurasa wa 30 ameelezea na ametupongeza kwa kweli Mkoa wa Dar es Salaam tumejitahidi sana kuweza kuelekeza na kutoa kibali ili madeni ambayo yalikuwa yanadaiwa basi tuwape watu waweze kutudaia na kwa kweli tumefanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nizungumzie upande wangu wa Halmashauri ya Temeke pamoja na kuwapa Mawakala wadai mikopo hii, lakini nilikuwa naomba Mawakala hao, basi wawe na lugha nzuri ya kuwafuata akinamama kuwadai hii inawadhalilisha sana, akinamama wanapekuliwa kwenye magodoro yao, wanapekuliwa kwenye makabati yao ili waweze kutoa nguo angalau ziuzwe kwa ajili ya kufidia mikopo ambayo walikuwa wamechukua. Sasa hii mimi nafikiria tunaongeza umaskini ama tunapunguza umaskini? Kwa sababu wamefikia mahali pa kutohitaji tena mikopo hii ya Halmashauri kutokana na unyanyasaji jinsi ya kufuatilia mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wazo hili ni nzuri. Nakumbuka kabisa wenzetu *LAAC* waliwahi kushauri kwamba tuweke Mawakala, lakini basi Mawakala hao wawe na utaratibu mzuri wa kudai. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana tusiwakatishe tamaa akinamama, hao Mawakala wadai kwa nidhamu zote na wasiwafikishe Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine tulielekeza kwamba watakapokuwa wanadai fedha hizo wasiziweke kwenye mabenki tu bali waendelee kutoa mikopo. Hayo yalikuwa ni mapendekezo yangu.

Mheshimiwa Spika, nilisema nitazungumzia suala la hospitali. Wilaya ya Temeke imepanuka na ni ya pili katika ongezeko la watu. Ninaishukuru sana Serikali yetu sasa hivi hospitali ya Temeke inakarabatiwa jengo la utawala ambalo lilikuwa limeungua linajengwa. Sasa ombi langu ni kuongeza zahanati kwenye Kata mbalimbali. Tunalo tatizo Kata ya Keko na Chang'ombe ambapo tulikuwa tumependekeza kwenye eneo moja tungeweza kujenga zahanati.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo tatizo sana la baadhi ya watu kutumia vile viwanja ambavyo tulikuwa tumevipendekeza wao kuviomba kwa ajili ya kuweka labda *Petrol Station* na kadhalika. Sasa nilikuwa naomba sana na ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kama kutakuwa na maombi hayo kwenye mujumuiko wa watu, mtu anaacha kutoa kibali kwa ajili ya ujenzi wa zahanati anatoa kibali kwa ujenzi wa *Petrol Station*, basi nilikuwa naomba hili alisitishe, tunalo tatizo kubwa kabisa la kiwanja pale Keko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale sisi tulifikiria kwamba tungeweza kuweka zahanati, lakini mtu mmoja mkubwa amekwenda kupewa kibali kwamba kiwanja ni cha kwake na anatarajia kuweka *Petrol Station* wakati *opposite* na kiwanja kile pia kuna *Petrol Station*. Kwa hiyo, mimi hili nilikuwa naomba kabisa lisitishwe ili Serikali iangalie kuwapa wananchi waweze kujenga zahanati kwa ajili ya Kata hizi mbili. Tukijenga zahanati hiyo itasaidia kupunguza msongamano ambao upo katika hospitali yetu ya Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimesema hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni nzuri na wala sikuwa na mengine mengi ya kuzungumza yalikuwa ni hayo matatu. Ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, lakini kwanza kabisa kama wenzangu walionitangulia naomba na mimi nijumuike nao kutoa salaamu za rambirambi zangu kwa familia za Waheshimiwa Wabunge ambao tumewapoteza kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa na Chama chetu cha CCM kuwa mgombea wa Urais kwa tiketi ya CCM. Pia mgombea mwenza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na pia Mheshimiwa Rais Amani Karume kuwa mgombea wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa tiketi ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, ninaomba na mimi nimpongeze na kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alisema harudi tena Bungeni. Namtakia yeye mwenyewe na familia yake maisha mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada hapo, naomba sasa nipate nafasi hii kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brig. General Hassan Ngwilizi na Naibu Waziri wake na Ndugu Mmari, Katibu Mkuu katika Wizara hiyo kwa hotuba nzuri sana kuhusu mapendekezo na maombi yake ya bajeti kwa kipindi cha mwaka wa fedha kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitamke kabisa kwamba naunga mkono hoja hii. Lakini kabla sijaenda mbele sana naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Wizara ya TAMISEMI kwa kutusaidia wana- Kinondoni kutujengea daraja la kuiunganisha Tandale na Mwanyamala. Daraja hilo ni la kisasa ambalo litasaidia sana watu wanaotoka Kata za Ndugubi, Tandale, Manzese na sehemu zingine kupita kwenye daraja hilo kwenda kwenye matibabu katika hospitali Mwanyamala. Lakini pia kwa upande wa wananchi wa Kata za Hananasifu, Mwanyamala, Kinondoni, kwenda kununua bidhaa zao kwenye soko la Tandale. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa msaada huo na wananchi wamesema nitoe shukrani zangu kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie matatizo ambayo yapo kwenye Jimbo langu. Naelewa kabisa kwamba hiki ni kipindi cha mwisho cha Bunge hili. Kwa hiyo,

huenda Serikali isifanye lolote, lakini naomba ichukue haya maombi kama kumbukumbu kwa kipindi kinachokuja ili yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, bado tuna matatizo mengi sana kuhusu maji katika Kata zifuatazo:- Tandale, Kigogo, Muzimuni, Ndugumbi, Hananasifu na Kinondoni. Sasa nashukuru kwanza kwamba hao wenzetu *City Water* waliondolewa na kama Mheshimiwa Waziri atakumbuka katika mchango wangu mwaka jana walipokuwa wanapewa *contract* hao watu wa *City Water* nilisema tunasikia kwenye magazeti kwamba watu hao hawafai kabisa, lakini Serikali ikawatetea.

Lakini nashukuru kwamba Serikali yenyewe sasa imegundua kwamba kwa kweli watu hao walikuwa hawafai kufanya hiyo kazi. Sasa ni mategemeo yetu basi kwamba hao wananchi waliopewa kuendesha *DAWASA* basi wataelekeza nguvu zao katika maeneo haya ili maji safi na salama yaweze kupatikana katika maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo mimi kidogo nimesikitishwa kwamba tunaendelea kuwabana akinamama na vijana kwamba hatuwezi kuwapa mikopo kwa sababu wenzao huko nyuma hawajarejesha mikopo hiyo. Sidhani ni jambo la busara kuwapa adhabu watu ambao hawajahusika na kutokurejesha hiyo mikopo. Ningependekeza kwamba hao Mawakala waliopewa hiyo kazi, kwanza namuunga mkono Mheshimiwa Hadija Kusaga kwamba watumie lugha nzuri kuwadai hao ambao hawajarejesha hiyo mikopo. Lakini pia wale ambao hawajapata mikopo wafikiriwe kupewa mikopo hiyo na ile asilimia 10 iendelee kutengwa kwa madhumuni hayo hayo kwamba akinamama na vijana wapate hiyo mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala dogo la mabwawa ya Msisiri haya yamekuwa ni mwiba katika sehemu zetu kwa muda mrefu sana. Lakini nashukuru kwamba sasa hivi mabwawa ya Msisiri yanashughulikiwa na Shirika lisilo ya Kiserikali liitwalo *CARE* ambalo limejitolea kusaidia kutatua hili tatizo.

Lakini wanahitaji wananchi kuchangia asilimia 10 ambayo ni fedha nyingi sana. Tungeomba Serikali itusaidie kwa sababu Manispaa yenyewe haina uwezo wa kusaidia kutokana na makusanyo yake kuwa hafifu sana. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itusaidie kutupatia hizo fedha asilimia 10 ili hawa *CARE International* waweze kutusaidia tumalize hili tatizo la mabwawa ya Msisiri.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la zahanati ya Kigogo. Zahanati hii ilijengwa na Manispaa lakini bahati mbaya sana mpaka hivi sasa tunashindwa kupata matibabu kwa masaa 24 na bahati mbaya sana Kigogo ni sehemu mojawapo ambayo wakati wa mlipuko wa kipindupindu basi sehemu hii inaguswa sana na hili tatizo.

Kwa hiyo, tungeomba zahanati ya Kigogo ambayo sasa hivi inafanya kazi, lakini inafanya kazi kwa masaa 12, tungeomba sana Waganga wapatikane pale ili waweze kufanya kazi kwa masaa 24 kuondoa tatizo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nikigusia na hilo, kwa kipindi kirefu sana hapa Bungeni Mheshimiwa Waziri wa Afya, amekuwa akisema mara kwa mara kwamba watoto chini ya miaka mitano, wazee na akinamama wajawazito wapatiwe matibabu bure wale wasiojiweza, lakini ukweli ni kwamba mpaka leo hii bado tatizo hilo lipo. Akinamama wananyanyaswa, wazee wananyanyaswa na watoto pia hawapati matibabu hayo. Kwa hiyo, naomba Serikali itafute jinsi ya kudhibiti hali hii ili kuhakikisha kwamba hao wazee, watoto na akinamama wajawazito hawapati matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linahusu hali ya kusikitisha na hatari kidogo nalo ni sehemu ya Kigogo ambayo kwa sasa hivi kuna mmomonyoko unaotishia kuigawa Kata hiyo katika sehemu mbili. Huko nyuma niliwahi kuchangia kwa maandishi kuomba wataalam waende katika maeneo hayo. Eneo linaloanzia kwenye Mto Msimbazi unaotokea maeneo ya SUKITA kuja sehemu za Jangwani katika maeneo hayo huo mto umekuwa ukigeuza njia yake mara kwa mara na niliomba kwamba Serikali ipeleke wataalam ili kuweza kudhibiti hali hiyo. Kwa hiyo, naomba tena Serikali ijaribu kuliangalia hili na kuzuia mmomonyoko ambao unaweza kusababisha maafa na kugawa Kata ya Kigogo katika maeneo mawili. Naomba sana kazi hiyo ifanyike.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwamba mafuriko ambayo yanatoka kwenye viwanja vya Biafra kuelekea maeneo ya Kinondoni Shambani mpaka kwa Binti Matola maeneo haya ni *squatter area.* Kuna fedha zinahitajika hapo.

Lakini kama nilivyosema kwamba tangu tumepunguza au tumefuta ada mbalimbali za kodi Manispaa ya Kinondoni imekuwa na uwezo mdogo sana wa kuweza kukusanya fedha ili kushughulikia hili suala. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itusaidie itupe fungu maalum ili tuweze kuondoa adha hii kwa wananchi wa Kinondoni Shamba. Naomba sana Serikali ilitazame hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la mifereji kujengwa na kusafishwa mara kwa mara. Katika swali langu hapa Bungeni niliuliza hivi, hizi kodi za majengo kazi yake ni nini? Na nikajibiwa kwamba kazi yake au moja ya kazi yake ni kutengeneza mifereji ya maji machafu, lakini kwa Jimbo la Kinondoni hili halifanyiki. Kwa hiyo, naomba kwa kweli Serikali itusaidie kuliweka hili sawa. Kuna maeneo mengi sana ambayo mifereji haitakiwi kuwa imejaa na kuwa michafu kama ilivyo katika maeneo ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia kuhusu kodi za majengo kwa wazee, nakumbuka Mheshimiwa Waziri alisema hapa kwamba kwa wazee ambao wanaishi kwenye nyumba za tope au mtu yeyote yule hastahili kulipa kodi ya majengo.

Lakini pia kuna wazee ambao wana vibanda vyao, wanakodisha nyumba zao lakini uwezo wa kulipa kodi ya majengo hawana uwezo kabisa kwa sababu kipato chako hakizidi shilingi 60,000/= ukimwambia alipe shilingi 10,000/= unakuwa unamnyima uwezo wa kuishi katika hali nzuri. Kwa hiyo, awali tuliomba kwamba wazee ambao watabainika kwamba kipato chao pamoja na kwamba wanapata katika pango basi kipato chao hicho kisiwalazimishe kulipa kodi za majengo wasamehewe. Naelewa kwamba Manispaa ina uwezo huo wa kusamehe basi itoe msamaha.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa kuhusu malipo ya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa pamoja na Afisa Watendaji wa Mitaa. Ninavyokumbuka mimi tangu nimeingia humu ndani Bungeni mwaka 1995 naambiwa na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kwamba hawajawahi kulipwa ile asilimia 3 mpaka leo hii. Na hivi juzi nafikiri mapema mwaka huu Mheshimiwa Naibu Waziri alituambia kwamba Halmashauri zimeelekeza kuwalipa hao watendaji, lakini ukweli ni kwamba mpaka hivi sasa hawajalipwa.

Inawezekana tena ni kwa sababu Manispaa haina uwezo mzuri wa kukusanya fedha, basi Serikali iingilie kati iwasaidie, kwa sababu kwa kweli wanaadhirika vibaya sana hao watendaji. Na ndiyo maana kuna malalamiko kwamba huwa wanadai fedha za kuandika barua za kutoa dhamana, mtu analipishwa shilingi 2,000 ambayo wananchi wanaona ni adha sana.

Kwa hiyo, tukiwapa mshahara nafikiri hii itasaidia kuondoa kero hii. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, langu la mwisho, ni kuhusu Madiwani. Katika mchango wangu nadhani mwaka jana 2004 kwa maandishi nilisema kwamba Madiwani wa Kitanzania siyo kama Madiwani wa nchi za wenzetu zilizoendelea. Nchi za wenzetu Diwani ni mtu mwenye uwezo anaweza kufanya vitu vyake na anajisitiri mwenyewe.

Lakini Diwani wa Tanzania ni mfanyakazi moja kwa moja na nilipendekeza kwamba hiyo posho anayopata ni ndogo mno. Ingependekezwa kwamba kila mwezi wangepata angalau kwenye shilingi 500,000/=hivi na waangaliwe kwamba wanapoondoka pia wanapata *gratuity* ambayo inafaafaa kidogo.

Lakini pia kuweza kupata mkopo wa magari. Naomba Serikali ilitazame hili kwamba Tanzania sio kama nchi zilizoendelea kumfanya Diwani apate kipato kidogo namna hiyo. Diwani wa Tanzania ni mfanyakazi saa zote kwa hiyo afikiriwe kwa maana hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Serikali itusaidie kutupatia fedha za fidia ya Shule ya Mapera ambayo Wizara ya Elimu imeshatupa fedha kujenga hiyo shule lakini kuna nyumba kama tano zinatakiwa kufidia. Manispaa kwa muda wa mwaka mmoja inasema haina hizo fedha za kuweza kulipa fidia. Tunaomba Serikali itusaidie kulipia hiyo fidia ili tuweze kujenga Shule ya Mapera ianze mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba maombi haya yote niliyozungumza hapa Serikali iweze kusaidia ili tuweze kuendeleza Elimu ya Msingi ya vijana wetu. Baada ya kusema haya yote naomba niseme tena kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi hii na napenda kabisa niwashukuru viongozi wa TAMISEMI kuanzia Waziri,

Naibu wake na Katibu wake Mkuu.  Katika Wilaya yangu nimepata bahati ya kuwa na Katibu Mkuu kunitembelea na kuona wananchi wanachofanya.  Kwa kweli namshukuru sana kwa jinsi alivyohamasisha wananchi wa Mbozi hasa kujitegemea na kusimamia maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Wizara hii pamoja na kazi nzuri wanayofanya lakini yapo matatizo ambayo kama Taifa halitayaona hatuwezi kufanikisha mafanikio ya maendeleo tunayoyatarajia.  Wilayani kuna migongano, nafasi ya *DC* na Mkurugenzi sasa hivi hazijawa katika hali nzuri.  *DC* hana utaratibu unaoeleweka wa kuelewa mipango yote ya Halmashauri anawakilishwa na *DAS.*

Sasa mimi sioni sababu,  kwa kuwa *DC* ndiye msimamizi kabisa ilitakiwa awe pale ajue mipango yote ya Halmashauri.  Ahusike katika vikao vya Halmashauri na aweze kudhibiti maendeleo na utaratibu wowote unaovurugika katika Wilaya yake na hii itampa nguvu na kurekebisha yale yanayokwenda tofauti na yale yaliyopangwa.

Mkurugenzi kwa sasa hivi hawezi kuamuliwa na *DC* kwa sababu wote wana ngazi karibu sawa, wote wanateuliwa na Rais.  Sasa nani amthibiti mwenziwe.  Sasa hili mimi nilikuwa naomba kulikuwa na pendekezo miaka hii ya nyuma kwamba Mkurugenzi aajiriwe na Halmashauri nadhani hili lingekuwa jema zaidi.  Mkurugenzi aajiriwe na Halmashauri na asimamiwe na Halmashauri, *DC* aone utekelezaji wa Halmashauri hiyo na aweze kuishauri katika vikao vyao hapo nadhani kutakuwa na hali nzuri ya kufanikisha shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, inakuwa haisaidii *DC* anapoambiwa kwamba Wilaya ina njaa hawakusimamia au haina maendeleo sasa atasemea wapi masuala hayo. Ni afadhali apewe nafasi ambapo atakuwa na nguvu ya kusemea na kutoa mawazo yake na kuagiza na kufuatilia vile vile.  Lakini sasa ni mtu ambaye kwanza hajui ni nini kinafanyika.  Hili nadhani lingetusaidia kama Wizara ingefikiria sana hapo na *DED* awe ni mtu ambaye adhibitiwe na Halmashauri yenyewe na ndipo atakapotii kusimamia maendeleo ya Wilaya ile.

Katika hilo ni kwamba *DC* akiwa bega kwa bega na Madiwani wake wakasimamia shughuli za maendeleo bila matatizo lakini sio kwa hali iliyopo sasa hivi, *DC*  lwake, Mkurugenzi  lwake.  Mara *DC* akisema hili Mkurugenzi inabidi apate kibali cha Madiwani sasa inakuwa ni kama watu wawili ambao hawafanyi kazi moja ya maendeleo ya watu wa sehemu ile kwa manufaa ya watu hawa.  Hili naomba sana Wizara iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, matumizi ya fedha. Ukaguzi unapofika katika Halmashauri haujielezi kwa vikao vya Madiwani makosa au matatizo waliyoyapata. Wanaleta maelezo tu.  Sasa ingesaidia sana kama hawa Wakaguzi wanakuja wenyewe na wanatoa maelezo mbele ya *full council* ili watu wajue kweli matumizi na makosa yaliyotendeka yanawahusu na wafanye nini ili kuyarekebisha.  Kuliko inavyofanyika sasa wanaleta tu maelezo na maagizo.  Kwa hiyo,  inakuwa ni kama kitu hakina nguvu na

Madiwani hawana uwezo wa kupinga pale au kuuuliza kwa sababu anayewakilisha ni yule yule Mkurugenzi ambaye ndiye amekaguliwa.

Kwa namna hii haiwapi Madiwani nguvu ya kuona tatizo la matumizi mabaya ya fedha. Mimi nadhani uamuzi wa kusema kwamba Halmashauri ambayo haikutekeleza au imepata hati chafu inyimwe fedha za maendeleo kwa kweli hili ni kosa la kuadhibu wasiohusika. Kwa sababu Mkurugenzi mmemleta wenyewe, Mhasibu nyinyi wenyewe, wameharibu leo mnatuadhibu sisi wananchi, hii ni dhambi kubwa nadhani Wizara hii ijisahihishe isiendelee na suala hili. Sisi hatuna kosa lolote wenye kosa ni nyinyi mmetuletea mbovu halafu mnatuadhibu juu ya uamuzi wenu wa kuleta ubovu, hapana, hili lisiwepo hata kidogo. Wilaya zote zipewe haki zao na fedha zao ili zifanye maendeleo. Kosa la Watendaji lichukuliwe nidhamu na taratibu zinazotakiwa kama tunavyotaka lifanyike. Vinginevyo hatutakwenda mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda tu ni mfuko huu wa pembejeo. Pamoja na mbolea hii ya ruzuku utaratibu unaotumika hauwezi kutusaidia hata kidogo. Leo pembejeo ziko kwa Waziri wa Kilimo. Waziri wa Kilimo ndiye mwenye mamlaka na hawa Watendaji. Lakini *DED* hana nguvu yoyote ndiyo maana shughuli za *extension* hazipo katika Wilaya. Ndiyo maana maendeleo ya kilimo yanakwama katika Wilaya. Sasa bado wanapata maagizo ya Wizara hatuwezi kwenda hata kidogo. Mimi nadhani hizi pembejeo akabidhiwe *DED* ndiye wa maendeleo ya Wilaya yake. Mimi nasema hizi mbolea za ruzuku Wilayani kwangu hata mkimletea *DED* sisi hatuombi kukopa. Tuleteeni tuna ghala pale kwenye Wilaya. Mleteeni *DED* mbolea yote pale ya ruzuku baada ya siku mbili njooni mchukue fedha watu watakuwa wamenunua hatuhitaji mkopo sisi. Wananchi pale wako tayari kununua mbolea *cash* ya ruzuku kuliko hali hii inavyokwenda. Tunaletewa leo mnapeleka mkoani, mkoa wapange bei ya mbolea ya ruzuku na usafirishaji halafu walete Wilayani, Wilaya Kamati tena nyingine ipange kuwagawia watu wasafirishe mbolea wapeleke Vijijini kwa namna hii hata maana ya ruzuku inakuwa haiko maana kila mtu amepewa faida fulani kutokana na hali ya kusafirisha mbolea pale ilipo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna hii tunapoteza bure na kuua uwezo na nguvu na ari ya kusema kwamba Serikali imetoa ruzuku. Hii mbolea yote ya ruzuku ipelekwe kwa Wakurugenzi, wao wakiitumia vibaya ndio walaumiwe na ndio wenye maendeleo sio Afisa Kilimo. Afisa Kilimo wa Mkoa anakuwa ndiye msimamizi wa kugawa mbolea mkoani anahusika nini na Wilaya. Kwa kweli hili mfanye utaratibu huu muubadili kabisa na Waziri wa kilimo bahati mbaya hayupo lakini mmwambie kazi hii nadhani abakie Wizarani kupanga mipango na kueneza ili Wilaya zibanwe kushindwa kuleta maendeleo au kuwezeshwa kuleta maendeleo. Hatuwezi kupata maendeleo kwa kutumia Wizara au mkoa. Wananchi hawatapata maendeleo itabaki ni hadithi ya Abunuwas tu ya kujenga nyumba hewani na nyumba haionekani. Kama itapelekwa kwa *DED* hata Madiwani watahusika kuona kwamba mbolea hii inafika kwa watu wao na inatumika inavyotakiwa na italeta maana na mafanikio na mtu wa kuulizwa hata na wananchi pale ni Diwani ndiye anayehusika na ndiye atakayewajibu watu kama atavuruga basi wale ndio watamdhibiti kwa kumchagua au kutokumchagua hili ndilo litakuwa lina maana hii.

Mheshimiwa Spika, halafu maendeleo tunayozungumza haya lazima yawe na watu wanaosimamia. Hawa Wenyeviti wa Vijiji wasiposimamia hakuna maendeleo yatakayofanyika. Hivi huyu Mwenyekiti wa Kijiji afanye kazi hiyo au amwachie Mtendaji wa Kijiji *VEO*. Hivi Mtendaji wa Kijiji kweli ataweza kusimamia maendeleo ya Kijiji. Inabidi Mwenyekiti awe pamoja bega kwa bega na Mtendaji. Sasa Mtendaji analipwa, Mwenyekiti halipwi hivi mtu huyu atasimamiaje kazi tangu asubuhi mpaka jioni hajalipwa kitu atakuwa na nguvu gani ya kusimamia. Mimi nadhani hapa tuangalie kwa kweli hatusemi kwamba watu walipwe mishahara iliyowekwa lakini wakipewa kama ahsante hata shilingi 2,000/= wanunue angalau sabuni za kufua nguo zinazochafuka na jasho wanapokuwa kwenye shughuli za kusimamia itakuwa ni heshima kubwa na watafanya kazi hii kwa moyo kuliko sasa kuweka tu watu na kuwakemea, utawakemea nini wakati hawana kitu wanachopata, ni kama kazi ya kujitolea tu hii. Nadhani hapa tuangalie kwa kweli au Serikali ya Kijiji iwe na kifungu fulani cha kuweza kumpa huyu Mwenyekiti angalau posho aweze kufanya kazi kwa moyo na wakati mwingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ningependa nishukuru huu Mpango wa Barabara Vijijini *(VTTP)*. Mimi ninaushukuru sana katika Wilaya yangu na katika jimbo langu, umetusaidia sana wananchi wamekwishaelewa, sisi katika maeneo mengi katika Wilaya yangu ukiwauliza watu waeleze juu ya *grader* hawajawahi kuliona. Sasa leo unawaambia barabara zilimwe watalimia nini. Wameamua wananchi kulima barabara kitu wanachokiomba ni msaada wa kujengewa madaraja. Ninashukuru kwamba Katibu Mkuu wa Wizara hii alifika akaona barabara walizolima wananchi na madaraja wanayojengewa yameleta mafanikio makubwa sana. Ningeomba utaratibu huu kwa kweli uendelezwe na upewe nguvu ili watu waweze kujiletea maendeleo ya mawasiliano vijijini na hii itasaidia sana mabadiliko ya huko vijijini. Nawashukuru sana kwa wale waliotoa msaada huu na wahisani hawa naomba sana katika Wilaya yangu watusaidie na waongeze misaada hii ili tuweze kuondoa tatizo la usafiri katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Wilaya yetu iliomba mkopo kwenye Wizara ya TAMISEMI kulikuwa na mikopo ili iweze kufanya angalau pale Wilayani tuondoe vumbi kidogo lakini hatukupata. Lakini Katibu Mkuu alifika akaahidi sasa bahati nzuri leo yupo nadhani hili suala hata wakati wa kujibu ataeleza kuwa sasa wanaliangalia. Sisi angalieni hata mikopo yote ya Halmashauri hatuna deni pale Wilayani tumerudisha yote. Sasa hili tulilolombea tunaomba mlitazame kwa nia na moyo wa kuweza kuendeleza shughuli hizi na kuwapa watu moyo. Tunasema mimi kwa sababu ya Wilaya nawashukuru sana kwa yote mliyoyafanya na ninaomba kazi hii mliofanya muendelee nayo.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja hii na ninaomba wote tuiunge mkono ila watusaidie sana hasa matatizo haya yanayojionyesha ambayo ndio pingamizi la maendeleo yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niunge mkono hoja hii ambayo imewasilishwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nianze kwa kusema kwamba Rais wa nchi hii Mheshimiwa Benjamin William Mkapa amefanya kazi kubwa sana kwenye kusimamia mageuzi ya uchumi. Kazi ambayo sio tu imejenga imani miongoni mwa wananchi wetu kwake lakini wananchi pia wamejenga imani kwa Serikali hii. Lakini sio hapo tu imejengeka imani na heshima kwenye Jumuiya ya Kimataifa. Amani ambayo kama hatukuvienzi vitu hivi gharama ya kuvirejesha itakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimeanza kwa kusema nataka kuiunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri basi niseme kwamba baada ya kuisoma hotuba ile mimi nataka nichukue nafasi hii kumpongeza yeye Mheshimiwa Ngwilizi, Naibu wake Mheshimiwa Pinda, Katibu Mkuu wake Bwana Mmari na kupongeza timu nzima ya Watendaji na Maafisa ambao wameshiriki katika kutengeneza hotuba hii ambayo imefanywa mawasilisho hapa na Mheshimiwa Waziri. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naiunga mkono naupongeza uongozi huu wa Wizara hii kwa kutambua uzito wa kazi ambayo Wizara hii inayo katika kutekeleza azma ya nchi hii kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Nasema tumeweka mikakati mingi sana hapa. Tumekuja kuboresha Elimu ya Msingi na sasa tunakwenda kwenye Elimu ya Sekondari. Tuna miradi mingi ya maji, huduma ya afya, barabara vijijini, mazingira, UKIMWI na mambo yote ya Utawala bora. Lakini tunasema kielelezo na kioo cha utekelezaji wa mambo haya yote ili kumgusa mwananchi wa kawaida *conduct* yetu ni Wizara hii. Sasa kazi hii kama nilivyoieleza kazi hii ni nzito. Kazi hii ni nzito lakini mimi nashukuru kwamba kwa kweli mpaka hapa tulipofikia wamejitahidi wameifanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hapa tumeelezwa na Mheshimiwa Waziri maendeleo makubwa ambayo yamefanyika hasa kwenye eneo la Utawala bora pale alipotaja kwamba jambo lililokuwa linasumbua sana la upatikanaji wa hati safi kwa Halmashauri zetu sasa angalau kuna maendeleo. Tuna Halmashauri karibu 39 ambazo zimepata hati safi. Hili ni jambo la kupongezwa na najua kwa hali ilivyo kwenye Halmashauri zetu pamefanywa kazi kubwa. Leo tunapotaja 39 haiwi tu 39 inatakiwa tutambue kwamba imefanyika kazi kubwa kutoka kwenye 3 safi kuja kwenye 39 safi leo. Hii kazi ni kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa nataka nitumie nafasi hii nitanabaishe kwamba hapa tunapozungumza, na hasa pale tunapounganisha na suala hili la Utawala bora, hoja yetu si usafi wa hati tu, hoja yetu ni ubora wa kazi inayofanywa na fedha ambazo tunazitenga hapa zikafanye kazi kwenye maeneo yetu. Maana ukizungumza habari ya usafi wa hati ukienda ndani kabisa utakutana na mambo mengi atakwenda Mkaguzi kwenye eneo ambapo anakwenda kufanya ukaguzi kwenye Halmashauri labda ataikuta hali ya fedha tuseme shilingi 200 milioni natoa mfano zimetumika. Zimetumikaje huyu Afisa Mhasibu anatakiwa aeleze zilivyotumika kwa kuonyesha angalau risiti ya zile fedha zilivyotumika. Kama siku ile hana risiti zile basi huwa anawajibishwa yeye kutafuta risiti zile azionyeshe siku nyingine. Sasa hili nalitaja kwa sababu siku atakaposema zile risiti za shilingi 200 zimepatikana basi huyu amekuwa anafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini tunapozungumza habari ya Utawala bora mwanakijiji aliyekuwa anategemea barabara ijengwe kwenda kwenye Kijiji chake yeye atakapoambiwa kwamba Halmashauri yako imepata hati safi kama haoni barabara ile imejengwa haelewi hati safi maana yake nini. Sasa ndipo hapo ninaposema ili ionekane kwamba kweli sisi haja yetu sio kusaka usafi wa hati tu haja yetu ni kuhakikisha kwamba yale tunayoyalenga yafanyike katika kumnufaisha mwananchi wetu yanatekelezwa kweli kwa kupitia kwenye Wizara hii. Basi tufanye ziada ya kupata zile hati safi. Maana nina hakika kabisa mahali ambapo barabara ilikuwa ijengwe na ikajengwa na hati imekuwa chafu wananchi wale hawapigi kelele.

Lakini mahali ambapo palitakiwa pachimbwe kisima na kisima hakikujengwa lakini hati ni safi wananchi wanalalamika. Sasa ndio nasema Wizara hii ina mambo mengi. Wizara hii ni kubwa hili dude kubwa na inawezekana kabisa kwamba kuna watu wanachukulia ukubwa huu wa dude hili ikawa wanafanya mambo yao huko waliko bila kupata taarifa Makao Makuu ya Wizara. Ssisi tunaomba niseme Wizara hii inatakiwa isaidiwe kwenye jambo hilo. Mimi ningependa kusema yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, mbali na kusema Kamati zako hizi zifanye kazi ya kufuatilia mahesabu haya ambayo unakuta hati safi, hati mbaya, hati nzuri, chafu na zile *conditional.* Mbali ya hili na msisahau kwamba tunapozungumza habari wa usafi wa hati tunazungumzia mahesabu ya mwaka 2003 miaka miwili imeshakatika leo.

Mheshimiwa Spika, hatujamfanyia jema hapa mwananchi. Sasa tufuate *value for money*. Ninachojaribu kusema hapa ziwezeshwe Kamati zako hizi zifanyi kazi ya ziada ya kuzifuata hizi hati. Ifike kwenye maeneo kule yanakotakiwa kufanyika mambo haya kwa manufaa ya wananchi waone kama kweli fedha zinazotengwa na zinazosemwa kwamba zimetumika na hati imetoka safi kazi imefanyika?

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu manufaa yake nimeyaona mimi. Mwaka jana Kamati yako ya kudumu ya Bunge hili ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilitembelea Wilaya yangu na ilipofika kule sijui walifanya nini lakini nataka kusema kwamba yale ambayo wameyafanya kule yameamsha kabisa ari ya utendaji na mwelekeo wa usimamiaji wa kazi kwa niaba ya wananchi.

Mabadiliko haya nimeyaona sio tu kwa wale Watendaji tu, hapana, hata miongoni mwetu sisi Madiwani na Wabunge. Sasa mimi nasema *impact* ya kwenda kutazama kama kweli fedha imetumika vilivyo hili suala la *value for money* na hasa likifanywa na Kamati zako za Bunge nina hakika kabisa, Bunge hili litafanya kazi, kazi yenye mafanikio na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ningeliomba niseme vile vile kwamba tumepata hapa tatizo wakati mmoja Serikali imefanya uamuzi wa kuajiri Makatibu Wakuu wa Serikali za Vijiji, wale Watendaji wa Vijiji ndio Makatibu Wakuu wa Serikali. Wale Makatibu wa Serikali ya Vijiji wameajiriwa lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ikajitokeza kwamba hawakuweza kutoa ajira kwa wote ambao walikuwepo *in place* kwenye maeneo yale.

Wale watendaji katika maeneo mengi na kwangu limejitokeza hili tulikuwa na mtafaruku mkubwa wako walioambiwa nyinyi ajira yenu inaanza halafu kuna wale wengine ambao pamoja na kutegemea kwamba na sisi tunafaa kupata ajira hawakupata ajira ile na maelezo yaliyotoka kwenye Wizara na Serikali yalikuwa yanasema kwamba hao ndio tunaoweza kulipa kwa sasa hivi na Halmashauri kama mnao uwezo hao wengine walipe mpaka hapo baadaye.

Sasa mimi nasema nashukuru kwamba nikifuatilia mawasilisho haya yaliyofanywa na Waziri hapa na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara zilizokwishatangulia ya Fedha na Ubinafsishaji naona jambo hili sasa limekwishafanyiwa kazi. Hili limetunusuru sana lawama katika maeneo tunakofanyia kazi. Kwa hiyo nataka kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo kwa kweli imetutengenezea nusura kubwa ya kuzidi mitafaruku hasa katika wakati huo ambao majimbo yana-b*eep. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niseme jambo lingine. Tumefuta kodi tunasema kodi za kero zile lakini Serikali ikaahidi kwamba zile kodi zimefutwa sasa tutaleta fidia kwa ukosefu wa mapato kutokana na kufutwa kwa kodi zile. Hapa tumesomewa na Mheshimiwa Waziri kwamba zimetolewa fedha shilingi 22.9 bilioni mwaka juzi na mwaka jana imetolewa shilingi 25 bilioni. Mimi nilikuwa nataka kusema pamoja na kutengwa kwa fedha hii lakini nadhani fedha hii manufaa yake yataonekana dhahiri zaidi kama zikiwa fedha hizi zinapelekwa kwenye Halmashauri zile kwa wakati. Tuna tatizo la fedha hizi kuchelewa kufika au pengine kukosekana kabisa.

Sasa katika hali ambayo unakuta Halmashauri inajipanga ingawaje inajua kwamba fidia itakuja na sisi tunapanga mipango yetu tufanye kulingana na tulivyoupanga mwaka fedha hii kama inachelewa au kama haiji kabisa kwa kweli inatutengenezea matatizo makubwa katika utekelezaji wa maazimio yote ambayo tunayafanya kwenye mipango ya kuendesha Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu niseme lingine na ikiwezekana liwe la mwisho. Mheshimiwa Waziri amezungumza ndani ya hotuba yake hapa jambo linalohusiana na kutoa huduma kwenye ofisi za Ma-*DC* na humo humo ofisi za Waheshimiwa Wabunge kama zipo. Mwaka wa jana na hapa nataka nizungumzie habari ya ujenzi wa ofisi ya *DC* wa Wilaya ya Tandahimba.

Mwaka jana hapa nilisimama nikalizungumza jambo hili nilizungumza kwa kutambua kwamba mwaka uliotangulia tulikuwa tumepangiwa fedha shilingi 73 milioni kazi ya ujenzi wa Ofisi ya Wilaya Tandahimba ianze.

Lakini mpaka mwaka wa jana tulipokuwa tunazungumzia kwenye hatua kama hii ya leo nilivyosimama hapa ilikuwa kazi ile hakijaanza na kiwanja hakijasafishwa na nikahoji hapa kuna uhalali gani leo tukute tumepangiwa tena fedha na mwaka jana ilikuwa 110 milioni tunapangiwa fedha hii hii wakati ile 73 iliyotangulia hatujaiona imefanya kazi gani, tunasemaje.

Tunasema zile 73 zilizotangulia mwanzo zitachanganywa na hizi 110 zinazotolewa mwaka ule uliopita ambao unakwisha sasa ili ziwe 183 ili tuone kazi inakwenda kwa haraka zaidi au tunategemea nini. Lakini Mheshimiwa Waziri nadhani alitoa jibu na sitaki kulisema hapa pengine analifanyia kazi bado.

Lakini nataka niseme kwamba hali ilivyo leo hakuna matumaini kwamba ofisi ile inaweza kwisha kujengeka kwake kwa utaratibu huu ambao tunakwenda nao sasa. Wale waliofika pale wanajua kabisa mwaka mzima baada ya mazungumzo yetu mwaka jana niliona kabisa kama lile jengo na sasa hivi hata nadhani halijafikia hata *level* ya *lintel* lakini kama kweli fedha hizi zimetolewa Shilingi 110 milioni mwaka jana na 73 milioni mwaka juzi, kama kweli fedha zile zimetolewa basi tuna 183 milioni zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa jengo ambalo halijafika hata hatua ya *lintel.*

Tunazungumza utawala bora, hivi wale watu wa Tandahimba wakisikia tumepangiwa fedha na Serikali inatutambua kwa kupangiwa fedha za kujenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya yetu fedha kiasi hichi ninachokitaja halafu waone kwamba jengo lenyewe ndiyo kama pale lilipofikia matofali yamekwenda si zaidi ya kozi sita, sidhani kama wataungana na sisi kusema haya tunayaendesha katia misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, nimelirudia hili kwasababu nina hofu kwamba inawezekana mwaka huu tumetengewa fedha zingine kwa ajili ya jengo hili, sasa tupate maelezo ambayo kwa kweli yatatushawishi na sisi tukapata imani ya kwamba jengo tutalipata na ikiwezekana na Mbunge akapata ofisi kwenye jengo hilo la Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sasa kama hali ni hii mimi napata hofu. Hofu hii haitaondoka mpaka hatua ambayo Mheshimiwa Waziri atakapotoa maelezo ya kuniambia kunachoendelea pale ni nini. Nilikuwa sikupanga kusema mengi zaidi ya haya niliyokwisha tangulia kuyasema na nilianza kwa kuunga mkono hoja hiii nzuri ya Mheshimiwa Ngwilizi na naomba kwa ruksa yako nimalizie kwa kuiunga mkono tena hoja hii, nakushukuru sana (*Makofi*)

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kuniruhusu niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara hii kuhusu Bajeti yake. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Ngwilizi kwa kazi wanayoifanya pale Wizarani na hususan nimshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda, anafanya kazi kubwa na nzuri sana. Waheshimiwa Wabunge pengine ni mashahidi kwamba hata anapokuwa anajibu maswali hapa hakasiriki hata kama umemuuliza swali baya wala hakufurahishi kwa kile ambacho hakipo, na ukiwafuata ofisini nadhani utaratibu anaoutumia ndiyo huo huo. (*Makofi*)

Mheshimima Spika, sasa kwa kuwa Wizara hii, Waziri kabisa kabisa ni Mheshimiwa Rais, basi ninapenda haya mengine nitakayoyasema pengine wamfikishie. Juzi wakati nachangia kwenye Wizara ya Fedha kuhusu Bajeti nzima na Mipango, nilitaja kitu ambacho nilisubili nije nimkamate Waziri kwenye fungu lakini fungu halikuwepo. Sasa nitakirudua hapa kwa sababu wahusika wako kwenye Wizara hiyo,

kwa sababu jiji la Dar es Salaam na zile Manispaa ndiyo walioweka lile soko la Magogoni lile linalofanya Ikulu inuke. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri na yeye kwa sababu anakaa maeneo yale ile harufu anaisikia, na wageni kutoka nje wanapokuja inakuwaje? Maana kuna kitabu kimoja kinaitwa *An enemy of the people,* kilikuwa kinazungumzia uchafu wa Serikali ya Manispaa huko Norway lakini alitumia dimbwi kwamba dimbwi ndilo linanuka

Sasa ule uchafu pale magogoni maana yake nini? Sitaki kusema sana kwasabu siku ile nilisema sana. Sasa kwa sababu Waziri anaye husika na zile Manispaa ambazo zimejenga pale tutaomba pengine aje atufafanulie.

Mheshimiwa Spika, jingine, niko Dar es Salaam pale Tandale, hivi nataka kujua Mheshimiwa Waziri watu wanoakaa pale Tandale na wanaofanya biashara wanalipa kodi? Sijui Mheshimiwa Spika nadhani hujawahi kufika pale, hujawahi kufika. *It is deplorable* yaani pananuka pachafu, sasa kama sio kudhalilishana kwa kweli ni kitu gani kinachofanyika.

Mheshimiwa Waziri naomba kabisa wewe kapige hata simu *DC* afike pale ni aibu. Nilikuwa napita pita tu mitaani natembea, yaani ni aibu. Huwezi kufikiria kama wanadamu Watanzania wanakaa katika eneo lile na wanafanya biashara katika mazingira yale halafu mtu anakuja na mfuko na kakaratasi eti anaomba kodi, unaomba kodi gani.? Sasa nisipopiga kelele sana nadhani kuna watu wameshafika huko wanaelewa.

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye yale ambayo pengine yanahusu Jimbo langu na mambo ya kwangu. Vipaumbele vya Wizara na Serikali kwa ujumla vinatutia wakati mwingine wasiwasi, kwa sababu katika dunia ya utandawazi ambako mashirika na makampuni makubwa ya kimataifa na kupitia ubeberu wa kimataifa alikwisha sema *Karl Max* huko nyuma kwamba kwa kweli miji inanyonya vijiji. Hiyo ni kanuni, *it is an axiomatic theory* na hakuna mtu anayeweza kuipinga.

Sasa mipango tunayopanga sisi vitu vyote tunaweka pale Dar es Salaam, maana ukizungumza barabara nzuri, ukizungumza umeme, ukizungumza maji, ukizungumza komputa vyote viko pale iwe ni kwa upande wa shule za Secondari, kila kitu kizuri kiko pale. Najua nako wanalalamika lakini sisi tunazungumza hapa tunataka kufuta umaskini. Sasa tumepanga hii Sheria ya *TANROAD* ile na hii inayohusu Mfuko wa Barabara watakupeni asilimia 30.

Lakini mwenye kilomita nyingi za barabara nchi nzima ni Serikali za Mitaa hawa watu wa TAMISEMI. Sasa wao unawapa asilimia 30, sasa unamaana gani? Wakati huo huo unajua mmeshakubaliana kwamba makusanyo ya taifa tutakuwa tunakata hela fulani tunaweka kwenye barabara kuu. Tutakwenda kwa wafadhiri, Japan, Norway watatupa hela tutaweka kwenye barabara kuu. Sasa huyu mwenye kilomita nyingi na ambaye ndiko watu wengi wanaa kule vijijini wao wanafaidi vipi?

Mheshimiwa Spika sina idadi ya watu wangapi wanaopita kwenye barabara kuu hii kwa mwaka hata kama wanarudia mara tano mara kumi, lakini ninauhakika kwamba

watu wanaokaa vijijini ambao hawajawahi kukanyaga kwenye barabara kuu za lami kuja Dar es Salaam ni wengi. Wao ndiyo wanaochangia, maana alinichekesha mtu mmoja alikuja kule Bukoba, mtu mmoja mkubwa sana, akasema Serikali inawajali sana siku hizi tunakamata matajiri wakubwa wale ndiyo wanalipa kodi. Nikamshangaa wanalipa kodi wapi? Kwa sababu kodi ya *VAT* inalipwa na mlaji anayetumia mafuta ya taa kule kwenye kibatari na anayenunu chumvi na sukari kilo moja moja, ndiyo bei kubwa inamangukia yeye. Sasa hawa watu waliowengi kama hatutaki kuwajengea barabara, mimi nauliza barabara hapa zina watu 500,000 zaidi ya nusu ya wakazi ya Zanzibar. Tunazalisha kahawa zaidi ya tatu ya nne ya kahawa ya nchi hii, robusta tunazalisha. Sasa nauliza haka kakipande kabarabara najibiwa, hata kwingine hawajatengeneza. Unajua wale ambao hawajui Jimbo langu ukitaka kushora ramani ya Tanzania kama wewe si mkorofi ni pale unapoanzia kuchora kwa karamu unakuja hadi Ukerewe unakwenda hivi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Sasa ni mbali kidogo kutoka kule Dar es Salaam, tunasahaulika kwa sababu ya barabara mbovu, limkungu la ndizi kubwa hivi shilingi 500, gunia la maharage shilingi 10,000, mfuko wa saruji kwa sababu ya umbali wa kusafirisha kutoka huku shilingi 15,000, bati moja shilingi 8,000, sasa kwa sababu ya jiografia na mahala tulipo tunapunjika halafu tukianza kuuliza hapa tunachogawana hakuna.

Mheshimiwa Spika, naomba Rais ajaye hata huyu aliyepo, suala la Wizara ya TAMISEMI mliangalie mmewapa majukumu mengi. Ukiuliza kuhusu elimu ya msingi watakwambia kamuulize Mheshimiwa Ngwilizi, ukiuliza kuhusu Zahanati au Kituo cha Afya, Wizara ya afya inasema sisi hatujui kamuulize huyo, lakini unamuuliza huyo hii *network* mnaifanyaje? Sijui kama *RAS* wa Kagera yupo hapa.

Tumezungumza kwamba tunajenga shule za Sekondari, nikazungumza na watu wa Wizara nikajenga hoja hapa kwamba sisi Karagwe bwana kwa mujibu wa hstoria na jiografia hatuna shule za sekondari nyingi. Nenda pale Bukoba kaeneo kadogo hivi tu wala hakalingani na eneo hili la mji wa nani. wana shule za Sekondari ya Kahororo, Ihungo, Bukoba, Nyakato, *Bukoba Day*, Rugambwa zote zimejazana pale.

Sasa tukapewa shule 10, mtu moja Wilayani sijui ni Mkoani hakupeleka hayo majina ya shule kumi zilizoanzishwa mpya kupeleka Wizarani. Kama *RAS* wa Kagera yuko hapa naomba amuulize. Sasa sijui anapata mshahara wa nini, hawa watu wamekaa huko wanapata mshahara wa nini? Maana yake kama ni Mkuu wa Mkoa wa Kagera hata angeliandikiwa barua na mwanakijiji ili mradi aweke sahihi na jina lake na mahala alipo, atamfuata amwambie wewe ulikuwa unalalamika tuonyeshe ulichokuwa unalalamikia. Sasa kama kuna mtu anakula mshahara wa Serikali anazungusha kiti hivi watu wanampa mambo ya kupeleka kule, anakaa tu kama *sultan* , anafanya kazi gani pale?

Mheshimiwa Spika, sasa mnasema umeme mnawekeza na mnasema wawekezaji wamesaidia jamii zilizokuwa pale pembeni, sasa wawekezaji si wanachagua kwenye dhahabu ambayo ndiyo yenye biashara kubwa. Sasa tunaposema nchi inapiga hatua. Naomba tufanye tathimini tupande Helkopta tuanzie Dar es Salaam iruke chini chini, tuondoe mashule yaliyojengwa kwa hela za MMEM za mkopo kutoka Benki ya Dunia, tuanze kangalia nyumba zilizoezekwa kwa nyasi kwa miaka kumi wameezeka ngapi kwa mabati na nyumba kumi ngapi za watu binafsi wacha zile shule wamejenga kwa matofari

ya kuchoma? Twende tupitie Shinyanga turuke hivi, twende, au ni wangapi kati ya hao wameweka hata sola, hakuna. Tunachofanya tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, nadhani kama kuna mahala kuna *conditions* kuna hali hazijawa sahihi ni wakati huu wakuziweka. *If the conditions are not ripe in the field we have to create them there.* Maana huwezi kusema hawawezi kuwekeza kwa sababu hayo mazingira hayapo. Tuyaunde hayo mazingira kule tuliko. Sasa Serikali inaleta utaratibu hapa, unajua tumekopesha vikundi vya vijana, wewe unawakopesha shilingi 50,000 kikundi cha watu kumi wanauza maandazi, wanauza nyanya au wanauza kitu gani? Hakuna maendeleo hapo. (*Makofi*)

Tumekopesha wanawake, mjiunge kikundi cha watu kumi, kumi wakafanye nini? Ningelikuwa mimi ndiyo napanga nasema hapana, nasema watu hawa pale Lushoto hivi wanalima machungwa tukiwawekea kiwanda cha kusindika matunda na bei ikawa kubwa itawapa *incentive* kila mmoja atakwenda kulima matunda auze humu na apate kwa sababu mtakuwa mmeongeza thamani. Sasa sisi hiyo hatutaki tunataka tu tunakwenda tunawakopesha kashilingi 10,000 kila watu kumi, hawana hela wanakimbia kimbia hawana hela, wakati tunagombea tunawanunulia pombe. Sasa kama watu wamekopeshwa wamelima mtama, wamelima mapapai si wanatengeneza pombe ya kwao kama wakitaka kutengeneza mapipa mengi wakaogelee humo si shauri yao, lakini angalau wauze.

Sio watu wanakaa maskini, wanawagawia kopo la pombe wanachekelea kabisa, ndiye anafaa, wewe unafurahi amekununulia kopo la pombe atakununulia miaka kumi yote ya maisha yako. Sasa tunachosema lazima hizi hela tunazotumia hapa tuna tupatupa tu tujiulize.

Kama ni wale wa korosho sio mwekezaji hakuja, Serikali iende pale ikajenge kiwanda cha Korosho Mtwara isema tunajenga mnabangua hapa kama kilo moja ilikuwa ni shilingi 300 basi mkapate 800. Sasa watu wana hela mfukoni hiyo ndicho mnachaoweza kufanya. Lakini sio hii tabia ya kwamba tumewagawia mkopo, panga hapo kikundi cha watu 200 mnawagawia shilingi 100,000/=.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo mambo ambayo tukubaliane, mimi Karagwe sijawahi kutumia mbolea hata ile ya ruzuku mnayosema, pamoja na lita ya petroli shilingi 1,500 kila kitu bei juu . Km 50 unatembea kwa nauli ya 5,000 ambazo ndizo unatoka hapa Km 400 kwenda mpaka Dar es Salaam. Sasa mimi nikija hapa nauliza kwamba hivi hatuwezi tukaangalia kila mazingira na hali yake. Hakuna wanaotaka kuangalia hayo wao wanasema sisi tuna kanuni tuna abracadabra, abracadabra ni hirizi ya Wahindi kule India inatibu magonjwa yote. Sasa tuna abracadabra nchi nzima haiwezekeni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunawaomba Wizara, yako mambo ya msingi, tunaweza kuzunguzia utalii hapa. Mheshimiwa Sebabili alikuwa unauliza swali Wizara ya Utalii mara nyingi ukiuliza wanakwepa wanasema muende kwenye Wilaya yenu.

Lakini Kituo cha Uwekezaji kwa nchi hii nzima kiko Dar es Salaam, matawi Mikoani hakuna, wale walioko kule Wilayani ukiwauliza kuhusu mambo ya uwekezaji hakuna kila moja anakimbia kimbia tu anasubiri posho.

Yako maeneo mengi kule, sasa hawawezi kwenda kwa sababu umeme haupo, anayetaka kujenga hoteli hawezi kujenga maji hayapo. Kwa hiyo tunaomba Serikali ifike mahala iangalie masuala haya, na tuamue namna ya kuwasaidia wananchi kwa kweli tuondokane na tabia hii ya kusema tunawapelekea mkopo waunde vikundi vikundi. Mimi nigeliomba Serikali iweze kufanya tathimini, hata hizi hela mlikuwa mnasema humu mmewakopesha wengine wamerejesha wengine hawakurejesha, *impact* ni nini? *We should invest for impact,* sasa *impact* haipo, unagawia gawia watu hela wanakimbia kimbia wanakunywa pombe halafu mambo yamekwisha.

Mheshimiwa Spika, tunaoimba Serikali ni hii nimeizungumza sana, kuna maeneo haya tuna shule, maana tunatofautisha watu hapa, shule ya vipaji maalum zote ziko huku mijini, shule zingine komputa mjini, sasa hata zile shule za vijijini tuwapelekee angalau *Generator* moja la shilingi milioni tatu, hata hiyo hatutaki.

Tulikubaliana hapa simu, wale watu wa *TTCL* nikisema wananiangalia kwa jicho kali, hawakupeleka. Sasa sisi twende wapi na wakati sisi tunanunua petroli tunachangia kahawa tunachangia mahindi, tunachangia kila kitu. Sasa Waziri wa Mambo ya Ndani anasema twende Uganda, ningetaka kwenda Uganda si nakata kipande changu nakipeleka kule, lakini sitaki (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika maana yake mambo kama hayo watu wanapoyasikiliza anaweza kutoka mwendawazimu mmoja anawashawishi anasema twende Uganda, kwa sababu Mbarara ni karibu, kuna umeme, kuna maji na nini, lakini hatuwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, tukubaliane kwamba tunavyogawana keki ya taifa tugawane vizuri. Nadhani mmenisikia, lakini pale panaponuka nitakamata kifungu hapo mtanieleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu mmesema mtaunda mfuko wa barabara, Naunga mkono hoja lakini mjirekebishe sana. (*Makofi*).

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza niombe kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya TAMISEMI. Kazi iliyofanyika ni nzuri na ni mwendelezo wa hayo yaliyokuwa yamefanyika kwa miaka iliyopita na sasa inatuonyesha au imetuletea dira tuelekee wapi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Serikali za Mitaa kupata vyeti vichafu. Kikubwa ni kwamba Kanuni za Utumishi zinaonekana kwamba katika kipindi tulichonacho zimekiukwa.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma, sisi tuliofanya kazi miaka ya kwanza, kwanza, kabla ya Uhuru kulikuwa na utaratibu wa Watumishi wakae katika maeneo fulani kwa muda kiasi gani. Kwa kweli mtumishi yeyote kukaa mahali kwa zaidi ya miaka mitano/sita, huyu mtu anabadilika kuwa Mangi Meza, anayazoea mazingira hata anajikuta kwamba amekuwa hana wasimamizi na kazi zake zinakwenda kama anavyotaka yeye. Kwa hiyo, naiomba Wizara ifikirie na kutazama kwamba sehemu

nyingi watumishi wetu hasa wale wanaotunza hazina wamekaa kwa muda mrefu sana, sasa hawajali kitu.

La pili, ni ujuzi. Wakati wa Bajeti mwaka jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitamka kwamba nchi hii haina wahasibu wa kutosha na wahasibu wenye ujuzi. Pamoja na kwamba Serikali inapeleka pesa nyingi sana huko Wilayani na Vijijini, Serikali inajua kwamba hakuna wajuzi. Sasa ukifikiria mabilioni yanayokwenda kila Wilaya sasa hivi wakati watunza hazina uwezo wao ni huo, lazima itegemewe kwamba vyeti vitakuwa vichafu. Sasa sijui Wizara hii inasema nini, kwa sababu baada ya Wizara ya Fedha sasa TAMISEMI ndiyo inakuwa ni ya pili katika masuala ya kutunza fedha ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mahali pengine kuna malumbano lumbano kati ya vitengo vya fedha na wasimamizi kwa maana ya *Accounting Officers.* Sasa kuna kitu kinachofanana kama kukomoana komoana. Mambo yatakapoharibika, Mkurugenzi Mtendaji watamuondoa au Mkurugenzi Mtendaji anaweza akafukuzwa kazi. Masuala haya mimi nafikiri kwamba Wizara hii iyatazame kwa sababu nchi hii ni kubwa na ingekuwa ni vizuri kwa kuwa Wizara hii ndiyo Wizara Mama ikaunda timu ndogo ambayo inaweza ikawa inapita huko Wilayani na Mikoani mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufuta Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango, kutokuwa Kamati inayoshughulikia zabuni, hili suala limekuwa ni kubwa sana, hakuna usimamizi. Nyumba hii ililipigia kelele kwamba pengine ingetoa mianya ya mali ya umma kutokutumika vizuri. Vyeti vichafu hivi vinaandamana na pesa kufujwa. Sasa nafikiri Wizara hii itazame, je, inaweza ikafanya mabadiliko katika suala hili kusudi jasho la wananchi liweze kusimamiwa vizuri na wawakilishi wao.

Mheshimiwa Spika, nafikiri na ukaguzi nao una matatizo hasa ukaguzi wa nje una matatizo kwa hiyo, ni kazi ya Wizara kutazama kinachoweza kufanyika ni kipi.

Napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri kuhusu maendeleo ya elimu, kwa kweli kazi imefanyika, mapinduzi ya elimu yanaonekana. wananchi wa Ngara wanaipongeza TAMISEMI. Kwa miaka mingi Ngara ilikuwa haijulikani kwenye chati ya Taifa hasa kwa mitihani ya darasa la saba, lakini kwa miaka mitatu mfululizo imekuwa ikiwa ya kwanza Kimkoa, kwa miaka miwili mfululizo imekuwa ya kwanza Kimkoa na Kikanda na kwa mwaka jana imeweza kupanda chati ikafikia kuwa ni ya pili Kitaifa. Kwa kweli tunajivuna sisi na kazi iliyoko mbele yetu katika Wilaya ile ni ngumu sana. *(Makofi)*

Naomba niwasilishe maombi ya wananchi wa Ngara kuhusu upanuaji wa shule za sekondari. Wilaya ya Ngara ina Sekondari tano tu na tatu zimejengwa katika kipindi cha 2000 mpaka 2005. Lakini kwa bahati mbaya sasa hivi tuna watoto zaidi ya 1303 ambao wako kijijini wakiwa na alama za A, B na C kwa kukosa nafasi mahali pa kwenda na kwa sababu ya umaskini wa wazazi wao.

Sasa nina maombi mawili hapa, kwanza kabisa kuna Kambi huko ya Wakimbizi, Kambi ya Mboba ambayo imefungwa. Halmashauri ya Wilaya haina uwezo wa ku-

*trasform* hiyo kuwa Sekondari lakini inafaa kuwa Sekondari kwa sababu majengo yapo, lakini tatizo letu kubwa ni maji. Wizara ifikirie kupeleka pale maji kusudi tuweze kuifungua kuwa ni Sekondari kwa sababu ya wananchi wa Ngara.

Lakini la pili, hata hao waliopata nafasi kwenda katika shule mbili ambazo zimefunguliwa mwaka huu shule ya Kibogora na shule ya Mgoma, hakuna walimu. Kibogora ina mikondo miwili lakini ina mwalimu mmoja tu. Nimekwenda Wizarani, nimeonana na wakubwa kila mahali lakini imeshindikana kupata walimu.

Kwa hiyo, hao walioko katika shule hii hawajatofautiana sana na wale waliobaki vijijini 1303. Tunaomba suala hili litazamwe kwa jinsi inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina kazi kubwa lakini isisahau kwamba mpaka sasa hivi mazingira wanayoishi walimu wetu wa ngazi zote ni mabaya sana. Sasa tunapozungumzia MMEM ambayo inaendelea na MMES ambayo ndiyo imeanza sasa hivi, kuna haja ya kuona mazingira ambayo walimu wetu wanafanya kazi yanafananaje. Kwa kuwa madeni yamefutwa, madeni ya ulimwengu wametufutia, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, tunamtakia maisha mema na afya njema, tunaomba pesa hizi Wizara iende ikatazame kama inaweza kushirikiana na Wizara ya Fedha kuomba fedha zaidi kwa sababu ya Taifa kujenga mazingira mazuri kwa walimu wetu waweze kuendeleza mapinduzi ya elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie taratibu za Serikali kuanza miradi na isiimalize. Naishukuru Serikali ingawa imeupa Mji wa Ngara umepata Umeme, lakini umeme huu hata baada ya kuahidiwa na Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi mwaka 1995, umeshindikana kukamilika.

Naomba Serikali ijue kwamba kwa kweli inapowaonjesha wananchi ambao wana ari ya maendeleo ikawaonjesha kitu ambacho wanakihitaji na isikikamilishe, kwa sehemu fulani inakuwa imewakosea. Umeme huu ulipaswa kwenda Kabanga, nguzo zimewekwa kwa muda sasa wa mwaka mzima lakini vinavyokosa ni nyaya, vinavyokosa ni vikombe. Pale katikati kuna kiwanda cha Kahawa. Kile kiwanda kimekaa hakiwezi kufanya kazi vizuri. Naomba Wizara hii ishughulikie ikishirikiana na Wizara nyingine inayohusika tuweze kupata umeme huo.

Mheshimiwa Spika, kutoka Ngara kwenda Lulenge ni kilometa 22 tu, lakini kuna malumbano ya kwamba kuna fidia njiani ambako hakuna chochote kabisa cha kufidia wananchi. Kinachohitajiwa ni kiasi cha nguzo kama 100 kuweza kufikisha umeme pale Lulenge. Narudia na hii ni ahadi ya Mtukufu Rais Benjamin Mkapa, kwamba kazi hii ingeweza kufanyika, sasa inafikia mahali aondoke katika madaraka wakati kazi haijafanyika. Naomba kitu hiki Wizara ya TAMISEMI kama Wizara ambayo ndiyo Wizara Mama basi isaidie kukamilisha kitu hiki kwa maendeleo ya wananchi wa Taifa hili kwa upande ule kwa upande wa Ngara.

Mheshimiwa Spika, sisi tuko mpakani, mwezi wa nne, Kata ya Bugalama waliuawa watu watatu kwa uvamizi wa wakimbizi, niseme ni wakimbizi kuvuka mpaka

kutoka nchi jirani ya Burundi kuja pale. Mwanzoni mwa mwezi wa Tano wakafa watu wawili katika Kata ya Mulusagamba. Sasa kuna bahati mbaya za aina mbili zilizoko pale.

Kwanza hakuna mawasiliano ya kutosha pamoja na kwamba Serikali inapongezwa kwa kuleta mtandao mzuri kule Ngara, lakini Kata za Mulusagamba, Bugalama, Bukililo, Kilusha hazina mtandao wowote. Vituo vya Polisi viko mbali sana, sasa wakati wa shida watu hawa hawana kimbilio. Tunayo *Celtel,* tunayo *Vodacom, Mobitel* nao wameingia sasa hivi lakini wameshindwa kujenga minara upande ule. *(Makofi)*

Napenda nimpongeze Mama yangu hapa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, naona nilipokuwa nazungumza amechukua kalamu kuiweka chini, nafikiri kwamba nitafanikiwa kwa hilo. Kwa hiyo, ninaomba kwa kweli upande huu kazi hii ifanyike, bado tatizo la wakimbizi halijaisha, wanarudi kwao hali inaonekana kwamba ingekuwa shwari lakini wako wavamizi na wako watu majambazi walioko msituni wanatupa shida sana. Watu wetu wanakufa, mali zinaharibiwa kwahiyo, tunahitaji kuwa na mawasiliano kwa kweli ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, tunayo barabara ambayo imeanza kujengwa kwa sababu ya kwenda kwenye Machimbo ya Kabanganikeli kutoka Kumubuga kupitia Mulusagamba, Muganza kwenda Kabanganikeli ambayo ni katikati ya Bugalama. Ni bahati mbaya sana zitakuwa zimebaki kilometa 8 tu kufika Machimboni na kufika Makao Makuu ya Kata ya Bugalama. Lakini wanasema itaishia pale Muganza, kumbe nafasi itabaki haikusaidiwa. Sasa itakuwa ni lazima kuweka mkataba mwingine tena baadaye ambao utawafanya tena Makandarasi waanze kufunga mizigo, waanze kuja kutengeneza kambi, kumbe kama kazi hii ingeweza kufanyika kwa wakati mmoja ingeweza ikasaidia.

Mheshimiwa Spika, kilometa zitakazokuwa zimefanyika ni zaidi ya kilometa 75. Sasa kilometa 8 zinabaki pale sawa sawa na mtu kula nyoka akashindwa kula mkia wake. Kwa kweli haipendezi, Serikali ingekuwa na utaratibu kwamba kazi kama zinapofanyika zinakamilika. Mkandarasi yupo pale kama anaweza kuingia mkataba wa pili akamaliza kazi ile itasaidia sana kupunguza gharama katika Serikali na bado itatusaidia sisi kwa sababu ile ni barabara ya ulinzi inayozunguka Wilaya ya Ngara kupitia Kibondo kwenda Burundi na kutokezea mpakani mwa Tanzania na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie uwezo, madaraka na kazi zinazofanywa na Madiwani. Madiwani wao ndiyo wenyeji wa kila mgeni kutoka ngazi zote. *DC* hawezi kwenda Kijijini, Mkurugenzi Mtendaji hawezi kwenda kwenye Kata, Mkuu wa Mkoa hawezi kwenda Wilayani kama Diwani hakuambiwa kuwapokea na kuandaa mikutano na kuandaa vikao ili kusudi shughuli za wakubwa hawa ziweze kukamilika.

Watu hawa mapato yao ni kidogo tunayafahamu. Watu hawa usafiri hawana kabisa, wanahangaika. Sasa hiyo inakuwa ni pamoja na wasaidizi wao, watendaji wa Kata, watendaji wa Vijiji. Ninaomba TAMISEMI ifikirie...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni kengele ya pili.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba watu hawa wafikiriwe kupewa mikopo ili waweze kufanya kazi yao vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono tena hoja iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru kupata nafasi hii, ili kuweza kuchangia katika hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Serikali za Mitaa Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi. Napenda niwashukuru Naibu Waziri pamoja na watalaam wote katika Wizara hii ambao wameandaa hotuba ambayo imejaa shughuli nyingi za Wizara ambazo ni za kuwahudumia wananchi katika Serikali zetu za Wilaya, Miji na Halmashauri mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwetu sisi ambao tunaitegemea kuweza kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo katika elimu, afya, barabara za vijijini, mazingira na uchumi wa wananchi kwa ujumla. Ni Wizara ambayo ni lazima iwe makini ili kuweza kuwasaidia wananchi waweze kupata maendeleo yao.

Sasa yapo maeneo mbalimbali ambayo nilitaka niyazungumzie katika Bajeti hii ili Wizara iweze kuangalia ni jinsi gani ya kuweza kusaidia maendeleo katika Vijiji vyetu, Kata zetu na Wizara zetu.

Mheshimiwa Spika, tukirejea nyuma Waheshimiwa Wabunge walikuwa wameomba kupunguziwa mzigo wa maeneo yao ya kiutawala au yale maeneo wanayowakilisha hasa ya Majimbo na Wilaya kugawanywa. Zipo Wilaya zimegawanywa lakini Wilaya nyingi sana ziliomba lakini hazikupata nafasi ya kuweza kugawanywa. Serikali imetoa maelezo kwamba bado Serikali haijapata uwezo wa kuweza kuhudumia Wilaya nyingi zaidi ya hizo. Lakini tunaomba Wizara hii iweke katika mpango wake kuangalia ni jinsi gani ya kuweza kuzigawanya Wilaya nyingine ambazo ni kubwa sana kama Wilaya ya Mpanda, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini ni Wilaya kubwa ambazo zina watu wengi sana na zinahitaji kugawanywa ili walau utawala uweze kwenda karibu na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Majimbo lilizungumzwa na Wabunge wengi walilalamika kwamba Majimbo yao ni makubwa, lakini nalo hili halikufanyika katika kipindi hiki bado Wabunge wa maeneo haya katika Majimbo haya wataendelea kubeba mzigo. Lakini ikumbukwe kuna Majimbo mengine ya wananchi wanaowakilishwa na Mbunge mmoja mpaka kufikia 300,000, 400,000, 500,000 wakati yapo Majimbo mengine yana wananchi wanaowakilishwa kama 10,000, 15,000 nadhani uwiano huu siyo mzuri inabidi Serikali iangalie ni jinsi gani ya uwiano huu utakavyoweza kuletwa katika miaka ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Kata, suala hili kwa kweli ni tatizo kubwa kwa Majimbo mengi. Mimi nimeshamuona Mheshimiwa Waziri, kuhusu tatizo la Kata zangu tatu. Kata tatu nilizokuwa naomba lakini Kata moja ina matatizo makubwa ni Kata ya Kasanga. Tarafa ya Kasanga ni Kata moja hiyo hiyo, lakini Kasanga imekaa katika Bonde la Ufa. Sasa wananchi katika Vijiji saba wanaokaa kando kando ya Ziwa, hawawezi wakakawasiliana kwa urahisi na wananchi walioko juu ya Bonde la Ufa. Sasa mawasiliano hayo kati ya wananchi wa Vijiji saba vilivyoko katika Bonde la Ufa na wale wa Vijiji kama vitano vilivyoko juu ya Bonde la Ufa kwa kweli tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, ni Kata moja na ni Tarafa moja hiyo hiyo, nimeisemea sana Mheshimiwa Waziri analifahamu, lakini jibu tunalopewa ni kwamba Serikali haina uwezo na haikuweza kutenga hivyo. Sasa Kata hizo mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri, aweze kulizungumzia suala hili atueleze suala hili limefikia wapi na litashughulikiwa namna gani. Kata ya Kasanga niliomba igawanywe walau katika kata mbili Kata ya Kasanga na Kata ya Kisumba. Halafu Kata ya Sopa nilikuwa nimeomba igawanywe na Kata ya Katete na Kata ya Mwimbi nilikuwa nimeomba igawanywe na Kata ya Ulumi ili kuweza kurahisha utawala katika maeneo hayo. Halmashauri ilikuwa tayari kuweza kuchukua mzigo huu na kuanza kulipa watendaji katika maeneo haya. Lakini kwa sababu Wizara ilikuwa haijatoa maelekezo yoyote imekuwa vigumu kuweza kuanzisha uongozi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia kuhusu suala la Miji Midogo. Tunayo Miji Midogo katika Jimbo letu, Miji ya Matai, Ulumi na Mwimbi nayo tungependa kujua mipango yake itakuwa namna gani katika Bajeti hii ili iweze kujihudumia yenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu vituo vya afya, tunashukuru sana Wizara hii imeshughulikia sana vituo vyetu vya afya na imeweza kuvikarabati vingi na kutoa magari ya kuhudumia wagonjwa lakini bado lipo tatizo la kituo changu cha afya kimoja cha Mwimbi ambacho hakijakarabatiwa. Ni matumaini yangu Wizara itaingiza katika mpango ili kituo hiki nacho kiweze kipatiwa ukarabati. Lakini tulikuwa tunaomba vituo hivi pia vipewe umeme wa jua *(solar)* ili walau viweze kuendesha shughuli mbalimbali hasa kipindi cha usiku ambapo unakuta katika mazingira ya vituo vya afya kunakuwa giza na vifaa vingine vingehitaji kutumia umeme lakini wanashindwa kuweza kuvitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la maji katika vituo vyetu vya afya, Kituo cha Mwimbi hakina maji safi na salama, tungependa Wizara iweze kusaidia kuona ni jinsi gani tutakavyoweza kupata maji safi na salama kwa ajili ya wagonjwa na kwa ajili ya matumizi ya Kijiji cha Mwimbi ambacho ni muhimu sana pale kwa ajili ya kuhudumia wananchi katika kata karibu tatu/nne, Kata ya Ulumi, Mambwekenya, Mambwekoswe na Legezamwendo. Tunaomba walau papatikane maji ili yaweze kusaidia katika uendeshaji wa kituo hiki cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la utawala bora ningeishauri Wizara ijitahidi kuangalia ni jinsi gani watumishi wake katika Halmashauri zetu wanavyowajibika

ipasavyo ili kuweza kutimiza azma hii ya utawala bora. Kuna malalamiko mbalimbali ambayo yapo katika Halmashauri nyingi juu ya watendaji ambao hawawajibika ambao wako chini ya Wizara hii na mimi mwenyewe nilishawahi kumwandikia

Mheshimiwa Waziri, barua ya kulalamika kuhusu Mhandisi wa Wilaya aliopo katika Halmashauri yetu ya Sumbawanga jinsi utekelezaji wake ni mbovu anavyoshindwa kusimamia kazi na kuna barabara zangu mbili ambazo ameshindwa kabisa kuzisimamia na tumepata hasara kwa sababu amezitengeneza katika kipindi cha mwaka mmoja barabara hizo zikawa zinaharibika sana. Ni kwamba tumepoteza fedha bure. Barabara ya kutoka Myunga kuja Kaengesa ilitengenezwa kwa usimamizi wa mkandarasi huyu lakini haikuwa na mafanikio yoyote ni barabara iliyoharibika katika kipindi cha mwaka mmoja. Kwa bahati mbaya tulipewa fedha nyingine za kutengeneza barabara ya kutoka Kafukoka kwenda Samazi katika Ziwa Tanganyika, barabara hii nayo pia haikusimamiwa vizuri na huyu mkandarasi nayo pia ipo katika hatari ya kuharibika katika kipindi kifupi. Tumekuwa tukimlalamikia sana huyu mtu lakini Wizara imekaa kimya.

Mheshimiwa Spika, nimeandika barua sijajibiwa mpaka leo karibu sasa ni miaka miwili na huyu mtu anaendelea kuwepo pale, anaendelea kuharibu mali ya Wizara, mali ya Halmashauri. Waheshimiwa Madiwani, waliwahi kabisa kumkataa na kuiambia Wizara kwamba hatakiwi, lakini Wizara imekaa kimya haijatujibu wala haijafanya kitu. Sasa ina maana gani? Tuendelee kupoteza fedha kwa msimamizi ambaye hawezi, basi kama hafai kwetu tunaomba apelekwe mahali pengine inapoonekana labda pengine atafanya kazi vizuri. Lakini katika Halmashauri ameshindwa kuwajibika ipasavyo na kuweza kupoteza fedha za Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la barabara, nilikuwa naomba barabara inayotuunganisha na Wilaya ya Mbozi mpakani kuanzia Tunduma kupitia Kakozi - Namchinka - Kalembe ifunguliwe kwa sababu hii ni barabara inayopitia mpakani, itatusaidia sana katika suala la kuendeleza biashara katika sehemu hizo za mpakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishaji wa Halmashauri, tunapozungumza suala la wataalam wanaosaidia Halmashauri, lakini tuangalie suala la Madiwani, kila Mbunge anayesimama hapa na anazungumza kwamba utendaji wa kazi katika Halmashauri zetu ni pamoja na Waheshimiwa Madiwani. Waheshimiwa Madiwani, wasipopewa posho inayotosheleza kwa kweli utendaji wao unakuwa ni wa manung'uniko na tunashindwa kufanya kazi vizuri. Lakini hawa ndiyo wanaoandaa shughuli nyingi kwa ajili ya viongozi katika Wilaya na Mkoa. Tunaomba sana katika awamu ijayo Serikali iangalie uwezekano wa kuanza kuwalipa Madiwani mshahara hata kama ni wa kima cha chini ilimradi tu waweze kupata kitu kitachowasaidia wao waweze kushiriki vizuri katika kuisaidia Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, tunaomba Wizara isaidie sana kupata Maafisa Ugani watakaosambazwa katika Kata zetu ili waweze kusaidia katika kilimo maana kilimo bila wataalam wa kuweza kuwashauri wakulima kwa kweli tunapata matatizo. Zipo Kata nyingi sana hazina washauri wa kilimo ambao wangeweza kuwasaidia

wakulima kuwashauri kuhusu kilimo, lakini tumekuwa tukilalamika mara kwa mara lakini hawapatikani, tunaomba Wizara iangalie jinsi ya kuweza kuongeza hawa Maafisa Ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la usambazaji wa pembejeo ya ruzuku inayopatikana tunaomba iwafikie wananchi Vijijini isiishie Mijini tu kwa sababu wakulima wako Vijijini. Tunaposambaza mbolea tunawaachia Mijini wananchi wanaendelea kulalamika kwamba Serikali haiwaangalii. Sasa zile Kamati zilizoundwa ziangalie ni jinsi gani ya kuifikisha mbolea hii Vijijini ili iweze kuwasaidia wakulima na bei iweze kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya uongozi tunashukuru sana kwamba Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata wamepata elimu, elimu hii isiishie hapa waendelee kuelimishwa ili waweze kusaidia mipango ya maendeleo ya Vijiji kwa sababu wao ndiyo watakuwa washauri wakubwa hasa kwa kipindi hiki ambacho Serikali hasa Wizara yako inapeleka fedha nyingi sana Vijijini, hawa wakipata mafunzo mazuri watasaidia fedha zile ziweze kutumika vizuri ili ziweze kuleta maendeleo mazuri kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kalambo kwa jinsi walivyoshiriki katika kipindi cha miaka mitano vizuri sana katika masuala ya maendeleo na shughuli nyingi za ujenzi wa shule za msingi kwa mpango wa MMEM na shule za sekondari ambazo zinajengwa na kuzitaka Kata zile ambazo hazijakamilisha ujenzi wa sekondari nazo zijitahidi ili ziweze kujenga shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote niseme tu ahsante kwa kuniona. Labda tu nianze kwanza kwa kusema Wizara hii ni Wizara ya maana sana na inahitaji utulivu kwa wale ambao wanaiongoza kwa sababu inabeba karibu mzigo mzima wa Serikali na mambo yake yote. Lakini niseme tu sina tatizo na Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, sina tatizo na Naibu wake, labda kwa sababu ya jinsi wanavyoendesha mambo katika Wizara. Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, kama askari anatumia njia zote za *profession* yake kama askari kabla hajakwenda ku-*attack* anapeleka *racking* na baadaye ana-*lay strategy* na baadaye anashambulia. Kwa hiyo, mambo safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mizengo Pinda, siijui *profession* yake, lakini naambiwa ni Mwanasheria akiwa anasaidiwa na Katibu Mkuu wake, *they are all lawyers* kama ni *all lawyers* wanakwenda na *evidence* kabla hawajatoa maamuzi. Mambo yao yote kila wanapopelekewa mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge wanaziangalia vizuri sana. Nayasema haya kwa sababu kulikuwepo na *fracus* kidogo pale Bariadi, wametumia utulivu wao na *profession* yao kuhakikisha kwamba hiyo *fracus* imekwisha.

Nilitaka tu niseme nashukuru sana kwamba Wizara imesikia kilio cha watu wa Bariadi kwamba tulikuwa tunahitaji ku-*link* Wilaya ya Meatu na Bariadi na Magu ili watu wa kutoka Meatu wapite Bariadi waende Magu na waingie Mwanza kwa urahisi kwa kupitia barabara inayotoka Meatu inakuja mpaka Kisesa inaingia Bariadi kwa kupitia Mto Simiyu pale kwenye kijiji cha nyumbani kwetu Gambasingu.

Kulikuwa na tatizo la daraja watu wengine wakaamua kutengeneza daraja la mataluma, bila kujali *professionalism.* Lakini bahati mbaya hata Mkuu wa Mkoa na yeye akaingilia kati hilo jambo bila hata kujua undani wa yale mataluma umetoka wapi. Mtu ana-*insist* kutengeneza daraja la mataluma. *Engineers* wanasema hilo daraja la mataluma halitaweza kusimama pale kwa sababu mwamba uliopo pale kwenye Mto ni mwamba *permeable rock* ambao ukiweka unaweza kukatikatika. Ingekuwa *igneous rock may be* ungeweza ku-*hold* yale mataluma.

Mheshimiwa Spikka, Mkuu wa Mkoa anasema hapana nunueni mataluma na ana-*insist* watu wa Bariadi wanunue mataluma kitu ambacho ilikuwa ni kwa ajili ya Wilaya zote mbili Meatu pamoja na Kisesa. Meatu pale Mkuu wa Mkoa hakuweza kuangalia ni kitu gani kifanyike mpaka akamfanya Waziri aanze kuandika barua kwenda Bariadi ambayo tunamshukuru Mwenyezi Mungu ameepusha yale mambo na kwamba tunashukuru kwa milioni 95 ambazo mmetuahidi kwamba mtatupatia ili tulijenge lile daraja kwa kufuatana na *professionalism* ambayo ipo.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema tu kwamba sisi kama wanasiasa tuwape nafasi wataalam kule Mikoani*, engineers,* madaktari wafanye kazi zao kwa kufuatana na *profession* zao, tusiende na *whims* zetu tu za kisiasa ili tuweza ku-*achieve* tunachokihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Madiwani limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wote. Mimi nilitaka niseme tu kitu kimoja Diwani ni kiungo kikubwa sana kati yetu wote tulioko hapa. Lakini pia mtu mmoja akaniambia Madiwani hawastahili kulipwa mshahara, hawastahili kupewa posho, hawastahili kupewa vitu vingine isipokuwa kwa kutegemea uwezo wa Halmashauri zao kama fedha ipo. Mtu mwingine akasema hao ni watu wa kuchaguliwa tu.

Sasa kama ni kuchaguliwa mbona ninyi mnapata mishahara, mbona ninyi mnakopeshana magari, mbona kuanzia Rais wote ni wa kuchagulia basi lazima kuwe na *policy* kwamba sasa tangu leo mtu yeyote ambaye ni wa kuchaguliwa *should forget about salaries, should forget about allowances* ili tuweze kwenda sawa. Lakini mimi nilikuwa nafikiri ni jambo la msingi kabisa tumsaidie Diwani. Diwani posho yake ya shilingi 30,000 hahitaji kitu kikubwa sana, anahitaji mumuongezee kidogo tu. Kama anahitaji kikubwa zaidi anahitaji pikipiki *trial* ambayo anaweza kutoa kwenye posho yake ndogo akaweza kulipia. Lakini siyo tu anategemea pia na *resources* zingine kwa hiyo hata kama tungeliacha hilo wazi kwamba ni kuwakopesha Madiwani tuwakopeshe Madiwani kwa kufuatana na jinsi wanavyoweza kujieleza wao na namna gani wanaweza kulipia hizo pikipiki zao wakaweza kufanya kazi ambayo tunataka wafanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inasimamia kama nilivyosema mambo mengi sana. Wataalam wengi wawe wa ushirika, wawe wa elimu, wawe wa kilimo, wote wamepelekwa chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa chini ya usimamizi wa Wakurugenzi wa Halmashauri. Lakini tatizo kubwa ambalo lipo ambalo halipitii katika Ofisi yako Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ni kwamba Wizara nyingine zote zinapeleka *circulars* kwa hawa Wakuu wa Idara. *DEO* anapokea amri kutoka kwa *REO* ambayo imetoka moja kwa moja kutoka Wizarani bila kupitia kwako. Yule wa kilimo na yeye anatoa *directive* kwa watu wa kilimo bila kupitia kwako, matokeo yake pale ni *confusion* tu.

Sasa mimi nilikuwa nafikiria kwamba umefika wakati katika Wizara pamoja na Wizara ambazo mnazisaidia kujenga mambo yake kule chini mkae pamoja, mtengeneze *mechanism* ya *flow of orders.* Kama inatoka Wizara ya Elimu, basi ipitie kwako wewe ndiyo utoe amri kule kwenda kwa *REOs* na *DEOs. Confusion* zitatokea mara nyingi sana Walimu leo wanalalamika hawajui mwajiri wao ni nani kwa sababu *directive* zote hazitatokea, zinatoka Wizara ya Elimu, wewe mtu wa TAMISEMI hazikuhusu. Mganga wa Wilaya na yeye hivyo hivyo inafikia mpaka hatua kwamba ni wakati gani Wabunge wanaanza kuomba hata Mganga wa Wilaya atoke wapi, unakuta Mganga wa Wilaya siyo mwajiriwa wa Wizara ya Afya, lakini *directives* zote zinatoka Wizarani bila kupitia kwako.

Kwa hiyo, mimi naona hii *confusion,* baadaye mngetafuta *a mechanism* ambayo mngeweza kukaa pamoja mkaitengeza *flow of information* ipitie katika *centre* moja kwenda mahali pengine ili mtu anapojibu hoja ziweze kwenda hoja kwa mtiririko unaofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa suala la *Health Centres* na Hospitali za Wilaya, nitajielekeza katika Wilaya yangu ya Bariadi. Kuna *policy* ambayo inasema *health centre* itajengwa kwa sababu inaweza kukata kwa ajili ya watu 100,000. Watu 100,000 katika maeneo labda ya Kilwa inawezekana. Lakini kwa *population* ya Bariadi ambayo ina watu karibu 700,000 hiyo *policy* ya watu 100,000 *does not hold.* Lakini siyo huwa *population* tu ya watu 100,000 kwa sababu unaweza kuwa na watu 100,000 wako kwenye kamji, hiyo inawezekana.

Lakini hawa watu wanaishi kutoka kwenye *Health Centre* kwenda kwenye kijiji wanakoishi ni kilometa zaidi ya 20. Siyo hiyo tu ukiangalia *Health Centre* ya Byuna ambayo inahudumia kwa Kata zaidi ya sita umbali wake kutoka Kata moja kuja pale ni mbali sana.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiria kwamba sasa tubadilishe *policy* tusiangalie *population* tu kwa ajili ya kujenga *Health Centre,* tuangalie pia na mazingira ambayo yako katika lile eneo. Kata moja, inawezekana kabisa ikawa na watu zaidi ya 100,000. Ukiangalia Kata ya Nkololo ina watu wengi kuliko kata nyingine yoyote katika Wilaya ya Bariadi, lakini haina *Health Centre* pale zaidi ya ile ambayo tunasaidiwa na Baba Paroko ambayo lazima tumshukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunafikiria kwamba sasa hii *policy* ibadilike iwe kila katika kijiji au vijiji vitatu viwe na *health centre* moja, inasaidia zaidi watu kuwa karibu. Lakini siyo hiyo tu, ikama katika *health centres* na yenyewe ni tatizo. Ukiangalia hiyo, *health centre* ambayo nimeizungumza ya Byuna ina *medical assistant* mmoja, ina *nurse* mmoja na *nursing auxiliary* mmoja. Lakini matatizo yaliyoko pale ni makubwa sana. Kuna wagonjwa ambao wanatoka karibu Kata sita wanakwenda kwenye sehemu hiyo hiyo moja. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiria kwamba hata ile ikama nadhani tubadilishe iwe na watu wengi zaidi wa kuweza kusaidia watu ambao wanakwenda pale. Pia tuwapatie *facilities* ambazo zinatosheleza kuweza kuhudumia watu wote hao ambao wanakwenda kutibiwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikia kengele inalia lakini nilitaka kuzungumzia kwamba Wizara hii, pia inasimamia mambo ya demokrasia. Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wake wa mwanzo amezungumzia juu ya chaguzi za vijiji, vitongoji, mitaa na kadhalika. Akasifu sana kwamba Chama cha Mapinduzi, kilishinda kwa kishindo. Sasa hicho kishindo anachokisema tuangalie ni mazingira gani waliyoweza kushinda.

Mheshimiwa Spika, Temeke mlishinda kwa risasi, mkacharaza watu viboko, Bariadi mlishinda Vijiji kama vitatu/vinne kwa polisi kuchukua masanduku na sehemu nyingine nyingi. Mimi nilikuwa nafikiria jenga demokrasia wote mko wageni katika demokrasia ya vyama vingi, *temperature* zishuke na mjenge utaratibu wa kuvumiliana wakati wote ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmesikia hapa rafiki yangu mmoja alikuwa anazungumzia juu ya demokrasia, akazungumza kwamba vyama vingi hawana demokrasia, wana udikteta. Lakini kila chama kina udikteta wake. Ukimwambia mtu wewe kwa rangi yako huwezi kugombea Urais, kumwambia mtu kwa sababu ya uzee wake fomu zake haziwezi kuwa-*discussed,* ni sehemu mojawapo ya udikteta ambayo ni wa kidemokrasia katika kila chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama watu wa *UDP* waliweza wakakaa aidha, kwenye ma-*godown* au popote pale lakini wakatimiza lengo lao ni sehemu yao ya Katiba. Wote tunajua tunakotoka. Mimi najua ninakotoka Bariadi na hakuna mtu ambaye anaweza akaniambia kwamba sijui kesho, sijui tujiunga tuige demokrasia ya chama kingine, mimi nasema huyu aliyekuwa anasema haya ni debe tupu, aliyoyataja humu yote angojee siku ya mwisho, kupiga kelele humu ndani tutarudia tu maneno ya *Sir* Edward Heath mwaka 1971 na wewe ulikuwepo katika Serikali hii wakati Obote alikuwa anapiga kelele *Sir* Edward Heath alimwambia wewe endelea kupiga kelele humu, lakini sina uhakika kama utarudi katika nchi yako na mimi namwambia huyu aliyesema haya maneno sisi hali ya baadaye tunaielewa, yeye aendelee kupiga kelele ya kusema juu ya demokrasia ya chama kingine, juu ya *UDP* inakaa namna gani, lakini uhakika ni kwamba watu wa Bariadi hukumu wameshaitoa, wakati anapiga kelele humu kule Bariadi wamesha-m*ake judgement* na matokeo yanajulikana. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi mara ya pili nizungumze, kwanza kabisa naomba nimwambie Waziri mimi naunga mkono Wizara hii na hotuba yake kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Kibaha kuishukuru Wizara kututengea Halmashauri mbili, tunaomba kushukuru. Tunaamini mwenzangu Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Msabaha, akirudi kwa kupitia Jimbo la Halmashauri ya Kibaha Vijijini na mimi Mungu akinisaidia nikifanikiwa kupitia Mji basi tunawaahidi tutakuwa bega kwa bega kushirikiana katika maendeleo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa stendi ya Mailimoja, mwaka jana ilikuwa kasheshe katika Bunge hili lakini wananchi wa Mailimoja wanakushukuru Waziri, wanamshukuru Naibu Waziri na watendaji wenu wote kwa kusimamia kero yao na kwa kweli imekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niishukuru Wizara hii kwa kusimamia mgogoro wa nyumba za Ma-*DC,* sasa hivi hata kama yapo basi ni kidogo. Kwa hiyo, tunaomba tutoe shukrani zetu za dhati sana.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru pia sasa hivi barabara ya Picha ya Ndege-Tumbi-*TAMCO* kwa kweli imetengenezwa, tunaomba kutoa shukrani zetu za dhati. Wagonjwa walikuwa wanafia njiani kabla hawajafika hospitali hasa wale wa *accident,* lakini sasa barabara hiyo ni nzuri, wasiwasi wangu tu imemeshaanza kuwa na mabonde ile barabara, haijafika hata miezi mingapi. Naomba mkaitazame vizuri.

Ombi langu baada ya shukrani hizi namwomba Mheshimiwa Waziri kama ulifanya vizuri kero za wananchi na moja hujaifanya na nina wasiwasi suala zima la huyu Mhandisi au Afisa Majengo wa Kibaha kwa ajili ya viwanja alivyovichukua na kuvigawa, akisema hivi viwanja vya Wizara ya Ujenzi. Wizara ya Ujenzi ikilijibu swali imesema siyo vyake kama kaiba au kala rushwa au kavigawa, hakugawa viwanja vya Wizara yake. Kwa hiyo, naomba nirudi kwako hili suala kwa nini halishughulikiwi.

Mheshimiwa Spika, nimelizungumza kwenye Halmashauri halishughulikiwi. Nimelizungumza kwenye Mkutano wa Mkoa halikushughulikiwa. Je, au kuna wakubwa wanaohusika, ndiyo maana mnaogopa? Ikiwa lile tatizo la nyumba za ma-*DC* lilishughulikiwa na lilikuwa gumu, kwa nini hili lishughulikiwe? Samahani sana Mheshimiwa Waziri hili nalizungumza, nisingependa kabisa kukaa katika vifungu na vifungu kuanza kulumbana na Waziri ambaye kweli umefanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nashauri tu kwenye hili sasa hivi kwa sababu kuna Halmashauri mbili, Maafisa wa Ardhi wa kila Halmashauri washughulikie ardhi ya Halmashauri zao. Halmashauri isiishughulikie ardhi ya Halmashauri ya Mji na ndiyo tatizo la rushwa hapa linaendea. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba pia nishauri suala la barabara kwa maana ya barabara za Halmashauri. Sasa hivi bado fedha zinaletwa kwenye Halmashauri. Matokeo Halmashauri ya Mji haina pesa. Kwa hiyo, hawana kauli, naomba Halmashauri ya Mji na yenyewe itengewe fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, mimi naomba niwapongeze Wabunge wa Mkoa wa Pwani. Kwa kweli kwa ushirikiano, wamefanya kazi ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi mia kwa mia. Naomba niwapongeze na nawapongeza kwa dhati na hasa wakishirikiana na mimi Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa huu nimeshirikiana nao. Isipokuwa naomba kabisa nitoe shukrani bila ya aibu kwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, kwa jina la utani tunamwita Bulji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maendeleo aliyoyasimamia na pesa yake mwenyewe kutoa katika mfuko wake kwa maendeleo ya Mafia, kwa kweli imepita hata miaka 25 ya nyuma. Amefikia hatua huyu Mbunge mpaka kuwa maskini anapeleka watoto anawasomesha, anasomesha walimu. Hivi sasa kwa hela yake anapeleka ma-*nurse* tusaidieni ili apate lile ombi aliloomba yeye la kupatiwa ma-*bulldozer* na ikiwezekana kutengenezewa ile gati. Naomba msaidieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi. Hii Wilaya ni mpya, lakini maendeleo yake yamekuwa makubwa sana, akiziacha zile shughuli pesa zilizotengwa na Serikali na pesa yake mfukoni, amesababisha maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nichangie uchaguzi. Naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri, kama itawezekana Sheria muibadilishe katika chaguzi za Madiwani. Hili suala la kusema wafanyakazi wasiwe Madiwani, tutaweza kupata Madiwani wa wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ibaki ile ile ya kwamba mfanyakazi wa Halmashauri asingombee. Lakini wengine wagombee, wengi wana uwezo. Hili ningeomba ili tupate Madiwani wa kusimamia Halmashauri zeti vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili naomba basi muiruhusu *PCB* sasa hivi isimamie katika suala zima la chaguzi za Madiwani katika vyama, wapeni ruhusa kwa sababu tunaposema rushwa, isiwe tu Serikalini iwe pia katika vyama, izungumziwe pia katika *private sector* ili kuondoa suala la rushwa, hongo, sasa hivi tunalalamikiwa sijui takrima.

Mimi nasema takrima ni neno la Kiswahili linaloonyesha kwamba unatoa kitu kumpa mtu siyo kwa kumtaka kitu, ni kushukuru au ndugu yako amekuja nyumbani, unamkaribisha unampikia. Sasa neno la takrima lisibadilishwe kuwa na rushwa. Rushwa ni neno lingine na takrima ni neno lingine, isipokuwa mtu akitumia vibaya takrima. Naomba adhibitiwe kwa sababu takrima siyo rushwa. Kwa hiyo, mimi naomba Wanasheria, watu wengi wanazungumza, watu wa Chuo Kikuu, neno takrima kwa Kiswahili chake siyo rushwa ni ukarimu unaotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la tafsiri ya wakazi. Tanzania Bara tafsiri ya wakazi bado katika sheria haijatafsiriwa vizuri. Hivi sasa kwa ajili ya tafsiri hiyo kutokuwa nzuri matokeo tunasumbuliwa Wamafia na Wakojani. Wakojani ni kabila linalotoka Pemba. Hawa huwa wanakuja na madago yaani wanakuja wakifika wanakaa katika kambi kwa ajili ya uvuvi, zile kambi zinaitwa madago na wanapewa miezi mitatu kisha warudi.

Lakini matokeo Wakojani hawa wakifika pale wanafanya makusudi kuoa wake ambao hawawapeleki Pemba, wanabakisha Mafia na watoto. Lakini inapofika suala la uchaguzi ndio wanajiandikisha wanasema sisi wakazi. Wenzetu Zanzibar wameweka *clear* kwamba mkazi ni yule atakayekaa miaka mitatu eneo lile. Sasa hivi kwa Mafia sisi *CUF* itachukua kwa watu ambao sio Watanzania Bara wala si wa Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, kwa hiyo, mimi naomba hili suala la Mafia mlitazame vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu naomba tusaidiane. Suala la Utawala Bora ni suala la kuwaelimisha Madiwani suala zima rushwa na ikiwezekana hata kuwa-*encourage* wawe na chama cha kupambana na rushwa. Sasa hivi bado elimu haijakolea kwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, pikipiki za Watendaji wa Tarafa. Nazungumzia Tarafa kwamba sasa hivi wamepewa pikipiki lakini hela ya matengenezo hakuna, inabidi watoe hela zao, wawafuate Wabunge wao, wawafuate na wahisani mbalimbali watengeneze. Naomba watafutiwe pesa za matengenezo ya pikipiki hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya maboresho, Mheshimiwa Waziri uliahidi Wabunge utawapa mafunzo ya maboresho. Bado hatujapata, kwa hiyo, siyo lazima kila Mbunge anajua kila kitu. Kwa hiyo, tunaomba haya mafunzo yatolewe kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, *SACCOS* ningeomba kabisa kwanza hili suala la *SACCOS* iwe ni utaratibu wa Wizara hii kuwaambia Halmashauri kila Kata iwe na *SACCOS* ili kwenye *SACCOS* hizi itasaidia wawe ma-*urgent* wa ile asilimia 10 na hela inayotoka kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Kazi, Maendeleo Vijana na Michezo. Nilikuwa naomba hizi *SACCOS* ndiyo zisaidie kuwa ma-*urgent* wazuri.

Lakini pia inatakiwa kwenye masuala mazima ya *SACCOS,* mafunzo yawe ya kutosha na tushirikiane na mabenki ambayo yamejitolewa. Kwa mfano *CRDB* imejitolea kutoa wataalam wake kwenda kufundisha watu masuala mazima ya *SACCOS.* Kwa hiyo, mimi ningeomba hiyo.

Mheshmiwa Spika, ajira ya Madaktari ni kweli nashukuru utumishi imetoa fursa hiyo. Lakini Halmashauri hazina hela ya kuwaajiri. Kwa hiyo, bado tatizo litabaki pale pale. Narudia nilimwomba Naibu Waziri, lakini naomba niseme hili ili anijibu kwamba tulikubaliana vizuizi visitumike kwa ajili ya kuchukua ushuru wa mazao. Lakini kwa

taarifa nilizonazo, ni kwamba Waziri umeruhusu baadhi ya Wilaya ziweke vizuia kuchukua mazao na Wilaya hiyo naomba niiseme ni Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, watu wanalalamika sana, mpaka wanafikia watu kupigana wale wenye mazao wanapigana na watu wa vizuizi. Kwa hiyo, naomba unisaidie hilo. Maafisa Ugani bado, hasa upande wa Kilimo hawajafanya kazi yao na ukweli inaonekana bado wananchi wanalima kilimo cha kizamani. Naomba tuweke taratibu nzuri, wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, mkulima akichukua ardhi ya mtu atapelekwa Mahakamani. Lakini mfugaji kupitisha ng'ombe unasema si tatizo. Naomba tukubaliane watengewe na wao maeneo ya kuchungia au ya kufuga au apewe ardhi kusudi wasiwe wanaingilia na wanachunga hovyo hovyo na kwa ajili ya kuoneana aibu ndiyo maana sasa hivi mpaka wakulima na wafugaji wanauwana.

Naomba kama wakulima wanapewa maeneo ya ardhi kulima, basi na wafugaji wapewe maeneo ya ardhi kuchunga kila mtu awe na eneo lake akiwa na ng'ombe 1,000 kwa hekta zake tatu shauri yake, atapunguza. Lakini kuwaachia ndiyo inasababisha vifo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kabisa nirudie tena nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Wizara na mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia isipokuwa tu anisaidie suala zima la huyu Afisa Majengo ama sivyo itabidi niinuke kwenye kifungu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Kwanza naomba nitangulize shukrani zangu kwa Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Kwa hiyo, naomba nikupe shukrani uzipokee na pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri amekuwa ni Waziri anayeijua kazi yake namba moja. Namba mbili amejitahidi kwa kina naamini amefika amefika kwangu mara mbili au tatu. Kwa hiyo, anaonyesha anaangalia kila kona ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama unavyonifahamu huwa siyo mwongeaji sana. Ni mtu wa vitendo, sasa wanasema siasa ili uwe bora lazima mdomo uchanganye, usipochanganya basi hawatakusikia. Lakini nalazimika pia niongee tu ili wajue kwamba badala ya vitendo pia najua kuongea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina maombi yangu ambayo napenda niyapeleke moja kwa moja kabla ya kuunga mkono. Ila kwa sasa hivi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 98.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutakuwa na 1.5 nitakayomalizia baada ya Mheshimiwa Waziri kunijibu. Nina maombi 9 namba moja, Mheshimiwa Waziri naomba Kibara iwe Mji Mdogo. Huu Mji tokea umekuwa ni eneo lililoendelea hata kabla ya Wilaya ya Bunda kuwa Makao Makuu, Kibara ilikuwa imeendelea. Lakini baada ya kuwa

tumeiacha kuiendeleza kwa kuipa mji mdogo imepoteza ile hadhi yake. Lakini ukiangalia katika Wilaya ya Bunda ni sehemu ambayo ina kipato kizuri na watu wake ni watu wema kabisa, wastaarabu waliondelea kimaadili na kiakili. Kwa hiyo, naomba pia ulione hili.

Mheshimiwa Spika, pili, tunaomba hospitali ya Kasaunga, Kibara ni Kituo cha Afya, kipewe gari la wagonjwa kwa sababu eneo ni kubwa, inahudumia eneo kubwa na haifiki sehemu nyingine kutokana kwamba hawana usafiri. Kwa hiyo, naiomba pia unifikishie ujumbe huu kwa Mheshimiwa Waziri na kwa sababu hospitali hii pia inahudumia ndugu zetu wa Ukerewe kwa hiyo, ukishindwa kufikisha ndugu zako watakuwa pia wanapata shida kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri lingine kuna vijiji kama vinne ambavyo ni vikubwa sana tungehitaji ikiwezekana vigawanywe ili kudumisha maendeleo ya pale. Vijiji hivyo ni pamoja na Nakatuba, Kistoria na Neruma, ni vikubwa kwa hiyo, tungeomba tuone uwezekano wa kuvigawa ili tuweze kufikisha huduma kwa wananchi.

Lingine pia ni kuhusiana na barabara ya Kibara. Ningeomba pia barabara hii ya Kibara inayotoka Bunda kuelekea Ukerewe nyumbani pako pale ambayo inapitia Kibara pia ihudumiwe kwa kina. Kwa kweli hii ni barabara mimi huwa naiita ya Mkoa kwa sababu inaunganisha Mkoa wa Mwanza na Mara.

Kwa hiyo, ningedhani kuna haja pia ya kufikisha ujumbe huu kwamba inahitaji kukarabatiwa kwa kina, ni muhimu sana na pia kwa ajili ya wavuvi wetu ambao wana samaki pale halafu pamba, kuna mambo mengi ambayo tungechangia Taifa hili kama barabara hii ingehudumiwa kwa kina kwa maana hata tutashindwa lami basi tuweke changarawe ya kutosha badala ya kuendelea kuikwangua.

Mheshimiwa Spika, halafu lingine ni kuhusu madini. Ninaomba nipendekeze Mwibara ina madini mengi sana. Ina madini *especially* dhahabu. Lakini tumeiomba Serikali yetu kwamba basi kama inawezekana itumilikishe sisi wakazi wa pale tuweze kuchimba na uwezo tunao. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba tuna uwezo wa kuchimba kama Geita.

Naomba ufikishe ujumbe huu kwamba tuna uwezo wa kufanya inachofanya *Geita Mining.* Lakini tumenyimwa kibali, nimewaomba wananchi wengi waombe, ili tumilikishwe lile eneo maadam sisi ndiyo wenyeji pale lakini wametukatalia katakata kwamba tayari kuna wazungu ambao wameshapewa hatimiliki za pale. Sasa inaniuma sana mpaka moyoni yaani ungekuwepo Mheshimiwa Waziri moyoni mwangu, nafikiri ungeshangaa. Hapa moyo unatetemeka kabisa kuona ardhi yao walikozaliwa babu zao wamezikwa, makaburi yao yatachimbuliwa, watakuja wageni watamiliki pale wakati sisi tuna uwezo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu chaguzi. Zimepita nafikiri mnajua kilichoendelea, hilo mnalijua. Huea mimi nasema anachojua mwenzio usimwambie kwa sababu anakijua kwa hiyo, ni kurekebisha tu utaangalia ufanyeje ili angalau maadili yetu

yaendelee kuwa mazuri ya kidemokrasia tuwatendee haki wote. Nilishuhudia uchaguzi katika Jimbo langu ilifikia sehemu nyingine nikakaa kwenye kiti nikaanza kucheka tu kwa sababu kitu kingine kinastaajabisha unaona hapana, kwa sababu kupigana huwezi. Ngumi unayo, lakini ukitumwa, wanakamata kamata. Kwa hiyo, unaona ngoja tu nikae, nicheke. Sasa itafikia sasa tuonekane vichaa kwa kucheka.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hilo unalijua. Kwa sababu si la kusema, unajua kabisa kwa sababu yanapangwa. Mengine yanapangwa, kwa hiyo, ulione kwamba kuna haja ya kuendesha demokrasia ya kweli siyo kama ilivyoendeshwa katika uchaguzi uliyopita. Ni aibu kwa Taifa letu ambalo wengi wanakuja kujifunza. Mna bahati moja Waheshimiwa kwamba wanapokuja kujifunza huwa hatusemi.

Sisi wapinzani wastaarabu mno. Mengi hatuyasemi kwa sababu ya maadili kwamba Tanzania yetu ni moja *and we love our country and then* hakuna haja ya kutoa kila kilichomo, mengine wanasema tutabadilisha pole pole kwa kuambizana humu. Kwa hiyo hakuna haja ya kusuguana wala nini.

Halafu lingine naomba pia niende kuipongeza Wizara kwa kina kabisa. Kama mnavyonifahamu mimi ni mwandishi wa vitabu na mwaka 1992 nilichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa *The Book Sellers Association of Tanzania.* Kazi ya kwanza ambayo mpaka leo hii nafikiri wanaendelea kunisifu ni kubadilisha mfumo wa kuwa tegemezi. Tulikuwa tuna-*import* vitabu kutoka Uingereza na kwingeneko na kama mnavyokumbuka Waheshimiwa Wabunge vitabu havikuwepo katika nchi hii bila kutoka Kenya au kwingine au Serikali itengeneze. Lakini nilibadilisha sera nikawahamasisha na mimi mwenyewe niliweza kutunga vitabu mwaka 1993 vya Sekondari na wenzangu pia niliwahamasisha tukaanza kutunga vitabu, nikawa Katibu Mkuu kwa miaka mitatu na baada ya kuja kuwa Mbunge nili-*retire* nikaamua kuacha. Juzi tena wameniomba baada ya wao kulegalega, sasa hivi mimi ni Makamu Mwenyekiti wa *The Sellers Association of Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakushukuru kwa Wizara yako kuwakubalia wauza vitabu wa nchini kwamba wauze na kweli mpaka leo hii ukiona vitabu vyote tunatunga ni Watanzania karibu wote ni Watanzania na tumeboresha vizuri kuliko hata Waingereza na kitabu kimoja kabla ya hapo kilikuwa kinauzwa kati ya dola 5 mpaka 10 kwa miaka hiyo. Leo hii tunakiuza kwa dola 2 mpaka dola 3.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani hata lengo lako Mheshimiwa Waziri isingefikia kama tungekuwa tunategemea nje kwamba tu-*import* vitabu. Kwa hiyo, naomba nitoe wito kwamba kuna haja Watanzania wenzetu kupewa mwamko na moyo na pia naomba mara nyingi WaheshimiwaWabunge huwa nikipiga wanafikiri siku zote ni dondoo tu. Lakini kuna dondoo inadondoka.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nidondoshe jambo moja kwamba kwa heshima ya Watanzania juzi nilikuwa nafanya kama masihara, *I didn't know* kwamba *you have to do such a things.* Nimeweza kuandika kitabu, nilikuwa na *hard time* ni kwa ajili ya Shule za Msingi. Kinaitwa, nitaomba nikionyeshe hapa kwa Waheshimiwa Wabunge

*(Hapa kitabu husika kilionyeshwa Bungeni na Mheshimiwa Mbunge kama kielelezo)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Hiki kitabu nitawaambia *why and why I am saying,* kinaitwa Mwongozo wa Utumiaji wa Kivuli cha Sayansi kwa Shule za Msingi, ni kwa nchi zote za *Comwonwealth* na kwa Kiingereza tunakiita *The Manual for Science Kit for Primary School.* Kwa hiyo, kinatumika kwa nchi zote na bahati njema nilikuwa ni kama masihara kama anavyosema lakini bahati njema katika dunia hii viko vitabu vitatu tu. Kimoja kimetengezwa yaani kwa ajili ya *Science Kit* nina *Science Kit* pia katika dunia hii ni Uingereza, India na Tanzania na Tanzania ni Mtanzania mmoja anaitwa Ndugu Muttamwega Mgaywa wa Mwibara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitabu hiki kimepita katika ubora na ni *the cheapest.* Kimekuwa ni bora kuzidi vitabu vya Uingereza na India kimepita na sasa hivi hapa unapokiona nimeletewa maombi kutoka nchi zaidi ya saba wanaomba kitafsiriwe katika Kiarabu pamoja na Kifaransa na Kiingereza na kwa Kiingereza nimeshamaliza kazi hiyo. Halafu Kifaransa nimewapa wataalam wanakiandika kwa ajili ya Shule zetu.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionyesha baadhi ya Kit kwa ajili ya Shule za Msingu Bungeni)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Kwa hiyo, ni kwamba ninaomba hizo pongezi nizifikishe kwenu na mimi kama Mtanzania ninayependa, ambaye nimesoma katika shule zetu nasema ni lazima niwajibike, nijiulize nimeitendea nini Tanzania yangu, mimi siyo malaika, sikusomea mbinguni wala kokote ni ninyi hawa hawa, wazee wetu mtumesomesha kwa Tanzania hii. Sasa basi naomba nitoe mchango wangu wa *kit* 300 zenye thamani ya shilingi milioni 120. Ninarudia Mheshimiwa Waziri nitapitishia mchango wangu kwako, *kit* hizi kwa Uingereza wanauza *kit* moja ni dola 1,000. Lakini sisi tunauza *at the cheapest* na ni bora kuliko *kit* za Uingereza na nime-*design* mimi mwenyewe Mtanzania mwenzenu na hiyo inanipa mwamko kwamba ni wajibu wangu pia niitumikie nchi yangu. Nitawasilisha hizi *kit* kwa Mheshimiwa Waziri na pia ningeomba azifikishe katika shule yetu au tuwape Waheshimiwa Wabunge wakati wanaondoka majimboni angalau waondoke nazo *kit* moja wawafikishie kwamba ni Mtanzania mwenzenu kafanya haya mawili matatu kwa niaba ya nchi. Kwa hiyo, nitawasilisha *kit* za milioni 120 kwako ili uweze kuwagawia Waheshimiwa Wabunge wafikishe majimboni kwao na la mwisho naomba nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa. Kwa kweli ni muungwana. Mimi nilikuwa naogopa sana CCM. Unajua CCM pia ni watu wazuri tu mnaweza mkaishi nao vizuri. *(Makofi)*

Sasa na yeye mwenyewe Mkuu wangu wa Mkoa ni uzao wa Mwalimu Julius Nyerere. Sasa mtu mmoja alinistua akasema unajua huyu ni uzao wa Mwalimu Julius Nyerere ni mtu nzuri tu, na kweli. Unajua wote ambao walikuwa na maadili ya Mwalimu Nyerere kwa kweli *they are good* yaani ni kwamba hana ubaguzi, hana ubaya. Yeye mnapambana naye tu wakati wa uchaguzi. Lakini atakupiga hata ngwala, lakini mkimaliza anakuambia kaa hapo, *let us go.* Ndiyo maana unaona Mkoa wetu umeendelea sana, kwa shule, kwa sababu hatubaguani na jimbo langu naomba niwahakikishie pia

limetangazwa juzi na *BBC* kwamba ni jimbo lililoendelea karibu kuliko majimbo mengi yakiwemo ya chama chetu ya CCM. Wamependekeza *BBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo siyo mimi, Waheshimiwa Wabunge wote walisikia *BBC* na wameomba hata Zanzibar waende kule Mwibara wajifunze kwamba kumbe upinzani siyo kuzuia, waliwaomba kule Zanzibar kwamba upinzani si kuzuia maendeleo ni kuwa pamoja kwenye maendeleo. Lakini msije kwangu tena, naomba maana yake watafikiri unono uko kule halafu wataning'oa, ndiyo tatizo la binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine pia naomba nimpongeze Ndugu Mkama kwa kweli Mkama anatoka jimboni kwangu amefanya ya maana sana Jijini Dar es Salaam. Dar es Salaam siyo ile. Naomba nifikishe lakini binadamu anasema kuna Mheshimiwa mmoja alikuwa ananichekesha siku moja anasema alimsifia ndugu yake mmoja alikuwa huko juu, baada ya kumsifia yule mtu akasema sasa bwana mimi hiki cheo hakinifai natakiwa niwe Mbunge. Sasa ndugu yangu Mkama naomba usije, lakini naomba nikupongeze. Maana yake ukimsifia Mbunge anataka Uwaziri, anataka awe Rais kama Muttamwega Mgaywa, juzi alikuwa anataka kugombea. Lakini yote hiyo ni sifa. Kwa hiyo, naomba pia hizo pongezi nimshukuru sana Mkama ametuonyesha picha nzuri kama uzawa wa Mwibara kwamba Mwibara pia ina watu ambao wanaweza kufanya mambo ya maana sana. Amelijenga Jiji la kule, kwa hiyo, naomba hata Mheshimiwa wakati unajenga Jiji lako la Tanga naomba u-*refer* kwamba amefanyaje mpaka Jiji lile limekuwa bora kuliko na Majiji tunayoyafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwashukuru naomba nimalizie kwa kusema hivi Watanzania wenzetu bado wana matatizo sana Mheshimiwa Waziri. Matatizo kuhusu matibabu, naomba kwa kweli nimepata shida, Watanzania hawana uwezo wa kulipia matatibabu. Juzi nilikuwa nasikia sikia wenzetu wageni ni kwa nini hatutoi matibabu angalau baadhi ya hospitali bure na sisi tunazo hospitali Mheshimiwa Waziri ambazo ziko katika maeneo ya *remote area* kama vijijini. Nafikiri kuna haja ya ku-*analyse* hata ile 500 mwananchi wa kawaida hawezi. Hawezi kabisa, tuangalie uwezekano wa kuwa na hospitali ambazo zitatoa huduma *free* yaani bure kabisa kwa ajili ya hawa Watanzania wenzetu hawana hata 200, mtu anakaa mwezi mzima mzunguko wake wa shilingi 200 haupo. Kwa hiyo, anapougua matokeo yake anaenda kwa mganga wa kienyeji kwa kumwambia nitaleta labda kuku au *what ever*. Sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri uangalie hili kwa kina, tuwe na hospitali kila angalau eneo fulani hospitlai za bure.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hilo naomba suala la madini. Nirudie tena sehemu ambako kuna vijiji na kuna madini naomba haki miliki ya ardhi iwe chini ya vijiji na wasimiliki ardhi ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nami nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza kabisa naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kutekeleza majukumu yao.

Nampongeza pia Katibu Mkuu wa Wizara hii na wataalam wote na watendaji wote kwa ngazi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba la kwanza kabisa nitakalopenda kulizungumzia nitapenda nizungumzie suala la UKIMWI. Napenda kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Wabunge wenzangu kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati nilipokuwa Mwenyekiti wa Wabunge wa kupambana na UKIMWI na kazi ambayo tumefanya nzuri humu Bungeni na nje ya Bunge na kuweza kufanya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Bunge la kwanza katika Bara la Afrika kuwa na umoja wa namna hii. Umoja huu pia umeweza kutambuliwa na nchi za *SADC* kwamba ni umoja wa kuigwa na nchi mbalimbali za *SADC.* Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeweza kutumia mifano hii kuelimisha Mabunge mbalimbali ndani ya Afrika na nje ya Afrika. Tumeweza pia kuelimisha Mabunge mengine na Kamati mbalimbali kwa hiyo, nawaomba Wabunge wenzangu tunapokua hapa tukienda huko wakati tunagombea *agenda* yetu tuendelee kuwa nayo ya mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie suala la kasoro iliyoko kwenye Muundo wa Kamati za UKIMWI zilizoundwa kwenye ngazi ya Wilaya na ngazi za Kata. Kasoro hii imeshasemwa na Wabunge wengine hasa kwenye Semina mbalimbali tulizoendesha. Ninaomba niseme, Mheshimiwa Waziri nimeshamwambia kwa mdomo, sasa naomba nizungumze hapa rasmi kwamba kasoro hii imewafanya Wabunge wanawake wa Viti Maalum na Madiwani wa Viti Maalum wasiweze kutoa mchango wao mzuri katika Kamati hizi.

Kwa sababu muundo huu umetamka kwamba Wajumbe ndani ya Kamati hii ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, atakuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Madiwani wawili mwanaume na mwanamke, watakuwa Wajumbe pamoja na Wabunge wa Majimbo. Hiyo ni Kamati ya UKIMWI ya Wilaya. Wabunge wa Majimbo, lakini wale Wabunge wa Viti Maalum walioko kwenye Halmashauri ile hawaruhusiwi kuwa Wajumbe katika Kamati hii.

Hapo ndio kasoro inapoanzia, tukichukulia kwamba waathirika wakubwa wa suala la UKIMWI na waliobeba majukumu makubwa ya kuuguza wagonjwa na kulea yatima ni wanawake na watoto wa kike, lakini inapokuja kwenye uwakilishi kwenye kutoa mawazo yao wale wanawake waliochaguliwa na wanawake wenzao huingia ndani ya Bunge na ambao ni Madiwani kwenye Halmashauri zao wanaachwa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alitazame hili na nitashukuru sana kama wakati aki *wind-up* hotuba yake litatolewa jibu leo hii hii ili tunapoendelea huko tukafanye kazi nzuri. Hii pia imekwenda mpaka kwenye Kamati za UKIMWI za Kata ambako muundo ni huo huo. Madiwani wa Viti Maalum hawaruhusiwi kuwa Wajumbe katika Kamati hizi. Sasa kama hawa Madiwani wa Viti Maalum ndio wanaohamasisha wanawake wote katika Kata na Vijiji kujiletea maendeleo na ndio

wanaowahamasisha wanawake kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya UKIMWI, inapofika kwenye maamuzi basi wenyewe wakae pembeni wanaume waamue. Kwa hiyo, hapo tunakuwa hatukutenda sawa tunaendeleza mfumo dume.

Kwa hiyo, ninaomba hili litolewe ufafanuzi ili tutakapoendelea, basi tuendelee vizuri ule muundo usahihishwe ili twende na kazi moja agenda ambayo Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza na mapambano dhidi ya UKIMWI ikiwa ni moja ya kazi nzuri inayofanywa na Chama hiki.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusisitizia na kuomba kwamba agenda ya UKIMWI kwenye Halmashauri zetu iwe ni kweli ya kudumu na ya vitendo. Kama tumeamua kwamba ni agenda ya kudumu, basi tuifanye kwa vitendo, tusingoje wakati tunafanya Semina tuna hela ndio tunaitisha Vikao. Iwe ni kweli kwamba Halmashauri zinaamua kuna siku zimetengwa kwa ajili ya kujadili tatizo la UKIMWI kwenye Halmashauri zao na iwe ni Halmashauri na Watendaji na Idara zilizoko kwamba; je, hivi kweli Idara za Serikali kuna siku zinakaa zinajadili matatizo ya UKIMWI yanayohusu Idara fulani, wagonjwa, wafanyakazi ambao wanaumwa, Idara inakaa inajadili ifanye nini?

Kwa hiyo, hili tunatakiwa tuanzie hapo, tuwe kweli na mkakati yaani twende kwenye vitendo. Tumeshakuwa na sera inayoeleza vizuri, tuna mkakati wa utekelezaji mzuri, lakini tutekeleze kwa vitendo tuhakikishe kama vile tunavyojadili masuala mbalimbali kila siku asubuhi, basi kuwe na siku hata mara moja kwa mwezi au itakavyokuwa imepangwa, kweli ijadiliwe na *minutes* hizo zionekane.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ninalopenda kulizungumzia ni uzazi salama. Akina mama wengi wanakufa na inakadiriwa kwamba wanawake wajawazito 16 kila siku hapa nchini wanakufa kutokana na matatizo ya uzazi salama. Lakini kwa sababu anakufa mmoja Lindi, mmoja Ludewa, mmoja kule Silali, hatuwezi kuwaona; mwingine Namtumbo, mwingine Peramiho, basi hatuwezi kujua kama hawa akina mama ni wengi kiasi gani, hivi kama kweli ingetokea hapo walipo watu 16 wamekufa kwa pamoja wote, tungeshituka.

Lakini hatuoni kama ni tatizo kwa sababu kila mmoja anakufa sehemu yake. Hii inatokana na matatizo ambayo yanaletwa shauri ya miundombinu au huduma ziko mbali, Wakunga wa jadi wako Vijijini huko, hawana vifaa. Siku hizi tumewapa mafunzo kwamba usizalishe bila kuwa na mipira ya kujihifadhi. Basi mama mjamzito anakwenda hawezi kumzalisha kwa sababu hana kinga, hawana motisha wahudumu wa afya ya msingi, hawaangaliwi vizuri.

Sasa kama hatuyatizami haya, Zahanati zetu au Vituo vya Afya havina wafanyakazi wa kutosha, mtu anahudumia ni *Nursing Auxiliary* anafanya kazi zote mpaka za kuzalisha. Basi hayo ndio matatizo yanayojitokeza. Kuna ucheleweshaji, mzazi amepata uchungu muda mrefu, anakaa mwishoni ndio hayo yanayotokea kwamba

anapoteza maisha.  Lakini ni maisha ambayo yangeweza kuokolewa, maisha ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, nafikiri sasa Mheshimiwa Waziri tunahitaji kuliangalia upya tufanye nini ili tupunguze vifo vya akina mama wajawazito, tufanye nini vijana wanaopata mimba katika umri mdogo hawajui lolote wanazalishwa kule Kijijini kwenye huduma ambazo ni duni. Kwa hiyo, tunahitaji kusisitizia suala la uzazi salama kwa undani zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine, kilio changu hata juzi nimesema, sasa naomba nirudie kusema, labda Mheshimiwa Waziri atanipa jibu.  Swali hili pia liliulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa nikapewa jibu kwamba Hospitali ya Ludewa inafanyiwa ukarabati na *Maternity Ward* na *Labour Ward* zinajengwa.  Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.  Naibu Waziri ameshatembela Hospitali ya Ludewa, ameona hali ilivyo, hakuna *Labour Ward,* kapo kachumba kadogo na mimi narudia kusema hili suala, ninaomba *Maternity Ward* na *Labour Ward* Wilaya ya Ludewa, Hospitali ya Wilaya ya Ludewa iweze kujengwa angalau mwaka huu basi, ikifika mwisho wa mwaka na wao wawe wanapata huduma nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la wataalam wa ugani, wataalam wa ugani hawa ni *extension works.*  Wako wa aina nyingi, wataalam wa kilimo, wataalam wa mifugo, wataalam wa maliasili, wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, ingawaje wao sio wengi sana katika ngazi za Vijiji. Wataalam hawa wengi wao wakifika kule Vijijini wanakata tamaa, kwa sababu za huduma zilizopo, hawana mahali pa kuishi wanaangaika.

Kwa hiyo nafikiri kwamba tuanze pia kuangalia wataalam hawa wajengewe nyumba kama tumesema ni wa Kata, basi kila Kata iwe na nyumba za watumishi.  Hawa wataalam wapate hadhi!  Mtu ametoka Chuo Kikuu, Diploma yake au cheti chake anafika kule hana mahali pa kuishi anakuwa *frustrated,* basi anafanya mwishoni anaingia hata kwenye ulevi. Halafu tunasema hawafanyi kazi hawatimizi wajibu wao.  Watatimizaje wajibu wakati hawana nyumba, hawana vitendea kazi, hawana hata usafiri.? Kwa hiyo, hili tunatakiwa pia tulitizame vizuri.

Sasa hapo hapo kwenye Halmashauri, kuna Idara ya Kilimo.  Hiyo Idara ya Kilimo imeunganishwa na Idara ya Mifugo. Mkuu wa Idara anaweza kuwa ni Afisa Mifugo au anaweza kuwa ni Afisa Kilimo.  Sasa hawa watu wako katika Wizara mbili tofauti, inakuwaje wote wawe katika Idara moja, wakati mmoja anapokea maelekezo kutoka Wizara ya Mifugo na Maji, mwingine anapokea maelekezo kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula? Hapo pana utata, ninaomba huu utata pia uangaliwe ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Ofisi za Wenyeviti wa Mitaa. Mwenyekiti wa Mtaa Ofisi yake ni nyumbani kwake.  *Document* zile zote anazopewa anatunzia nyumbani kwake.  Hivi kweli tena ananiongezea Mjumbe hapa kwamba samahani, nyumbani kwake ndio Ofisi inakokaa, sasa kweli atafanya kazi vizuri huyu

kama nyumba yake huko chumbani ndio atakakotunzia *file* lake? Akiondoka, kila kitu kimeondoka, siri za Mtaa zote zitajulikana, kama ni mama au ni baba, basi siri zote ndani ya nyumba.

Hivi tuna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba zinajengwa Ofisi za Wenyeviti wa Mitaa? Hata kama na Vitongoji, ili watu waweze kuhudumiwa, kesi zinakuja zinaletwa ndani ya nyumba ya mtu, kama una chumba kimoja, basi utaleta pale utaondoka alale mtu ambaye amehukumiwa pale, labda amepigwa nyumbani kwake wamesema hawezi kurudi kule.

Mheshimiwa Spika, sasa kweli ndio tunavyoendesha shughuli zetu hivi! Tunatakiwa tuangalie sasa hivi vitu na hasa tunapofika wakati wa kuajiri. Sasa hivi tunaajiri Watendaji wa Mitaa, watafanyia wapi kazi zao wakati wa Ofisi hazipo?

Mheshimiwa Spika, naomba niseme lingine na nichukue nafasi hii kumpongeza mwanafunzi, msichana Sara Mwamilawa, msichana ambaye ameongoza katika mtihani wa Kidato cha Sita na nimeambiwa kwamba yuko hapa Bungeni leo. Sasa naomba huko aliko sijui yuko wapi, asimame tu tumwone huko aliko na Wabunge waweze kumpungia mkono na kumpongeza. Sasa ninachotaka kusema sielewi kama kuna utaratibu. Yule pale, huyo hapo. *(Makofi)*

*(Hapa mwanafunzi Msichana Muhusika Alisimama na kuonekana na Waheshimiwa Wabunge)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Ninachotaka kusema ni kwamba utaratibu gani umewekwa wa kuangalia watoto wenye vipaji vyanamna hii ili kuweza kuwaendeleza? Kwa sababu ni vipaji ambavyo vinahitaji kuendelezwa! Nimesema hili, sijui kama nitapata nafasi ya kuzungumza kwenye Wizara ya Elimu kwamba liangaliwe, hawa watoto waendelezwe kutumia vipaji vyao, lakini pia watumike kuelimisha watoto wenzao wenyewe wanafanyaje ili kuweza kufikia hatua hiyo waliyofikia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nirudie kusema kwamba ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Cheyo amesema kwamba debe shinda halitikisiki. Nimesema CCM ni debe shinda halitikisiki ila debe tupu lenyewe linavuma tu linayumbayumba. Kwa hiyo, nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri waliyoifanya na naunga mkono hii bajeti kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawatakia mafanikio katika hotuba yenu.

Pili, wananchi na viongozi wa Nachingwea wamefanya kazi kubwa sana ya kujenga jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri Kuu ya Wilaya. Wanastahili

kupongezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri awapongeze wananchi wangu kwa kuchangia zaidi ya shilingi milioni 500 kupitia mazao na wafanyabiashara. Likitoka tamko Bungeni la kuwapongeza wananchi hao na viongozi wao, itatutia moyo sana.

Mheshimiwa Spika, jengo ni zuri lakini bado kuna kasoro. Tangu jengo lianze, mahesabu hayajakaguliwa. Hata Tume aliyoiunda *RC* wa Lindi, Mheshimiwa Nicodemus Banduka imeshauri mahesabu yakaguliwe. Nimeshangazwa na barua ya *RC* aliyokuletea hivi karibuni akisema Tume haikubaini wizi! Kama Mbunge sijawahi kudai kuna wizi. Nimedai na ninadai maelezo ya kina pakiwa na *audited report*. Huyu mwizi anayesema hayupo, utampataje mwizi kama unamtafuta mwizi bila ku-*audit* vitabu?

Mheshimiwa Spika, kwenye barua ya *RC* amedai jengo ni zuri sana. Nakubaliana naye 100% lakini sielewi kwa nini *RC* hata baada ya kushauriwa na Tume yake hakukueleza kuwa ataagiza matumizi ya jengo yakaguliwe na *independent auditors*. Siyo suala la ngedere kwa ngedere.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba *RC* asifumbe macho na kuonyesha kuwa Mbunge kudai *audit* kwa *public funds* ni ukorofi. Tupate *audited report*. Kuna wanaofikiri jengo hilo litaniuwa kisiasa, *no*! Ni kazi ya Mbunge kudai *audited report*.

Mheshimiwa Spika, tatu, wapongezeni wananchi kwa kujenga shule za sekondari 24 kila Kata.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaheshimu sana haki za binadamu na utawala bora lakini yapo maeneo ambayo yakiachwa yaendelee bila kupatiwa ufumbuzi, dhana nzima ya utawala bora na haki za binadamu hayatakuwa na maana. Kwa mfano, Wilaya ya Bukombe ina idadi ya watu 394,220, ina vijiji 128, Kata 14 na Tarafa 3 na kwa muundo huu wa maeneo ya utawala wananchi wamekuwa hawapati huduma za kiutawala na kijamii kama inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kugawa maeneo ya kiutawala katika Wilaya ya Bukombe ikianzia na Wilaya yenyewe, Tarafa, Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bukombe ina upungufu mkubwa wa maji. Kuna mradi wa maji ambao umeanzishwa mwaka 2002 lakini mpaka sasa dalili za kukamilika kwa mradi huu hazipo na kuna hisia za kuhujumiwa kwa mradi huo. Hivyo, naomba Serikali ifuatilie maendeleo ya mradi huu ili wananchi wa Mji wa Ushirombo waondokane na kero ya kutokuwa na maji.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine iliyoko katika Wilaya ya Bukombe ni mishahara ya Watendaji wa Vijiji. Watendaji hawa pamoja na kwamba baadhi yao hawakubahatika kupata ajira mpya lakini hata haki zao hawajalipwa. Hivyo Serikali iwajibike kuwalipa haraka Watendaji hawa.

Mheshimiwa, mwisho napongeza bajeti hii, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kazi nzuri ya kuliongoza Bunge. Naunga mkono hoja asilimia 100. Nawapongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi na Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kuwa mgombea Urais kwa tiketi ya CCM na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa mgombea mwenza, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kuwa mgombea Urais kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo machache. Kwanza ni sekta ya afya. Pamoja na kuwa na mifuko mingi yenye nia ya kuboresha huduma za afya ikiwemo *Basket Fund* na kadhalika bila kuwa na wataalamu kama rasilimali watu tutaendelea kuwa na huduma mbovu.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo ni kwa nini Hospitali ya Wilaya ya Handeni kwa takribani miaka mitatu sasa haina *DMO* mbali ya kuwa na Madaktari wachache sana wasaidizi *(AMOs)* wanne, ukizingatia kwamba Hospitali ya Wilaya ya Handeni inahudumia zaidi ya watu laki nne wakiwa ni wananchi wa Wilaya mbili za Handeni na Kilindi. Ingawa kila siku ukihoji jibu ni kuwa hakuna mtaalam anayekubali kuja Handeni mwenye *Masters in Public Health*. Sasa nani atalivalia njuga suala hili? Wananchi waendelee kuteseka mpaka lini? Wizara ya TAMISEMI inawaeleza nini wananchi wa Handeni na Kilindi wanaopoteza maisha yao kwa tatizo linaloweza kutatulika?

Mheshimiwa Waziri kwa vile wewe ni mmojawapo wa Wabunge wa Mkoa wa Tanga, naamini utanipa jibu la kuniridhisha ukiwa kama mkereketwa, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, bado kuna haja ya kuboresha huduma za afya Handeni kutokana na tatizo nililotaja hapo juu. Suala la kuwepo kituo cha Afya Kata ya Chamka linasuasua. Mheshimiwa Waziri ni vipi utatusaidia ili kituo hicho cha afya kiweze kujengwa kwani itasaidia sana kupunguza mzigo mkubwa unaoibeba hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kukosekana kwa waganga katika Zahanati ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi na zimeisha, tayari zinazo *kits,* lakini hazina watumishi na hazijaanza kazi. Mfano Zahanati ya Kwasunga, Kiva katika Wilaya ya Handeni.

Mheshimiwa Spika, VVU/UKIMWI bado ni tatizo. Fedha ambazo zinapitia *Global Fund for HIV/AIDS* haziwafikii walengwa vijijini. Inaonekana Kamati za UKIMWI/VVU katika Halmashauri bado hazijaweza kupanga *strategies* zao ili kumfaidisha mwathirika. Bado kuna umuhimu wa kuangalia kwa karibu eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa vile mambo mengine yameainishwa katika hotuba, ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wake utakuwa makini.

Mwisho, nawapongeza tena Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri, nawatakia kheri ili waweze kurudi kuendeleza mipango yao. Nawapongeza pia Watendaji kupitia kwa Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuupongeza uongozi wa Wizara hii kwa kusikiliza na kuchukua hatua za kuwaondolea wananchi wa Tarafa ya Nangaru kero sugu ya barabara ya Mtutu hadi Nangaru.

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Ndugu D. Mmari kumtuma *Engineer* Lymo kwenda Nangaru kujionea hali halisi ya barabara hiyo. Matokeo ni ya kutia moyo. Daraja la Nangaru limekamilika na sasa mkandarasi anaendelea na ukarabati katika maeneo korofi ili barabara hii iweze kupitika mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imetupatia shilingi milioni 100 mwaka wa fedha 2004/2005 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Lindi, kijijini Kitomanga. Inatia moyo kuona kuwa mwaka wa fedha 2005/2006 tumepangiwa tena shilingi milioni 100. Naomba Wizara itusaidie usimamizi wa karibu ili ipate fursa ya kuona namna ya kuharakisha umaliziwaji wa awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atufikirie kwa umakini na umuhimu wa pekee juu ya maombi yafuatayo:-

(a) Uandikishwaji wa Vitongoji vifuatavyo ili viwe vijiji:-

(i) Ruvu – Kata ya Mchinga;
(ii) Kitohavi – Kata ya Matimba;
(iii) Rucheni – Kata ya Milola.

Mheshimiwa Spika, maombi tayari yalishatumwa Wilayani na kila kitongoji kina shule ya msingi.

Naomba tufikiriwe juu ya ujenzi wa barabara za:-

(i) Mikalawanje – Mtumbikile – Matimba;
(ii) Mkwajuni – Lihimilo – Namkongo;
(iii) Milola – Namtamba;
(iv) Milola – Kiwawa;
(v) Mchinga – Kijiweni.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inasimamia shughuli za Wizara nyingi huko Wilayani kama vile elimu, maji, afya, ustawi wa jamii, maendeleo ya vijana na michezo, kilimo na kadhalika.

Napenda kushauri kuwa Wizara ambazo shughuli zao kwa kiasi kikubwa zinasimamiwa na TAMISEMI huko Wilayani ziangalie namna bora ya kuwawezesha wataalamu wao kitaaluma na kitaalumu ili kuzipunguzia mzigo Halmashauri na kuongeza ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, Naibu wake, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Katibu Mkuu, Ndugu Deo Mmari pamoja na wataalam husika kwa hotuba nzuri ambayo naiunga mkono kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nashauri juhudi zifanywe kuboresha maelewano ya kimajukumu kati ya Wizara hii na Wizara mbalimbali kama afya na kadhalika kwani mara nyingi maamuzi mbalimbali ya maendeleo au watumishi yamekuwa yakiyumba au kuchelewa kutekelezwa kutokana na migongano ya majukumu kati ya Wizara hii na Wizara mbalimbali husika na maamuzi hayo. Hali hii pia inachangia kuleta *personality crashes* katika baadhi ya Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi hazina uwezo hasa zile zilizoko nje ya Miji Mikuu kwani kipato cha Wilaya ni kidogo kwa vile hazina miundombinu ya kiuchumi, hazina makampuni wala viwanda, ni wakulima tu ambao mazao yao yanategemea hali ya hewa na hivyo kipato chao hakina uhakika hata wa bei ya mazao kama ufuta na korosho kwa Liwale. Hali hiyo pia inachangia uduni wa maisha ya Madiwani ambao ni kiungo kikubwa cha kusukuma maendeleo hadi vijijini. Nashauri Serikali iwatengee Madiwani fedha kiasi fulani wapewe wakati wa kumaliza muda wao wa miaka mitano. Halmashauri ziwajibike kuongeza kiasi kitachopatikana kulingana na uwezo wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi hazina miundombinu ya kutosha kuruhusu Benki kutoa mikopo kwa watumishi waliopo katika Halmashauri. Kwa mfano watumishi wa Halmashauri ya Liwale mpaka hivi sasa bado hawajafanikiwa kupata mikopo ya *NMB* kama ilivyo Wilaya nyingine kwa madai kwamba mawasiliano ya kibenki na makao makuu hayajakamilika.

Hivyo watumishi hawa wananyimwa fursa ya kujiendeleza. Nimefuatilia kwa karibu kwenye vyombo husika lakini mafanikio bado. Pia Benki ya Posta wameonyesha nia ya kuwakopesha watumishi wa Halmashauri nchini lakini wanadai sharti la makato ya mikopo hiyo ifanyike hazina na sio kwenye Halmashauri husika. Kwa nini Wizara isiwasiliane na Wizara ya Fedha ili sharti hilo lijadiliwe na kuafikiwa ili watumishi walio

chini ya Halmashauri nchi kote wafaidike na mikopo hiyo wakiwemo watumishi wa Wilaya Liwale?

Hivyo nashauri, Serikali ichukue hatua za dhati kuwasaidia watumishi wa Halmashauri kufaidika na *facilities* za mikopo nchi nzima. Hali hii itawafanya wafanyakazi/watumishi hasa Walimu wa shule za msingi na wengine wote walioko chini ya Halmashauri kuwa na motisha ya kufanya kazi vizuri kwenye Halmashauri yoyote nchini ikiwemo ya Liwale.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwishoni mwa mwaka jana palikuwa na mpango wa kupeleka magari ya ukaguzi wa ujenzi wa barabara Wilayani kwa ajili ya Mhandisi wa Wilaya na Wilaya ya Liwale ni mojawapo ilifikiriwa kuwa Wilaya ya kwanza kupata, mpango huo umefikia wapi kwani mategemeo ya awali ilikuwa kabla ya Machi, 2005.

Pia nashauri Wizara kuzipatia Wilaya gari kubwa kwa shughuli za maendeleo. Kwa Wilaya ya Liwale yenye *39,000sq* kms barabara zake ni ndefu na wakati wa masika gari iliyopo imefanya kazi ngumu ya ziada na ya masafa marefu imechakaa na ni mzigo kwa Halmashauri kwani linahitaji matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga tena mkono kwa 100%.

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI, Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mizengo Pinda, Katibu Mkuu, Ndugu Mmari, Watendaji wataalam wote wa Wizara na wengine wote ambao kwa njia moja au nyingine watakuwa wamechangia katika kukamilisha kwa ufanisi mkubwa sana matayarisho ya bajeti hii ya Wizara iliyopo mbele yetu leo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hotuba nzima hii ya Wizara, imeandaliwa vizuri na kuwasilishwa mbele ya Bunge vizuri sana. Naiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara katika maeneo yote lakini zaidi sana katika eneo la barabara vijijini (vifungu 18/19 ukurasa wa 11/120), kichocheo kikubwa cha uchumi na maendeleo yetu ni pamoja na barabara hizi. Wananchi wetu vijiji, wanazihitaji sana barabara hizi kwa safari zao wenyewe pamoja na usafirishaji wa mazao yao. Zaidi ya asilimia 90% ya wananchi wetu waishio vijijini wenye mtandao wa jumla ya kilomita 50,000 ni eneo linalohitaji kupewa umuhimu wa kiwango cha juu sana. Bagamoyo imenufaika na mpango huu unaosimamiwa vizuri sana na kutekelezwa kwa ufanisi wa kuridhisha sana. Bado tuna shida ya barabara za mjini Bagamoyo na zile zinazoelekea kwenye hoteli zetu za kitalii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kupongeza mpango mzima wa maendeleo ya elimu ya msingi (Vifungu 24/25, ukurasa wa16/18). Bagamoyo lilikuwa eneo la mfano wa shule duni sana kama vile shule ya msingi ya Mwetemo na Visezi. Leo shule hizi zina sura mpya, nzuri na zinazovutia sana. Kwa ujumla shule zetu za msingi Bagamoyo zimepitia mabadiliko makubwa sana chini ya mpango huu. Naipongeza kwa dhati Wizara

katika kusimamia vizuri mpango huu kiasi cha cha utekelezaji wake kuwa mzuri sana hasa Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kugusia Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo, (Kifungu cha 30, ukurasa wa 21). Naelewa na napongeza sana dhamira njema na mikakati mahususi ambayo Wizara inaitekeleza kwa madhumuni ya kuona Chuo kinatekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa ndani ya sheria iliyokianzisha. Katika hili, napenda kutoa pongezi maalum na za dhati kabisa kwa Katibu Mkuu, Ndugu Mmari.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu amekuwa akikipa Chuo hiki umuhimu na misaada pia upendeleo wa kipekee katika kuhakikisha Chuo kinafanya kazi kwa hali yoyote. Katibu Mkuu amejihusisha kwa karibu sana na Chuo chetu cha Hombolo. Tunampongeza na tunamshukuru kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Wizara katika kutoa msukumo maalum kwa maendeleo vijijini (kifungu cha 34 ukurasa wa 23). Sera ya maendeleo vijijini (kifungu cha 45/47, ukurasa wa 28/30). Inatia moyo sana kuona namna Wizara inavyotambua umuhimu wa kusimamia maendeleo yetu vijijini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia Wizara juu ya suala la Mfuko wa Mikopo ya Wanawake na Vijana (Kifungu 48 ukurasa wa 30/31). Hesabu za Halmashauri (ukurasa wa 43 kifungu cha 67). Napenda kuipongeza sana Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hassan Ngwilizi, Mbunge na Waziri wa Nchi, TAMISEMI kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yake. Pia nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa kazi nzuri anazofanya. Kwa namna ya pekee pia nampongeza Katibu Mkuu, Ndugu Deo Mmari kwa kuongoza mabadiliko makubwa katika Wizara hii ambayo leo hii kila mmoja wetu ni shahidi. Napongeza timu nzima ya Wizara hii kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja yenyewe, naishukuru sana Serikali kwa kuleta mpango wa Kitaifa wa usafiri vijijini kwa kushirikiana na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la *NORAD.* Jitihada hizi ni hakika zitaleta mapinduzi makubwa katika ujenzi wa barabara vijijini ambapo ni msingi mkubwa katika mikakati wa kuondoa umaskini na kuharakisha maendeleo vijijini. Naomba Wilaya yangu ya Babati ifikiriwe katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupiga vita rushwa, eneo mojawapo ni la zabuni. Tunajua sasa elimu ya kutosha imetolewa lakini ningeshauri kuwa ndani ya Halmashauri zetu eneo la zabuni lingeangaliwa kwa karibu zaidi. Usimamizi wa kazi ufanyike kwa karibu zaidi lakini pia wakandarasi wasibanwe sana na kucheleweshewa malipo yao. Hii inatokea sana mara nyingine inaashiria mwelekeo usio mzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maboresho, tunashukuru kazi kubwa imefanyika. Hapo awali wananchi waliwajibika katika kazi za maendeleo kwa nidhamu ikiwa ni pamoja na kuhudhuria mikutano mikuu ya vijiji. Wakikosa kufanya hivyo waliadhibiana, mtu aliweza kupigwa faini au kuchukuliwa mali yake na baadaye kulazimika kuigomboa. Nidhamu ilikuwepo. Siku hizi katika enzi ya maboresho ni vigumu au imekuwa vigumu kudhibiti vitendo vya ukosefu wa nidhamu. Watu hawa hawalazimiki kuhudhuria mikutano ya vijiji na hata kazi za maendeleo kama ilivyobainishwa katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 66 aya ya 98(iii) na hatua zinapochukuliwa kunakuwa na pingamizi nyingi zinazoishia Mahakamani, je, tutafanyeje?

Mheshimiwa Spika, tumeona mafanikio makubwa ya MMEM. Mpango huu unaishia mwaka 2006. Je, ni nini kinafuata baada ya mpango huu mkubwa kumalizika ili kufanya maendeleo ya elimu kuwa endelevu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, pamoja na mafanikio ya *CHF* Kitaifa bado *CHF* Babati ni sawa na hakuna, mafanikio yaliyopo ni *marginal* na hata taratibu zake hazijaeleweka kwa wananchi. Bado Zahanati na vituo vya afya vilivyo karibu na wananchi havijapangwa kutoa huduma za *CHF,* kitu kinachokatisha tamaa kwa wananchi kutoa michango yao. Tunaomba mtusaidie ili Babati iende sawasawa na sehemu zingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa vijiji naishukuru, Serikali kwa kazi nzuri iliyofanyika. Pamoja na zoezi kufanyika kuhusu usajili kwa vijiji vya Wilaya ya Babati kwa bahati mbaya kulikuwa na *omission* fulani ambayo iliacha vijiji sita vikiwa na sifa zote. Naomba vijiji vyetu vifuatavyo ambavyo maombi yake yako ofisini kwako visajiliwe ili kukamilisha zoezi zima kwa Wilaya yetu ya Babati.:-

1. Kijiji cha Mandi – Kaya 731;
2. Kijiji cha Managha – Kaya 980;
3. Kijiji cha Tsamasi – Kaya 802;
4. Kijiji cha Qash – Kaya 793;
5. Kijiji cha Erri – Kaya 790;
6. Kijiji cha Minjingu – Kata 906.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo na maombi hayo, napenda niseme naunga mkono hoja ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu mikopo ya vijana na akinamama. Ni wazo zuri Halmashauri kutumia wakala.

Ushauri wangu kwa kuwa tayari Serikali kupitia hotuba ya Mipango, imedhamiria kukuza *SACCOS* na mabenki kata, ni bora sasa 10% hizo zipelekwe katika *SACCOS* za vijana. Mfano mzuri ni *SACCOS* za Kiwilaya za wanawake Mkoa wa Ruvuma kwa nini zisifanyiwe majaribio kwa kuwa ziko pale *specific* kwa ajili ya Halmashauri zote?

Mheshimiwa Spika, pili, UKIMWI. Kanuni inayounda Kamati za Kudumu za UKIMWI katika Halmashauri, Miji, Manispaa, Jiji, inatamka wazi Wabunge wa Viti Maalum sio wajumbe, kwa nini? Naomba Serikali itupe maelezo kama dunia yote iko na wanawake, TAMISEMI haioni kuwa suala la afya wanawake wana mchango mkubwa?

Mheshimiwa Spika, tatu, Mfuko wa Pembejeo. Kwa kuwa sasa madaraka ya kuleta maendeleo ya jamii na hasa ndani ya MKUKUTA yako katika Halmashauri, ni lini Wizara itamaliza majadiliano ya kiutendaji na Serikali kufanya Mfuko wa Pembejeo kuwa chini ya TAMISEMI na hivyo kuwafikia walengwa kwa urahisi?

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu posho za Madiwani. Vyanzo vingi vya mapato vimefutwa na Serikali na hivyo kupunguza uwezo wa Halmashauri. Serikali ifikirie kuongeza posho za Madiwani na viinua mgongo vyao. Madiwani hupoteza muda wao mwingi wa kujiajiri kusimamia mipango ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, tano, posho za Wenyeviti wa Vijiji ziendane na za Watendaji au Madiwani. Tunapeleka pesa nyingi vijijini lakini wasimamiaji hawana posho (fedha mfukoni), ni hatari.

Mheshimiwa Spika, sita, maombi ya usajili wa vijiji, urasimu upunguzwe kama kijiji kinastahili baada ya kutimiza masharti basi kipewe.

Mheshimiwa Spika, saba, MMEM/MMES, kama ni kwa manufaa ya Watanzania, tunaomba katika kila shule basi kuwepo na madarasa ya MMEM na kila Kata mpango wa MMES ufike.

Mheshimiwa Spika, nane, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji kwa kazi nzuri.

**MHE. ALI A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii. Naomba nichangie katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kupambana na umaskini. Mheshimiwa Waziri, nafikiri wakati umefika sasa kwa Serikali kufikisha na kuratibu maendeleo ya wananchi moja kwa moja mpaka ngazi ya vijiji, kupitia Halmashauri (*Local Government*) ambazo sasa zimeimarika. Ninachosema hapa ni kwamba Serikali za vijiji sasa zipangiwe bajeti moja kwa moja na Serikali Kuu (ruzuku) ili wawe na mpango na vitu maalum vya kukamilisha kila mwaka katika ngazi ya kijiji. Kwa kufanya hivyo, kutakuwa na utatuzi wa kero maalum kila mwaka zinazoathiri uwezo wao wa kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pili, miundombinu, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na mfumo wa kujenga, kukarabati barabara za vijiji kwa kutumia kandarasi, ni muhimu katika maendeleo ya sasa ambayo yanaenda haraka kwa Halmashauri kuwa au kujenga uwezo wa kujenga barabara mpya na kukarabati barabara zote ambazo zitakuwa zimeathirika kila kipindi cha masika (mvua). Hii itapunguza

gharama za marudio yaani kukarabati barabara zile zile kila mwaka na ili kuweza (kupasua) kujenga barabara mpya ambazo kwa sasa zinahitajika sana na fedha ni finyu.

Kwa hiyo basi, ingefaa Wizara hii ilete Muswada wa Marekebisho Bungeni wa kufanya marekebisho katika sheria inayosimamia ujenzi wa barabara katika Halmashauri nchini ili katika kila Halmashauri kuwe na vyombo muhimu vya ujenzi wa barabara yaani *grader,* kijiko na *press* (trekta la kushindilia barabara) ili kuhakikisha barabara za kubeba mazao ziwe zinapitika wakati wote. Ni muhimu sana. Tafakari ifanyike.

Mheshimiwa Spika, tatu, mtendaji. Kumpa madaraka makubwa kama tulivyofanya hivi sasa Mkurugenzi Mtendaji ni hatari. Pale ambapo Mtendaji huyu ni mjanja mjanja akiweza kuwameza Madiwani ambao wengi wao ni maskini, kwa hiyo, kama *Accounting Officer* anaweza kuwamudu kwa urahisi tu. Hilo linapofanyika na *DC* anakuwa hana madaraka hata ya kukemea, ni hatari.

Kuna haja tukafiria upya *role* ya *DC* iwe inafahamika *as a moderating factor* katika Halmashauri. *Role* ya *DC* katika shughuli za Halmashauri kama *Governor* wa Wilaya lazima ifafanuliwe upya. Nashauri ingefaa *DC* awe mshauri mkuu wa shughuli zote katika Halmashauri husika ili katika Wilaya kuwe na kiongozi ambaye Mkurugenzi atawajibika kwake kwa kiwango fulani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa sio tu ni nzuri pia inatoa mwongozo katika maeneo mengi yanayowagusa wananchi vijijini na Wilayani. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wote wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongezi, sasa naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo katika maeneo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu watumishi kadhaa wa Halmashauri ya Iramba ambao sasa wamezamia zaidi kwenye biashara, ufisadi na hujuma badala ya kuwatumikia wananchi. Tarehe 4/11/2001, mimi na Mheshimiwa Mbunge wa Iramba Mashariki tuliandika barua na kuorodhesha majina ya watumishi tisa wa Halmashauri ya Iramba ambao wamekaa hapo Wilayani kwa miaka mingi sana na sasa wamejiingiza kutenda dhambi mbalimbali na kwa hiyo, tulimwomba Mheshimiwa Waziri awape uhamisho kutoka Halmashauri ya Iramba lakini mpaka sasa ni mtumishi mmoja tu amepata uhamisho. Watumishi wengine waliorodheshwa ambao Waziri hawajawapa uhamisho wanatambua wazi wazi kuwa Waheshimiwa Wabunge wa Iramba hawatuwezi, je, kama sio Mheshimiwa Waziri anawalinda watumishi hawa wanaovuruga maendeleo ya wananchi wa Halmashauri ya Iramba ni nini kilichomfanya Mheshimiwa Waziri asichukue hatua zinazofaa za kuwapa uhamisho au kuwastaafisha watumishi hawa kwa manufaa ya umma?

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako namwomba Mheshimiwa Waziri atoe majibu na maelezo ili kuwaridhisha wananchi wa Halmashauri ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, pili, barabara mbovu kiasi cha kuwatenga wananchi wa Kata ya Kidaru, Tulya, Ntwike na kadhalika. Kwa kweli inasikitisha kuona kuwa barabara zitokazo kijiji cha Kisiriri kupitia mlimani mpaka kijiji cha Kidaru na barabara kutoka kijiji cha Kisimba kupitia mlimani na kushukia kijiji cha Tulya (Mesi) mpaka Doromoni ni mbaya sana na kwa sasa hata gari yoyote ni hatari kujaribu kupita.

Mwaka 2002, mimi pamoja na Mkurugenzi *(DED)* tulimwomba Mheshimiwa Waziri aisaidie Halmashauri ya Iramba kuzitengeneza barabara hizi mbili haraka iwezekanavyo. Barabara hizi mbili ni za milimani na Halmashauri haina uwezo wa kuzitengeneza kwa kiwango cha kuweza kuwahudumia wananchi kibiashara na kijamii. Pasipokuona umuhimu wa kuzitengeneza barabara hizi mbili ni sawa na kuwaweka wananchi wa vijiji hivi kama wafungwa wa maisha na gereza lao lipo kwenye kisiwa. Hivi kweli Mheshimiwa Waziri anataka hali hii iendelee kuwatesa kimaendeleo wananchi wetu? Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aone umuhimu wa kuwafungulia wananchi wafungwa wa kiuchumi na kimaendeleo, vijiji vya Kidaru, Tyegelo, Luono, Megilango, Tulya, Doromoni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo Halmashauri ya Iramba inamsihi Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ni ile itokayo kijiji cha Sekenke machimboni kwenda Nkonkilangi, Nsunsu, Mingela, Doromoni mpaka Kidaru. Barabara hii inahitaji madaraja na ma-*drifts* kwenye mito na makorongo kutoka milimani. Halmashauri ya Iramba haina kabisa uwezo wa kuitengeneza barabara hii.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri angalau aone umuhimu wa kutoa msaada wa kujenga madaraja na ma-*drifts* kwenye barabara hii. Eneo zima ambapo barabara hii imepitia ni eneo muhimu kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mifugo, uvuvi, maliasili, utalii na madini.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza kuwa kama TAMISEMI itasaidia kujenga madaraja na ma-*drifts*, wananchi na viongozi wao wako tayari kushiriki kujenga (kulima) barabara mpaka kufikia kiwango cha kupitikia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya TAMISEMI.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Spika, hii ni nyongeza ya maelezo yangu niliyochangia kwa mdomo jana.

Mheshimiwa Spika, mwaka uliopita wakati kama huu nililalamika juu ya uamuzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo kuuza nyumba mbili mali ya kijiji cha Makiidi kwa wafanyakazi wake. Nyumba hizo zilikuwa zikitumika mahsusi kwa ajili ya wataalam wa mifugo ambao wamepangiwa kufanya kazi sehemu hizo. Ni kweli Serikali ilitoa mchango kidogo wa mabati na pengine saruji lakini nyumba hizo zilibaki kuwa mali ya kijiji. Hii ndiyo sababu hata Mahakama Kuu Kanda ya Moshi ilitoa amri ya kuzikamata na kuziuza kutekeleza hukumu katika kesi ya kijiji. Serikali hata wakati wowote haijajitokeza kutetea nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, tukiwa katika Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, tulielezwa kuwa nyumba hizo ziliuzwa na Wakala wa Nyumba wa Serikali. Sasa wanakijiji wa Makiidi wanauliza, tangu lini nyumba hizo zikawa mali ya Serikali? Hata kama ni za Serikali, je, kwenye mazingira ya vijijini, hivi mtumishi mwingine akiletwa pale kijijini ataishi wapi? Wananchi wa kijiji cha Makiidi wanaomba warejeshewe nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar es Salaam kumekuwa na watu wanaouza mashamba ya wananchi kwa kizingizio kuwa ni mashamba yaliyotelekezwa. Hawa wanajiita Serikali ya Kijiji wakati Dar es Salaam hakuna vijiji. Jambo hili liko hasa katika Kata ya Kibamba Manispaa ya Kinondoni. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya amekemea jambo hili na kuamuru wenyewe warudishiwe ardhi yao, lakini hawa watu wamekuwa na kiburi. Naomba Serikali itoe tamko juu ya jambo hili la sivyo kutakuwa na fujo na hali ya kutoiamini Serikali.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutambua nyumba zilizojengwa katika sehemu ambazo hazijapimwa. Sasa nina ombi. Katika eneo la Kunduchi, Pwani na Kondo Kata ya Kunduchi, Manispaa ya Kinondoni, kuna nyumba za aina hiyo lakini baadhi ya maeneo yamepimwa na kumilikishwa watu wageni wa maeneo hayo. Naomba umilikishwaji huo ubatilishwe na wenyeji wamilikishwe. Hii itawaokoa kutokana na adha ya kubomolewa nyumba zao. Hakutakuwa na hasara kwa wale waliomilikishwa kwa sababu hawajaviendeleza viwanja hivyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la Pwani ya Manispaa ya Kinondoni yaani Msasani, Mikocheni, Kawe, Kunduchi, Ununio, Kondo na Mbweni kuna shughuli za uvuvi ambazo zinaajiri watu wengi. Hata hivyo, kuna soko moja tu la samaki ambalo liko Msasani, soko la Kunduchi halina hali nzuri. Nashauri kuwa mipango iwepo ili bandari za uvuvi angalau mbili zijengwe katika maeneo haya. Pia masoko angalau mawili yajengwe na yapatiwe vifaa kama majokofu ili wavuvi waweze kutawala biashara yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali nyingi za miji na Wilaya wanao wanasheria ambao wanazishauri katika mambo ya sheria. Hata hivyo, imedhihirika kuwa uwezo wa wengi wao ni mdogo. Nashauri hali za wanasheria ziboreshwe ili wale wazuri, wenye uzoefu na uwezo waweze kushawishika kutafuta ajira katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, Idara ya Sheria Wizarani iongezewe nguvu ili tatizo la sheria ndogo ndogo za Halmashauri zinazopitishwa na Waziri zisiwe na mgongano ambao unaweza kuleta vurugu katika utendaji wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba na naunga mkono hoja yake.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara kwa kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Babati. Halmashauri mpya ya Babati sasa inahitaji kuwa na akaunti yake ili iweze

kuwa na mamlaka ya matumizi ya fedha. Utaratibu wa kugawana mali na watumishi usimamiwe kwa uangalifu ili wakurugenzi wawili wasije wakasukumiwa watendaji wabovu. Ni vema wale wabovu waondolewe na nina hakika waliokaa miaka mingi ambao hawawezi kuleta mabadiliko kwenye Halmashauri mpya ya Mji wa Babati na mali igawanywe kwa vigezo na umuhimu. Nashauri jambo hili lisimamiwe pia na Wizara.

Mheshimiwa Spika, pili, Halmashauri ya Mji wa Babati kwa *GN.352* inajumuisha Mitaa 35 na vijiji 13 ndani ya Halmashauri ya Mji. Hivyo inaonekana kuwa Halmashauri ya Mji imepewa watendaji 35 badala ya 48. Naomba watendaji 13 ambao inaonekana walisahauliwa tu, kibali cha hao 13 kitolewe ili katika kipindi cha uchaguzi kusitokee malalamiko ambayo yanaweza kurekebishwa kiutawala tu.

Mheshimiwa Spika, tatu, ugawaji wa vijiji. Vipo vijiji ambavyo havikusajiliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Babati imeshaleta mapendekezo yake. Tunaomba yashughulikiwe sasa ili kuondoa migogoro na malalamiko wakati huu.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali imeanzisha Halmashauri za Miji tatu yaani Babati, Korogwe na Kibaha. Lakini katika majedwali mgawanyo wa fedha za maendeleo inaoenakana Halmashauri ya Mji wa Babati imepewa fedha kidogo sana chini ya kitu kinachoitwa *general purpose,* imepewa shilingi 5,925,200 tu wakati Korogwe imepewa shilingi 122,155,200 na Kibaha imepewa shilingi 77,644,700. Vile vile chini ya mpango wa bajeti ya maendeleo 2005/2006 (jedwali 4) inaonyesha kuwa Halmashauri ya Mji wa Babati imepewa shilingi 5,746,200 na Halmashauri ya Wilaya ya Babati imepewa shilingi 177,018,200 na wakati huo huo Korogwe imepewa shilingi 662,519,200 na Kibaha shilingi milioni 27. Kwa maelezo hayo, napenda kufahamu fedha za maendeleo kwa Halmashauri ya Mji wa Babati ni hizo tu shilingi milioni 5 au zimewekwa wapi? Kwa nini kuna tofauti kubwa kati ya Halmashauri hizo za Mji mpya? Nitaomba ufafanuzi wakati wa vifungu au nipate maelezo wakati unajibu hoja.

Mheshimiwa Spika, nakutakia kazi njema.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa Wizara hii kwa juhudi, maarifa na maamuzi mbalimbali sahihi ya kuleta maendeleo ya jamii ya Watanzania kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ninalotaka kuchangia ni lile la mgawanyo wa Wilaya. Kwa hakika tunamshukuru sana Rais Benjamin William Mkapa, kwa uamuzi wake wa kugawa eneo la Wilaya yetu ya Shinyanga kuwa Wilaya mbili ambapo Kishapu imekuwa Wilaya mpya. Kimsingi, ni azma ya Serikali kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yetu ya Shinyanga vijijini iliyobaki baada ya kuzaliwa Kishapu, Makao yake Makuu bado yako Shinyanga Mjini, ombi na ushauri ni kwamba hali iliyopo sasa hivi ya kubaki na makao makuu mbali sana na wananchi wa Shinyanga vijijini kunaleta athari ya ufanisi wa kazi ikiwemo pia usimamizi wa karibu kwa viongozi wa Wilaya kwa miradi iliyoko katika Kata, Tarafa na vijiji. Aidha, wananchi wenyewe kushindwa kupata huduma ya viongozi wa Wilaya kwa sababu wako

mbali mno zaidi ya kilometa150. Naomba Serikali ianze kuona umuhimu wa kuhamishia makao makuu katika mji mdogo wa Iselamaguzi eneo ambalo ni katikati ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, aidha, *Health Centre* ya Nindo (Iselamagazi) ipandishwe daraja na kuwa na hadhi ya Hospitali ya Wilaya ili kukidhi mahitaji ya Wilaya hii.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopelekwa katika Halmashauri za Wilaya zetu kwa ajili ya ujenzi wa barabara kutokana na *Road Toll Fund* nashauri zikabidhiwe Wakala wa Barabara *(TANROAD* Mkoa) ili wasimamie ujenzi wa barabara za Wilaya badala ya Halmashauri ya Wilaya kwa sababu nyingi hazina Wahandisi walio na ujuzi unaokubalika. Matokeo yake ni kuwa usimamizi wa kipindi hiki kwa barabara zinazojengwa chini ya *Council* ni mbovu sana.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya Watendaji wa Vijiji na Kata, napenda kuipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuchukua dhamana hii lakini naomba sana mwaka huu walipwe mapema na aidha ufuatiliaji wa Wizara uwepo kwani wakati mwingine katika baadhi ya Wilaya watumishi hawa hukatwa fedha zao za mishahara kwa visingizio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni Madiwani kama wawakilishi wa wananchi ambao wana majukumu mengi sana. Naomba na kuishauri Serikali iandae utaratibu mpya wa mishahara, usafiri (pikipiki) na malipo yao ya mwisho (baada ya miaka mitano) yawe mazuri na yanayofanana na uzito wa kazi wanayofanya kwa wananchi wanaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naomba kutamka bayana kuwa naunga mkono hoja hii na naitakia Wizara hii ufanisi wa hali ya juu kwa majukumu yao kwa mwaka ujao 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza wote kwa kazi nzuri wanayofanya kuendeleza Wizara ya TAMISEMI. Pongezi za pekee zimwendee Waziri, Naibu Waziri mwenzangu, Katibu Mkuu na wengine wote. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, daraja la *Shan Cinema* (Morogoro Mjini). Nashukuru sana kwa jibu alilolitoa Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa Mheshimiwa Oscar Mloka kuhusu daraja hilo. Nashauri kazi hii ifanyike haraka kwani daraja hili lina hatihati lilijengwa *early 60s* sijui kama ukarabati umefanyika au la.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs)*. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote zenye *FDCs* kwa kazi nzuri wanayofanya kuviendeleza vyuo hivyo wakiwa Wenyeviti wa Bodi. Naomba wavisimamie kwa ukaribu sana kwani wanaonufaika ni wananchi wao.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kuna upungufu mkubwa wa Maafisa hawa hususani katika ngazi ya Vijiji/Kata. Hawa ni wahamasihaji wazuri sana katika maeneo yao wapewe hadhi wanayostahili kupata. Wao wanaohusika kote kote yaani ni mtambuka, kwa hiyo, kazi yao ithaminiwe na washirikishwe kikamilifu.

Nashukuru mahali wanaposhirikishwa, kazi ya kujitegemea/kujitolea na wananchi wanaitika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya wanawake na vijana. Tunashukuru baadhi ya Wakurugenzi wameanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu la kutenga 10% kwa mifuko hii miwili, ingawa hawajafikisha 10%. Waheshimiwa Wabunge wameshauri itungwe sheria kwani agizo halina meno.

Mheshimiwa Spika, *early childhood development (ECD*). Hii inawahusu watoto wenye umri wa 0 mpaka miaka 8. Inaelekea tumewasahau ukiacha afya, kwa upande wa afya tumesifiwa sana lakini elimu bado. Kila shule ya msingi inahitajika iwe na *pre-primary classes* lakini utakuta agizo hili halijafanyiwa kazi, husuani vijijini. Hawa watoto wanahitaji kutunzwa kikamilifu (*cross-cutting issue*). Bado shule zetu za Serikali *pre-primary* hazitoshi. Natoa pongezi kwa asasi, mashirika ya dini, watu binafsi kwa kuanzisha shule za awali. Katika programu ya *ESDP* (shule za awali) zilisahaulika.

Mheshimiwa Spika, tumejenga madarasa mengi katika mpango wa MMEM je, tumewafikiria walemavu? Je, majengo yana *provision* ya *slopes*, *toilets e.t.c for this special group?* Wakurugenzi wangeagizwa waweke *provisions* katika majengo yao kwa kundi hili. Kwa kweli wanafunzi walemavu wanapata matatizo ya kupanda hizo ngazi na kuvitumia vyoo vya kawaida.

Mheshimiwa Spika, shukrani.

Mheshimiwa Spika, *all is well, that ends well. Amin.*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake yote. Pamoja na pongezi hizo napenda kupata ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhus mradi wa *quick start,* (mahakama). Kwa vile nimekuwa na mawasiliano na Serikali kwa maana ya Waziri wa Sheria na hatimaye Waziri kurusha mpira kwa Katibu Mkuu TAMISEMI na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kufuatilia sula la *Quick Start* (Mahakamani) kwa barua kwa Katibu Mkuu TAMISEMI na hadi sasa hakuna hatua iliyochukuliwa. Je, kwa vile fedha za wananchi zilikusanywa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Karatu kupitia Makatibu Tarafa na hadi leo vitabu zaidi ya 149 (stakabadhi) hazijulikani ziliko japo waliokabidhiwa wanajulikana. Serikali inatoa kauli gani na inachukua hatua gani ili fedha za wananchi ziwe salama na kama zimpotea wahusika wanachukuliwa hatua gani?

Kwa vile Wizara ya Sheria na Katiba imefanya jitihada kufuatilia fedha hizo na hata kumtuma Mkurugenzi wake wa *Quick Start,* Karatu na kwa vile hata fedha zilizokusanywa shilingi milioni 9 au zimetumika vibaya au hazijulikani zilipo, Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa fedha hzi zinapatikana na kuelekezwa kwa malengo yanayohusika?

Je, Serikali inatoa maelekezo gani ya jumla ili imani ya wananchi waliotoa fedha zao kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama za mwanzo na Wilaya?

Mheshimiwa Spika, kwa vile *St. Joseph Hospital* ya Marekani ilitoa fedha kiasi cha shilingi 21,000,000 zaidi ya mwaka mmoja sasa kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Karatu *(DDH)* ambayo inaongozwa na Kanisa la KKKT Jimbo la Kaskazini; na kwa vile mradi huo umekwamishwa na kundi la watu wachache na kuungwa mkono na Mkuu wa Wilaya na hata baada ya Tume aliyounda Mkuu wa Wilaya kuagiza maji yapelekwe mara moja Hospitalini hakuna kinachoendelea na suala hili liko Ofisi ya Rais na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Je ni sababu ipi hasa imefanya mradi huu ukwame pamoja na kuwa Huduma ya Hospitali ni uhai wa Watanzania, na kwa kukosa maji hospitalini huduma nyingi zikiwemo za o*peration* zimekwama wakati kwa zaidi ya mwaka mmoja fedha siyo tu zinakaa bali kupoteza thamani pia.

Kwa vile wafadhili wa *St. Joseph Hospital,* wanaendesha mradi mkubwa wa *Village Wellness Program* katika kata tatu za Mbulumbulu, Rhotia na Eudamarariek na kwa sasa wametishia siyo tu kusimamisha mradi huo wa maji wa shilingi milioni 21 bali pia mradi wa *Village Wellness Program* wenye thamani ya shilingi 300,000,000 na wanafika 6.6 kwa uamuzi wa mwisho. Je, baada ya suala kufika kwa Mheshimiwa Rais (Barua ya Mkuu wa Jimbo kwa Rais) na kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mheshimiwa Mohamed  Babu ni kitu gani kimefanya ufumbuzi wa tatizo hilo usipatikane?

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa mradi utaanza?

Mheshimiwa Waziri ni imani yangu nitapata majibu ya kina kwa maswali yote haya mawili vinginevyo ninategemea pia kutuma kanuni wakati wa vifungu. Naamini hatuna sababu ya kufikia hatua hiyo.

Napenda kuomba ufafanuzi ufuatao, kwa vile Ubalozi wa Ubelgiji kupitia Wizara ya Afya na TAMISEMI ulilenga kufadhili mradi wa Elimu ya UKIMWI katika Wilaya Saba za Tanzania Bara ikiwemo Wilaya ya Karatu;  na kwa vile wataalam waliisha kupita katika Wilaya husika kufanya utafiti na Wizara ya TAMISEMI kueleza kuwa mpango huo ungeanza mwaka wa fedha 2004/2005 sasa je, kwa kuwa Wilaya hizo zilishajiandaa kupokea mradi huo wenye thamani ya shilingi milioni 144 kwa Wilaya umekwama wapi na ni matatizo gani ya msingi yaliyokwamisha mradi huo?

Mheshimiwa Spika, je, mradi huo sasa utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, taarifa niliyonayo na kuwa tumekwisha poteza fedha nyingi kwani sasa ni mwaka wa nne tangu Ubalozi wa Ubelgiji ulipotoa fedha kwa ajili ya

mpango huo na kila mwaka fedha zimetengwa ila tumeshindwa kuzitumia. Je, kwa utaratibu huu ni kweli kuwa tunaona UKIMWI kuwa Janga la Taifa linalohitaji *Emergency Action?* Natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Waziri, kwanza naunga mkono hoja ya Wizara yako.

Naomba tu nipewe ufafanuzi wa kina kuhusu mambo yafuatayo, kwanza ni Wizara yako kupitia Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya inawajibika kwa mambo gani ya Idara ya Elimu? Kumekuwa na kelele kuhusu mafao ya aina ya walimu, je, Wizara yako inahusika na kipi kuwa sababu ya matatizo hayo?

Pili, taarifa ya Tume ya Waziri Mkuu kuhusu Mafao ya Walimu uliipokeaje na umefanya nini kama matokeo ya taarifa hiyo.

Wabunge wa Viti Maalum huteuliwa kutokana na asilimia ya majimbo walioingia Bungeni na Wabunge hawa wa uteuzi wao huwa pia Madiwani wa Halmashauri za Wilaya zao wanazoishi. Je, Mbunge wa Viti Maalum wa chama fulani ambacho hakina Wabunge wa Majimbo katika Wilaya ambayo pia haishi Wilayani humo anaruhusiwa kuwa Diwani wa Wilaya kwa misingi ya sheria gani?

Mheshimiwa Spika, muundo wa Serikali wa kuchanganya mifugo, maji na kilimo inarahisishaje utendaji iwapo mifugo na maji ipo chini ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya mifugo na Kilimo chini ya Waziri wa Kilimo na Chakula wote chini ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya?

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja. Agizo la Rais la kugawa Kata na Tarafa katika Jimbo la Igalula hadi sasa bado kupata maelekezo.

Mheshimiwa Spika,tunaingia katika uchaguzi, wananchi wa Jimbo hili wamekuwa na kiu kusikia hayo aliyoyatenda mbele ya umma, wakati akihutubia mkutano wa hadhara huko Isikizya Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Spika, imekuwa kero kutoka kwa wananchi wa Jimbo hili na kuuliza kulikoni?

Mheshimiwa Spika, nitashukuru kusikia maelezo muafaka ya jambo hili ili katika kuhitimisha mjadala utamke kuna agizo la Rais linatekelezwa ili wananchi hao watoe salaam na shukrani kwa Rais na Wizara tekelezi ili imani iendelee kujengeka kwa Serikali na Tamko la Rais.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ninaomba ufafanuzi wa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Watendaji wa Kata ni watu muhimu sana, naomba kufahamu ni lini Wizara itafikiria kuboresha mishahara yao pamoja na kupewa usafiri wa pikipiki ama hata wa Serikali. Naomba ama kufahamu kama kuna mipango yoyote ya kuwahudumia watendaji hawa.

Katika kujibu hoja ya utengenezaji wa barabara za Manispaa ya Shinyanga katika Bajeti ya Wizara ya mwaka 2004/2005 Mheshimiwa Waziri ulisema kuwa barabara hizo zitaanza kutengenezwa kwa Bajeti ya 2004/2005 kwa mradi wa *EU.* Naambatanisha nakala. Kwa bahati mbaya hatukuona Juhudu za utekelezaji wa ahadi hiyo inatekelezwa. Niliandika barua kufuatilia sikuweza kupata majibu yoyote.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii sioni mahali popote ambapo imeonyesha kuwa barabara za Manispaa ya Shinyanga zitaboreshwa kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI inavyofanya katika Manispaa zingine za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo wakati Waziri anahitimisha Bajeti hii ya 2005/2006, vinginevyo naona ahadi hii iliyotolewa ni ya kulidanganya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mengine napongeza kwa kazi nzuri zilizofanywa na *Council* na Manispaa zake – Maji, Shule za Msingi na *Secondary School;* afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri kwa utekelezaji wa malengo mliyojiwekea kwenye Bajeti ya 2005/2006.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuiunga mkono hotuba ya Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia.

Aidha, napenda kutoa hoja zifuatazo, hitaji la Daktari wa Wilaya ya Namtumbo ni ombi la siku nyingi. Kwanza Wizara ya Afya ilimpendekeza TAMISEMI Dr. Aaron Chiduo lakini bila kuelewa sababu wenyewe TAMISEMI mkatengua uteuzi huu bila kuleta Daktari mwingine. Je, kulikoni? Ni lini tutampata Daktari huyo wa Wilaya? Ningeshukuru kupata jina nikawaeleza wapiga kura kabla ya tarehe 28 Julai 2005.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka minne sasa Halmashauri ya Wilaya Ulanga na Halmashauri ya Namtumbo tumekuwa tukishughulikia kuunganisha barabara kuu mbili za Mkoa. Barabara ya Mkoa ya Lupilo hadi Kijiji cha Kilosa kwa mpepo (Mkoa wa Morogoro) ili iungane na barabara ya Mkoa ya Lumecha hadi kijiji cha Kitanda (Mkoa wa Ruvuma).

Wizara ya Ujenzi imetoa msaada wa Fedha kujengea madaraja ya Mwatisi na Furua (Mlanga) na Mto Ilondo (Namtumbo) lakini fedha hazitoshi kumalizia kujenga barabara ya kiungo kuvuka mito mitatu niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, tayari Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma imependekeza barabara ya kiungo kati ya Kijiji cha Kitanda na Kijiji cha Kilosa kwa

Mpepo iwe ya Mkoa ili fedha zote zipatikane toka Wizara ya Ujenzi. Lakini bado jibu la Ujenzi wanashauri tutumie fedha za TAMISEMI, *Road Fund* tumalizie kazi hii Ndugu Shemangali anafahamu mradi huu. Tafadhali nithibitishiwe msaada toka kwako. Tayari michoro ya madaraja yote matatu – Furua, Mwatisi na Ilondo ni tayari.

Barabara hii ni muhimu kwa sababu tunaunganisha Mikoa ya Morogoro na Ruvuma, inarahisisha watalii kutoka *Mikumi National Park* kuja Namtumbo kutembelea mbuga kupitia *Selous Game Reserve*, kurahisisha kwa wananchi wa Namtumbo na Ulanga kutembeleana, tayari tumeoleana, kufupisha barabara, uchukuzi wa mazao ya chakula na biashara toka Namtumbo/Songea hadi Mikumi hadi Dar es Salaam bila ya kuzungusha kwanza Njombe na Iringa hadi Morogoro na Dar es Salaam na miradi mikubwa ya *Irrigation* ya Kitanda itazalisha mpunga mwingi ambao utakuwa rahisi kufika Dar es Salaam na hiyo kutekeleza MKUKUTA kwa vitendo. Aidha, mbao zitarahisisha kufika Dar es Salaam bila kuanza kupeleka Namtumbo na hatimaye kuzunguka Njombe na Iringa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Hombolo ni muhimu kutia mkazo kuwafunza Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Miji katika kuwapa o*rientation* na *refresher courses* ili kuwaandaa kusimamia maendeleo ya kijamii na kiuchumi Wilayani. Wengi wao ni dhaifu sana kwenye shughuli za *Extension Services* hasa katika kuwasimamia watumishi wa kilimo, mifugo, maliasili na maendeleo vijijini. Hii ilikuwa rahisi huko nyuma kupitia Chuo cha *Local Government* kule Mzumbe Chuo ambacho sasa ni *University.* Hakika tukitaka kuendelea haraka vijijini *DEDs* wasajiliwe kwenye *orientation courses* haraka sana. *DED* ni kiungo muhimu wa kusukuma maendeleo.

Kuhusu mfuko wa pembejeo. Mfuko huu ulipendekezwa kwa Bunge na Wizara ya Kilimo na sio TAMISEMI. Kwa sasa kwanza TAMISEMI ifanikishe huduma za *Extension* Wilayani ambako haziridhishi na Wizara ya Kilimo kulaumiwa Mfuko wa Pembejeo utasumbua sana! Katika miaka ya 1990 ulitusababishia deni la shilingi bilioni 5 kwa kutegemea sana Ofisi za Halmashauri! Napendekeza ikibidi Halmashauri zenyewe ziunde mifuko yao ya kununulia pembejeo kukidhi mahitaji ya pembejeo au vijana na wanawake.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, kwa Hotuba yake nzuri, iliyo wazi na yenye mwelekeo mzuri wa maendeleo ya Taifa letu hili la Tanzania na kwa Wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa thelathini na moja katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaeleza kuwa katika jitihada za kuboresha majukumu yake, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliandaa na kuwasilisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pendekezo la muundo mpya ambao ulipitishwa na

Kamati ya Utekelezaji ya Rais na hatimaye kuridhiwa na Mheshimiwa Rais mwezi Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, sambamba na pendekezo hili kwa nini hapakuwepo na pendekezo lingine ambalo lingewezesha Wizara hii kuwa ni moja kati ya Wizara za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo ipo katika Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nauliza hili hasa kwa kuzingatia kuwa Nchi yetu ya Tanzania ina jumla ya Mikoa ishirini na sita. Kati ya Mikoa hii ishirini na sita, Mikoa mitano iko Zanzibar, yaani Mikoa mitatu iko Unguja na Mikoa miwili iko Pemba. Kwa hiyo, kutokana na hali hii ni vizuri viongozi wetu wakuu wa nchi wakaliangalia suala hili na kuliwezesha Mikoa yetu yote kuwa katika usimamizi mzuri wa kimaendeleo kwa faida ya viongozi hawa wa Mikoa na Wilaya pamoja na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa aliyoitoa tarehe 26/4/2004 Uwanja wa Amani, Zanzibar kuadhimisha miaka arobaini ya Muungano wetu wa Tanzani alisema kuwa; "Muungano wetu wa mwaka 1964 haukuasisi umoja wetu, ulirejesha na kuudhihirisha tu umoja wetu, ulirejesha na kuudhihirisha tu umoja wetu. Ni vema vijana wetu wajue jambo hili."

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia historia ya chama chetu cha *TANU* inaeleza kuwa chama cha *TANU* kiliundwa mwaka 1954. *TANU* tunaelezwa kuwa ilikuwepo Malawi, Zambia, Zanzibar na Tabora. *TANU* muda wote ilikuwa inahimiza umoja na usawa.

Mheshimiwa Spika, umoja wa wananchi wa Taifa hili ni vizuri ukajengwa na kuimarishwa kuanzia katika Mikoa yetu yote ya Tanzania, Wilayani mwetu hadi vijijini ili kujenga Tanzania iliyo imara zaidi. Kwa hiyo, ni jambo la msingi kwa Mikoa yetu kupata huduma na malezi ya Serikali Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo katika ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio mhimili mkuu wa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika mchango wangu huu ninaziomba Halmashauri zetu zote hapa nchini kuwafanyia haki vijana wanajulikana kama wachinga ambao wanajishughulisha na shughuli zao mbalimbali za Biashara, mama ntilie na Wananchi wote kwa ujumla. Vitendo vinavyojitokeza vya baadhi ya askari wa Jiji/Halmashauri vinawasumbua sana Wananchi hawa jambo ambalo pia linatoa sura ya udhalilishaji kwa umma. Pia baadhi ya askari hawa wanasababisha kuwepo shaka ya kubambikiziwa kesi mbalimbali zisizokuwa na msingi na kusababisha kuwepo na mahabusu wengi katika magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile ninaomba Wizara hii kuzisimamia vizuri Halmashauri hasa katika masuala ya kudhibiti upotevu wa fedha za umma katika Halmashauri hizo. Vile vile Halmashauri zinazolipa mishahara ya waalimu na watendaji wengine wawelipe mishahara yao kwa mujibu wa taratibu zilivyowekwa bila ya kuwacheleweshа.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba Mikoa yetu na Wilaya zetu zilizopakana na nchi jirani, wajenge uhusiano mzuri na nchi hizo ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza kati ya nchi yetu na nchi hizo jirani.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilichangie nitanukuu taarifa ya Kamati ya kudurufu sera ya madini kama tulivyopewa hapa Bungeni katika semina iliyofanyika tarehe 27/4/2005, tumeelezwa kuwa fidia kwa wananchi wanaohamishwa kupisha migodi ni ndogo. Naiomba Serikali iangalie fidia hii na kulipa vizuri wananchi hawa ili kuwaondolea umaskini wao. Pia katika taarifa hiyo kuwa mikataba ya madini imeweka *USD 200,000* kwa mwaka kama kiwango cha juu cha kodi kinachoweza kutozwa na Halmashauri. Lakini masharti yaliyomo katika mikataba hiyo, hayaruhusu utozaji wa kodi hizo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25/5/2005 hadi 26/5/2005, Kamati yako ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, ilitembelea Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imeshatembelea karibu mipaka yote ya nchi yetu isipokuwa mpaka wa Ruvuma. Kwa kweli tumeona juhudi kubwa za Serikali yetu zilizofanya ndani ya nchi yetu hii ya Tanzania. Tulikwenda kuutembelea mpaka wetu wa Tanzania na Msumbuji.

Mheshimiwa Spika, hali ya mpaka wetu huu uko shwari sana, na kwa kweli tunastahili kuwapongeza sana wananchi wa Mtwara na ndugu zetu wa Msumbiji kwa uhusiano huu mzuri walioujenga kwa faida ya nchi zetu na wananchi wa nchi hizi zote mbili yaani Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara zetu za ulinzi ni mbaya sana. Barabara hizi za ulinzi ni vyema zikahudumiwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeweka madaraka Mikoani ni vizuri Serikali yetu ya Tanzania kufanya mazungumzo na ndugu zetu wa Msumbiji kuangalia uwezekano wa kuwaondolea matatizo wananchi wa Mtwara na wa Msumbiji kwa kuwapatia huduma za *visa* katika maeneo haya kwa hivi sasa kama unataka kwenda Msumbiji unalazimika kufuata *visa* Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia katika mchango wangu huu wa maandishi ni kama katika ziara yetu hii ya Mtwara, tulielezwa kuwa Huduma za Afya zinaridhisha lakini katika Mkoa huu kuna matatizo ya madaktari.

Mheshimiwa Spika, hawana Daktari Bingwa hata mmoja. Naiomba Serikali kupeleka Daktari Bingwa katika Mkoa huu na Mikoa mingine ambayo haina madaktari ili kuwapatia huduma muhimu nay a lazima kwa maisha na maendeleo ya watu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulieleza ni juu ya mipaka yetu katika makambi yetu ya majeshi nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la kambi ya Jeshi ya *umoja camp* iliyopo Mtwara, eneo lake kubwa limeingia katika eneo la Bahari. Wizara ilituma wataalamu kwenda kupima. Wanaomba kuwa ile ramani ipitiwe tena upya.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, narudia kuunga mkono hotuba hii na kuitakia mafanikio katika utekelezaji wake. Ahsante na naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara kwa kutayarisha hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo juu ya mgawanyo wa fedha za maendeleo juu ya mgawanyo wa fedha za maendeleo kati ya Ofisi za Mikoa, Halmashauri za Miji na Halmashauri za Wilaya. Vigezo gani Wizara inatumia kwa kugawa fedha hizo. Katika mgao wa mwaka huu fedha nyinyi zimepangwa kwa ajili ya Ofisi za Mikoa badala ya Halmashauri za Miji na Wilaya zenye kazi nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano fedha za maendeleo kwa mwaka 2005/2006 mgawanyo ujao kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi za Mikoa zimetengewa ... ... ... Shs. 45,907,578,900/=;
(b) Halmashauri za Miji ... ... ... ... .. Shs. 885,203,600/=;
(c) Halmashauri zote za Wilaya ... ... ... Shs. 4,796,123,200/=;
(d) Jumla ya fedha za maendeleo ni ... ... Shs. 51,588,905,700/=;

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha za maendeleo wa namna hii si mzuri. Ni vema fedha nyingi za maendeleo zingegaiwa Halmashauri za Miji na Wilaya badala ya Ofisi za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii ya mgawanyo wa fedha za maendeleo tunaomba maelezo kwa nini iko hivi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma hauna Hospitali ya Rufaa na Mkoa uko mbali sana na Hospitali za Rufaa Mbeya au Muhimbili, Dar es Salaam. Katika hali hii tunaomba sana Hospitali ya Mkoa ikapanuliwa na kuwezeshwa ili ikapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, la tatu katika jedwali la mgawanyo wa walimu, wanafunzi wapya waliomaliza na kupangwa katika vituo mbalimbali mwaka huu walikuwa 11,351

na walioripoti ni walimu 10,478 na wasioripoti ni walimu 871 na kwa Wilaya ya Mbinga walipangwa walimu 109 lakini walioripoti ni walimu 77 tu na walimu 32 hawajaripoti.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba barabara zifuatazo zingefikiriwa kufanyiwa matengenezo kwa kuwa ni muhimu sana kwa maendeleo ya Wananchi Jimboni mwangu:-

(a) Barabara ya Mbinga – Mpepai – Liparamba hadi Mitomoni;
(b) Barabara ya Mpepo hadi Darpori;
(c) Barabara ya Matuta hadi Mango; na
(d) Barabara ya mwisho ni Mikaranga hadi Lundo.

Mheshimiwa Spika, hayo yote niliyoyafikisha kwake Mheshimiwa Waziri kupitia kwako naomba sana yakafanyiwa kazi ipasavyo.

Naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri mia kwa mia.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii muhimu sana hoja ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono kwa sababu zifuatazo; kwanza imebaini waziwazi mafanikio kwa mujibu wa mapitio ya makadirio ya 2004/2005. Pia imebaini matatizo yaliyokabili makadirio ya 2004/2005 waziwazi. Aidha Waziri ametaja malengo ya utekelezaji kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, mimi nachangia jambo moja nalo ni kuhusu Daraja muhimu sana liliopo katika Mto Bubu, Kondoa, TAMISEMI wanalijua sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichambue kwa ufupi hoja zangu nikianza na daraja la Munguri, Kondoa.

Barabara hii ambayo daraja hili limo ni ya Halmashauri chini ya TAMISEMI.yaani fedha zake hupangwa na kutumwa na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Daraja hilo ni la muhimu kwa sababu ni kiungo pekee kati ya Kondoa mjini na Tarafa za Kwamtoro na Farkwa, Kondoa na Katesh (Hanang), Kondoa na Kata za Changaa, Thawi, Kikilo, Bereko hadi Babati mpaka Arusha. Ni ya kiuchumi, kiusafiri na usafirishaji mazao. Gharama yake ni shilingi 313,000,000/=, kilicholipwa kwa mkandarasi ni milioni 176.0, mkandarasi ni *WESONS,* kiasi bado (deni) *WESONS*/washauri ni milioni 130.0 na daraja limekamilika kwa 98% na magari yalianza kupita (majaribio).

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mkandarasi amelishikilia haruhusu magari mpaka deni lilipwe ni shilingi milioni 130. Naishukuru TAMISEMI kwa ushirikiano, lakini bado tunahitaji msaada wao. Halmashauri sasa haina fedha hizo milioni 130.0, wananchi wadau wa mradi huu wamenituma kuniambia Serikali yao Tukufu yafuatayo:-

Kwanza, wanaishukuru Serikali kwa ushirikiano Hazina, TAMISEMI wameshiriki.

Pili, Serikali imeombwa itoe fedha hizo kuwezesha mkandarasi alipwe zote, na Halmashauri iwe inakatwa kwa kufidia deni hilo hatua kwa hatua. Ndiyo namna pekee ya kuwasaidia wanyonge ho ama vinginevyo tuhurumiwe bure.

Tatu wananchi wa mji wa Kondoa waliowengi takribani 98% hutumia kivuko hicho kwa shughuli za kilimo, biashara, matibabu, cho cha maendeleo ya wananchi Munguri, kwenda Hanang, Waziri Mkuu, Usafiri na usafirishaji, kwenda mpaka Singida, kwenda mpaka Arusha shughuli za ufugaji.

Mheshimiwa Spika, pia vijiji vifuatavyo vinatumia daraja hilo kufikia mjini kushughulikia matibabu ambavyo ni Senya, Mongoloma, Changaa, Chololo, Isari, Hondomairo, Kuramafundi, Mwembeni, Thawi Juu na Thawi.

Naomba Waziri wa nchi TAMISEMI na Waziri Fedha tuwasaidie wananchi hao kupata daraja hilo.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, napendekeza ufanywe utaratibu wa kupima vijiji na kuwapa wananchi hati za kumiliki ardhi vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wizara itoe fedha za kujenga nyumba za Walimu wa Sekondari Singida ili kuvuta Walimu hawa kukaa vijijini. Shule za binafsi za Sekondari, chini ya utaratibu wa ruzuku kwa shule za msingi na sekondari zisaidie kuongeza uwezo wa miundombinu na kuajiri Walimu hasa vijijini. Naunga mkono hoja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kusema kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa hoja zangu kidogo kuhusu suala hili la mgawanyo wa Kata.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilolo ni Wilaya mpya, hivyo moja ya sababu kubwa ya kuligawa eneo hili kuwa Wilaya, kuna vigezo ambavyo vilizingatiwa moja ni kusogeza huduma muhimu kwa wananchi kupunguza ukubwa wa utawala. Hivyo Wilaya yetu iliomba nyongeza ya Kata/Vijiji/ Tarafa, lakini hatukupewa hata Kata moja.

Mheshimiwa Spika, vigezo vyote kuhusu sifa ya kugawanya Kata vililetwa na kizuri zaidi Kata mfano Kata ya Kimala iliyo katika Tarafa ya Kilolo ambayo ilishawahi kuwa Kata na ikapewa hata Afisa Mtendaji na Chama cha Mapinduzi ikawapa Kata kichama lakini Serikali ikasitisha. La kushangaza Kata hiyo imeshindwa kupewa heshima hiyo.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa chama na Serikali walishatoa ahadi ya kupata Kata hiyo. Kilichotokea sasa Kata hiyo wapinzani wameamua kutumia hoja hiyo kama bunduki. Namwomba sana Mheshimiwa atusaidie tupate Kata hiyo ya Kimala.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Kilolo kuwaombea Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi na Mheshimiwa Mizengo Pinda, waweza kushinda tena kwenye uchaguzi ujao.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Waziri naanza kwa kukupongeza wewe, Naibu Waziri wako na Katibu Mkuu kwa hotuba yenu nzuri lakini hasa hasa kwa jinsi mnavyotusaidia sana katika kutatua matatizo ya kiutawala ya Wilaya yetu wa Urambo. Kwa sasa Urambo inaonekana imetulia na ina dira. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwa asilimia 100%.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nielekeze hoja yangu kwenye kilio chetu cha muda mrefu sisi wananchi wa kijiji cha Kaliua. Kaliua hivi sasa ina wakazi wasiopungua 10,000, Kaliua ina kituo cha afya kikubwa cha *RC*, ina shule za msingi tano, mbili zikiwa na watoto zaidi ya 1,000. Kaliua ina njia za reli na barabara ya kuaminika na pia ina mtandao wa simu. Ombi letu sisi wananchi wa kijiji hiki tunaomba uwe Mji Mdogo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunisikiliza na narudia kuunga mkono hoja kwa asilimia zote kabisa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, posho za Madiwani wanazopata ni kidogo ukilinganisha na hadhi yao na mazingira wanayofanyia kazi, ukizingatia kuwa ili tupate Madiwani wenye uwezo wa kushauri, kusimamia na kukosoa lazima wawe wasomi, hivyo basi tunashindwa kupata Madiwani wenye sifa nzuri kwa sababu ya posho, zinakuwa ndogo ukianzia posho za vikao, posho za mwezi na mafao yao ya mwisho mara baada ya kumaliza Udiwani. Naishauri Serikali itazame upya posho hizi kwa lengo la kuboresha maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kutoa pikipiki nchi nzima kwa maafisa wa Tarafa jambo ambalo limewapa ari mpya, nguvu mpya na kazi mpya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ianze kuwakata maafisa wa Tarafa fedha kwa ajili ya mikopo ya pikipiki hizo ili ziwe zao na waweze kuzitunza vizuri zaidi kama mali yao.

Vile vile maafisa hawa wa Tarafa wanatakiwa kupewa mafuta wanapokuwa kwenye shughuli za miradi au shughuli za maendeleo tofauti na ilivyo sasa kwani wamekuwa omba omba.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kusimamia ipasavyo Halmashauri zetu nchini kwani idadi ya Halmashauri zenye hati safi zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka. Hivyo nazipongeza Halmashauri zote zilizopata hati safi kwani zimeonyesha nidhamu ya hali ya juu katika matumizi ya fedha za umma. Mfano, Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru viongozi wa chama na Serikali wa Mkoa wa Singida bila kuwasahau Katibu Tawala Mkoa, Wakuu wa Wilaya zote, Wakurugenzi wa Halmashauri zote, Watendaji, wapiga kura wangu na wananchi kwa ujumla kwa jinsi walivyonipa ushirikiano katika kutekeleza ilani ya uchaguzi kwa kipindi changu chote cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi na Naibu wake, Mheshimiwa Mizengo Pinda, wakishirikiana na Katibu Mkuu mwenye uzoefu na mchapa kazi ndugu Mmari.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri na maombi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Wakurugenzi na Watendaji wa Halmashauri mpya kama vile Kilindi wasiwe wapya katika nafasi zao. Wawe na uzoefu mkubwa na ikibidi wawe wamewahi kuanzisha Wilaya mpya sehemu nyingine. Sababu za hoja hii ni za wazi kiasi kuwa haihitaji maelezo wala ufafanuzi.

Pili, *GN* zinazoanzisha Wilaya mpya ni budi zitoke mapema kutamka mipaka ili utawala mpya wa Halmashauri ufahamu maeneo yake. Kwa mfano, kukosekana kwa *GN* ya Wilaya mpya ya Kilindi kumemkwaza Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Handeni kushindwa kuandaa utaratibu wa kuanzisha Mahakama ya Wilaya kwa Wilaya mpya ya Kilindi. Kwa vyovyote vile, tangazo la mipaka ya Wilaya mpya ni zoezi muhimu katika kupanga maendeleo ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ombi muhimu kuhusiana na Wilaya mpya ni kuwa Wilaya hizi zingenufaika sana kama Serikali ingezipa *unconditional grant* kwa kipindi cha miaka ya mwanzo ili zijenge misingi imara ya uendeshaji na utendaji hata kama Wilaya mama zitakuwa na hatia zisizo safi. Bila ya msaada huu, Halmashauri zinazoanzishwa zinaweza kuchukuwa muda mrefu kusimami kwa miguu yao.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine ni la vifaa/mitambo ya ujenzi wa barabara. Wilaya mpya ya Kilindi ina upungufu mkubwa wa mtandao wa kuchongea barabara na tipa angalau moja. Fedha za barabara kwa ajili ya Halmashauri ni ndogo na makandarasi hukaa mijini na kwamba gharama za ku-*mobilize* mitambo kufika kwenye maeneo ya miradi huchukua *tender* hizo au hufanya kazi kwa kiwango hafifu kutokana na fedha chache zinabaki. Tunaomba *Force Account* itumike katika mazingira kama haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba nizidi kuishukuru Serikali kuifanya Kilindi kuwa Wilaya na sasa kuipatia Halmashauri. Aidha, nitoe shukrani pia kwa Serikali kumteua Mheshimiwa F.W. Ligubi kuwa Mkuu wa Wilaya mwanzilishi ambaye ni mzoefu katika kuanzisha Wilaya mpya na jasiri katika kupambana na mazingira magumu kijografia kama Kilindi. Aidha, yeye ni mpenda maendeleo na rafiki wa wachapakazi wote na muwazi na mkweli katika kutetea wananchi wanyonge ambao ni rahisi kunyanyasika.

Mheshimiwa Spika, maombi ya wananchi wa Kilindi ni kwa Serikali kumwacha asaidiane nao kufyeka pori la maendeleo ya Kilindi kwa miaka kama mitano au zaidi na Wilaya itakuwa ya mfano Kikanda na hata Kitaifa. Tunaomba asihamishwe mapema maana tuna mhitaji sana kama Wilaya mpya yenye matumaini na mikakati mikubwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza TAMISEMI na naunga mkono Bajeti hii ili wapate fedha ya kutekeleza mikakati yao mizuri kwa manufaa ya Taifa letu.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalam mbalimbali kwa kazi nzuri wanayofanya.

Pili napenda kumpongeza kwa kazi nzuri ya kufanya maboresho kwa wataalam wake wote kuanzia ngazi ya Kitongoji hadi Wilaya kwenye Halmashauri zetu. Pamoja na kupongeza hapa nashauri maboresho yafanyike kwa wataalam wote wakiwemo na wa Serikali Kuu wanaofanya kazi katika Wilaya na mikoa yetu wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Haitoshi kuboresha watendaji wa TAMISEMI na mkalimani tu ukawaacha kwa mfano idara ya ukaguzi wa shule katika Wilaya.

Tatu, naipongeza Wizara kwa kuwalipa watendaji wa vijiji wanaodai malimbikizo ya mishahara yao. Ombi maalum Halmashauri ya Mji wa Korogwe ni mpya, hakuna hata mmoja alikwishalipwa. Hivi ni kwa nini? Naomba walipwe sasa.

Nne, napongeza Wizara kwa kuipandisha hadhi Manispaa ya Tanga kuwa Halmashauri ya Jiji la Tanga na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Korogwe kuwa Halmashauri wa Mji wa Korogwe.

Mheshimiwa Spika, ombi na ushauri, naomba sana tatizo sugu lililopo Korogwe toka mwaka jana sasa lipatiwe ufumbuzi, Mji wa Korogwe unapata fedha zake za maendeleo ya miradi mbalimbali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe matokeo yake fedha hizo hawazipati, zinatumiwa na Halmashauri ya Wilaya. Hali hii imeleta mgogoro usio wa lazima kwa Halmashauri hizi mbili. Sasa naomba sana Halimashauri ya Mji wapatiwe fedha zao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba sana na ushauri sana Halmashauri ya Mji wa Korogwe ipatiwe sasa wataalam wake na miundombinu yote inayostahili kupata hadhi ya

Mji vikiwemo ofisi, wataalam wa idara zote hata ikiwa kwa awamu, magari ya taka, magari ya maji machafu na kadhalika.

Naomba sasa Halmashauri ya Mji wa Korogwe itengewe fedha zake za barabara kutokana na mfuko wa *Road Tall* wa TAMISEMI ili kuboresha barabara na mifereji mibovu ya Mji wa Korogwe na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya ya Magunga, hospitali hii inahudumia wagonjwa wengi wa majeruhi. *Data* nilizo nazo ni kwamba kila mwaka zinatokea ajali zaidi ya 100, ambapo wagonjwa wanalinda miwa katika hospitali hiyo. Naomba kusisitiza hospitali hiyo ipewe kipaumbele kama ilivyo ya Hospitali ya Tumbi, Kibaha ili kuokoa maisha ya Watanzania na ni muhimu ujenzi wa nyumba ya maiti ya kisasa ikajengwa.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa Majimbo, naomba Wizara ifikirie kuligawa Jimbo la Korogwe Vijijini kuwa Majimbo mawili kwani ni kubwa kiasi cha kwamba ndiyo Wilaya ya Korogwe yote. Jimbo la Korogwe Mjini ni eneo dogo sana kiasi ambacho hata ilivyokuwa Tarafa ya Korogwe imegawanyika mara mbili ndio Jimbo la Korogwe Mjini kwa mantiki hiyo vigezo vilivyotumika kugawa Majimbo ya Korogwe Magharibi na Korogwe Mashariki zipo pale pale. Suala hili ni nyeti sana, naomba lipewe uzito wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, elimu, mpango wa MMES upo utata kati ya ofisi ya Mkurugenzi, wananchi, mahali shule inapojengwa kwa kutokuelewa ni nani anasimamia fedha hizi ili kufanikisha ujenzi wa shule hizi. Mpango wa MMEM ndio utumike, mpango wa MMES hauna uwazi. Halmashauri, Ukaguzi Elimu Wilaya, Diwani, Kamati ya Ulinzi, Mwalimu Mkuu ndio wanafahamu maendeleo ya ujenzi wa shule za sekondari.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maombi ya muda mrefu ya kuomba Wilaya ya Kilosa kutokana na ukubwa wake. Kutoka na hotuba ya Waziri hakuna kugawanyika, kuwa na Wilaya mbili, mbili, kwa niaba ya Wilaya ya Kilosa naomba nipate majibu ya kugawa Kilosa atakapokuwa anajibu hoja Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naomba ugawaji wa Kata tulizoomba kuzigawa kama vile Kata ya Kidodi kuwaganyika kupata Kata mpya ya Ruaha, Kata ya Ulaya kupata mpya Mhenda. Katika kata ya Mabwerebwere na ombi kuomba tupate Kata mpya ya Tindiga maombi yameletwa muda mrefu, naomba kupata majibu.

Mheshimiwa Spika, nimeomba muda mrefu soko la Ruaha lipate fedha kupitia hotuba hii ya Bajeti, soko la Ruaha limepitiwa na kufanya makisio na shilingi 30,000,000/= kwa ujenzi soko la Ruaha. Naomba nipatiwe fedha hiyo kuondoa kero kwa wananchi wa Ruaha.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo la mhandisi wa barabara na ujenzi. Mhandishi wa ujenzi anahitaji apate msaidizi kwani hata sasa kuna daraja la Nyameni

ambalo hata Wizara imeona, lakini hakuna taarifa iliyoandikwa na mhandisi huyo. Ahsante.

**MHE. *MAJOR* JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza sana Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa hotuba yake nzuri mno ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa 2005/2006 pamoja na wataalam wake. Tawala za Mikoa zina Magavana wafuatao, Mwenyekiti wa Kitongoji ni Gavana, Mwenyekiti wa Kijiji ni Gavana, Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa Mtendaji wa Tarafa, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa ni Gavana. Mkubwa wa Magavana hawa ni Rais. Kuanzia Mwenyekiti wa Kitongoji hadi Rais kila mmoja wao ana kadi ya Chama cha kisiasa anachokipenda na haruhusiwi kuongoza watu wake kwa kujikweza kuwa anawaongoza watu hao kwa itikadi ya chama chake kwani kwa kufanya hivyo atawafarakanisha wananchi wake. Ni kama kuongoza watu na kujidai unaongoza kwa nguvu za Ukristo au Uislamu.

Tawala za Mikoa zimeingiwa na dosari kubwa pale Rais Benjamin Mkapa ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu alipochangisha shilingi milioni 160 eti kunyonga Upinzani Kilimanjaro. Kumbe ni Amiri Jeshi Mkuu wa CCM na si Amiri Jeshi Mkuu wa *Democratic Republic of Tanzania.* Saa yake ya *Rado* imekwenda, mkufu wa mkewe wa dhahabu umekwenda, Vunjo, Hai, Moshi Vijijini na Moshi Mjini kwa uchaguzi Mkuu tarehe 30 Oktoba 2005 ushindi ni wa Upinzani uliowatumikia wananchi wake kwa kufa na kupona tangu mwaka 2000 hadi 2005 kwa mafanikio makubwa. Mheshimiwa Mkapa mwaka 2000 alichangisha shilingi milioni 45 na kumpa ndugu Felix Mosha kugombea Jimbo la Vunjo kwa tiketi ya CCM na wana Vunjo wakala fedha zile na ushindi hakupata.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu Rais ameongeza dau ya kufikia milioni 160 na zote zitaliwa na Mheshimiwa *Major* J. J. Makundi, atashinda tena ili aendelee kuhudumia wana wa Vunjo. Jambo hili lizidi kumdhalilisha Mheshimiwa Amiri Jeshi Mkuu mbele ya wananchi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kitendo cha mgombea Urais kwa tiketi ya CCM Luteni Kanali Jakaya Mrisho Kikwete kunadi kipande cha madini ya *Tanzanite* na kunuliwa kwa shilingi milioni 8 imeonyesha jinsi Rais huyu mtarajiwa alivyoficha *Tanzanite* nyingi nyumbani kwake na akiwa Rais atazidi kulimbikiza *Tanzanite* hivyo kukosesha TAMISEMI fedha za kuhudumia wananchi wake. Si busara.

Kitendo cha Waziri Mkuu kuwaambia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuwa wao ni viongozi wa kisiasa *(political leaders)* ni udhalimu mkubwa katika nchi hii ya mfumo wa siasa ya vyama vingi. *RC* na *DC* wana rungu la dola la Ugavana wakipewa tena rungu la CCM itajenga hofu kuu kwa vyama vya upinzani ambao ni *side mirror* ya Serikali. Hivi sasa maendeleo ya TAMISEMI yamethia sana. ni hofu tupu.

Mheshimiwa Spika, naamini Bajeti hii nzuri mno itanufaisha kimaendeleo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na namtakia kila la kheri Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri wa TAMISEMI. Naunga mkono hoja.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya TAMISEMI kwa jinsi inavyoratibu na kuunganisha shughuli za Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya. Hata hivyo ningependa kupata majibu kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuna wale waliokuwa Makatibu Kata ambao hawakuchukuliwa na Halmashauri za Wilaya kama Maafisa Watendaji kwa kuwa baadhi hawajalipwa mafao yao, ikiwemo gharama za kusafirisha mizigo yao, akiwamo Bwana Gregory Katunzi wa Kata ya Kasuga ni lini watalipwa? Kuna kada ya *Regional Local Government Officer* kwenye Sekretarieti ya Mkoa. Kwa nini ngazi hii haiteremki hadi ngazi ya Wilaya? Nini nguvu aliyonayo juu ya Wakurugenzi ili kuhakikisha kazi zao zinaenda vizuri? Kwa nini hawana vitendea kazi ikiwemo gari ili wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Spika, inakuwaje Mkurugenzi anayevurunda kazi anabadilishwa kazi kuwa *R and GO?* Ataheshimiwa vipi hasa akipangwa katika Mkoa ule ule? Na kwa nini Wakurugenzi wasiopata hati safi za mahesabu kwa miaka mitatu mfululizo wasiwajibishwe au hata kukaripiwa au kuvuliwa madaraka? Kwa nini kusiwe na kitengo maalum cha kufanya tathimini ya kupandisha ngazi ya Miji, pia kugawa maeneo ya utawala badala ya kutegemea Mikoa au Vijiji iombe yenyewe? Kutatokea nini kama hakutakuwa na ombi toka Mkoa wakati kila hali zinaonekana Mkoa au Wilaya, unahitaji kugawanywa? Je, TAMISEMI italifumbia macho na kukaa kimya tu?

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati ikijibu swali langu kuhusu ujenzi wa Kituo cha Afya Tarafa ya Kasanda, iliahidi kuanza ujenzi huo mwaka huu yaani 2005/2006 na kwamba shilingi milioni 60 zitatengwa. Wananchi wamehamasika sana na wamekwishafanya yale yaliyoko katika uwezo wao. Je, TAMISEMI inasemaje kuhusu upatikanaji wa fedha hizo ili kazi zianze?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kupongeza kwa kazi nzito, nzuri hapo Wizarani. Naamini kazi mzifanyazo zimeweka msingi mzuri wa Serikali ijayo ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwanza Ibara ya 63 ya Hotuba ya Waziri imeelezea maombi ya kuanzishwa Vijiji/Mitaa/Kata, Wilaya na Mikoa. Ushauri wangu ni kwamba wakati tunangoja hali ya uchumi tuwe na uanzishwaji wa Miji na Miji Midogo hasa katika vituo *(centres)* ambazo wananchi wamekaa mfano Nzega, Ndala, Bukene na kadhalika ili sehemu hizo zipimwe. Vijiji vingi vinakuwa na *centres* bila mipango ya Kimji. Mipango mizuri ya Vijiji, Mji itawezesha kuwa na Miji, Manispaa zilizo na mpangilio

Ushauri wangu wa pili ni kuhakikisha watendaji wa Halmashauri wote wanabadilika kifkra *(mindset)* ili wawe watendaji wa kusukuma maendeleo. *Programme* za MMEM, MMES, MKUKUTA na MKURABITA hazitafanikiwa iwapo fikra za watendaji hazitabadilika. Naomba Ofisi yako iwapime Watumishi hawa kwa kigezo cha kumbadili mwananchi kwa kumletea maendeleo. Pia nashauri fedha za MMES zipitie kwenye Halmashauri badala ya mtindo wa sasa wa kupeleka hazina ndogo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itizame kwa macho ya huruma Mikoa ya Kanda ya Magharibi mfano Rukwa, Kigoma, Tabora, Singida na Shinyanga ambayo haipati fedha nyingi za nje. Nashauri ili kuibua uchumi ulioko katika maeneo hayo mfano madini, mazao ya kilimo biashara/chakula, mifugo, utalii na biashara kwa nchi zinazopakana Zambia/Zaire/Rwanda na Burundi kwa kuwa na barabara za uhakika umeme na mawasiliano. Ninawatakia kazi njema.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: **Ninachotaka kusema ni kwamba utaratibu gani umewekwa wa kuangalia watoto wenye vipaji vyanamna hii ili kuweza kuwaendeleza? Kwa sababu ni vipaji ambavyo vinahitaji kuendelezwa! Nimesema hili, sijui kama nitapata nafasi ya kuzungumza kwenye Wizara ya Elimu kwamba liangaliwe, hawa watoto waendelezwe kutumia vipaji vyao, lakini pia watumike kuelimisha watoto wenzao wenyewe wanafanyaje ili kuweza kufikia hatua hiyo waliyofikia.**

**Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nirudie kusema kwamba ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Cheyo amesema kwamba debe shinda halitikisiki. Nimesema CCM ni debe shinda halitikisiki ila debe tupu lenyewe linavuma tu linayumbayumba. Kwa hiyo, nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri waliyoifanya na naunga mkono hii bajeti kwa asilimia mia moja.** ***(Makofi)***

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawatakia mafanikio katika hotuba yenu.

Pili, wananchi na viongozi wa Nachingwea wamefanya kazi kubwa sana ya kujenga jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri Kuu ya Wilaya. Wanastahili kupongezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri awapongeze wananchi wangu kwa kuchangia zaidi ya shilingi milioni 500 kupitia mazao na wafanyabiashara. Likitoka tamko Bungeni la kuwapongeza wananchi hao na viongozi wao, itatutia moyo sana.

Mheshimiwa Spika, jengo ni zuri lakini bado kuna kasoro. Tangu jengo lianze, mahesabu hayajakaguliwa. Hata Tume aliyoiunda *RC* wa Lindi, Mheshimiwa Nicodemus Banduka imeshauri mahesabu yakaguliwe. Nimeshangazwa na barua ya *RC* aliyokuletea hivi karibuni akisema Tume haikubaini wizi! Kama Mbunge sijawahi kudai kuna wizi. Nimedai na ninadai maelezo ya kina pakiwa na *audited report*. Huyu mwizi anayesema hayupo, utampataje mwizi kama unamtafuta mwizi bila ku-*audit* vitabu?

Mheshimiwa Spika, kwenye barua ya *RC* amedai jengo ni zuri sana. Nakubaliana naye 100% lakini sielewi kwa nini *RC* hata baada ya kushauriwa na Tume yake hakukueleza kuwa ataagiza matumizi ya jengo yakaguliwe na *independent auditors*. Siyo suala la ngedere kwa ngedere.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote waliojiandikisha kuchangia hoja hii wamepata nafasi. Kwa hiyo tumefikia mwisho wa mjadala wa jumla mtakapo rejea kipindi cha mchana watoa hoja wataanza kuhitimisha hoja yao na kukamilisha shughuli za hoja hii. Lakini hoja inayofuata hata kama wakimaliza mapema hoja inayofuata itatolewa kesho asubuhi kwa mujibu wa ratiba kama ilivyo. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 6.44 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma S. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba nianze kwanza kwa kutangulia kuungana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa pongezi alizozitoa kwa Viongozi mbalimbali ambao wametusaidia sana katika uendeshaji wa shughuli za Serikali yetu pamoja na wale ambao wako katika kinyang'anyiro cha Ugombea nafasi mbalimbali za Kitaifa.

Lakini naomba vilevile niungane naye kwa rambirambi mbalimbali alizozitoa, hususani kwa ajili ya Wabunge ambao wametutangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, naomba basi niseme kwa kifupi kwamba kwa kuwa inawezekana Bunge hili kwa wengi wetu hatujui mambo yatakuwaje, basi niseme machache kuhusiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa mantiki hiyo, naomba kwanza nimshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi kwa Uongozi wake madhubuti sana. Nimejifunza mengi kutoka kwake na kwa kweli naondoka namaliza Bunge hili na fahari kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaomba vilevile, nimshukuru sana Katibu Mkuu pamoja na wasaidizi wake wote, kwa kweli tumefanya kazi kwa ushirikiano mzuri sana na wametusaidia sana katika kutushauri inavyotakiwa. Ninawashukuru sana Kaka zangu Waheshimiwa Mawaziri pamoja na wenzangu Manaibu Mawaziri ambao kuwepo kwao kwa mchanganyiko niliouona katika kipindi hiki, tumejifunza mambo mengi sana kutoka kwao.

Ninaomba niwashukuru Viongozi wangu wote wa Mkoa wa Rukwa Wilaya ya Mpanda kwa ushirikiano mzuri sana ambao tumeutekeleza kwa pamoja katika kipindi hiki cha miaka kama minne au mitano na ninadhani ndiyo maana baadhi ya Waheshimwa Wabunge wanauliza siku hizi Mpanda kulikoni na Mkoa wa Rukwa kulikoni? Kwa sababu pametulia ukilinganisha na miaka ya nyuma. Kwa kweli hali ni nzuri zaidi. *(Makofi)*

Ninaomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Kaka na Dada zangu kwa msaada mkubwa sana mlioutoa kwangu hasa kwa sababu Wizara hii ni kubwa. Lakini kwa kupitia maneno yenu mazuri, nimejitahidi kufanya yale mliyoweza kuona yanafaa. Mimi nawashukuru sana kwa yote haya ambayo yamejitokeza. *(Makofi)*

Mwisho, nataka niwashukuru Wapigakura wangu, wamenivumilia sana katika kumsaidia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, nimetumia muda mwingi pengine kuzunguka Wilayani na Mikoani, lakini walistahili na walinivumilia sana. Lakini kubwa, nawashukuru sana kwa kuwa katika kinyang'anyiro hiki wameamua kunichangia karibuni Sh.500,000/= kwa ajili ya kuchukua fomu ya Ubunge. Kwa kweli nawashukuru sana wote kwa ujumla wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijaribu kutoa mchango wangu katika baadhi ya maeneo. Tuna hoja karibu 85, nina hakika hatuwezi kuzimaliza zote kwa sababu ni nyingi sana. Lakini kwa yale ambayo tutashindwa kuyatekeleza kwa maana ya kujibu hoja, ninaomba Waheshimiwa Wabunge mlichukulie kutoka Ofisi yetu kwamba tutajitahidi kabisa kuyajibu kwa maandishi kama ambavyo tumekuwa tukifanya.

Naomba nianze na masuala ambayo yamezungumzwa kwa ujumla wake ambayo Mheshimiwa Lubeleje pamoja na Profesa Mbawala na Mheshimiwa Janguo na hata Mzee Halinga wamelizungumza sana hilo la Mfuko wa Pembejeo. Lakini kwa uzito wake, nadhani Mheshimiwa Waziri ataweza kuliweka vizuri zaidi ili muweze pengine kuona mtazamo wetu ni nini juu ya jambo hili. Vinginevyo, naomba niseme kwamba kwa haya masuala ya Wakuu wa Wilaya ni kweli kwamba baadhi ya Wabunge wametusaidia kuli-*clarify* hapa vizuri sana, lakini nadhani Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kuliweka vizuri zaidi pengine kusaidia hasa wenzetu wa upande wa Upinzani na baadhi pengine ambao bado tuna mawazo tofauti kidogo juu ya majukumu ya Mkuu wa Mkoa na Jukumu la Mkuu wa Wilaya. Ni eneo moja kubwa na ninafikiri ni vizuri likaeleweka vizuri. Vilevile, nilitaka nisema kidogo tu kuhusiana na baadhi ya mambo ambayo nina uhakika Mheshimiwa Waziri hatayasema kwa sababu nadhani yako kwenye uwezo wangu, ni haya yafuatayo kuhusiana na yale ambayo Mheshimiwa Grace Kiwelu alikuwa ameyasema.

Kwa ujumla tunasema, kuhusu Mkakati wa Maendeleo Vijijini tuna kubaliana naye kabisa kwamba tunahitaji kutoa elimu zaidi na juhudi zinafanywa kwa kweli kujaribu kutafsiri makabrasha mbalimbali ili yaweze kuwa katika lugha ya Kiswahili na kwa maana hiyo iweze kusaidia zaidi jamii katika kuelewa jambo hili . Kwa maana ya Mfumo wa Fursa Sawa na Vikwazo kwa Maendeleo, haujawanufaisha wananchi walio wengi ni kwa sababu vilevile bado zoezi hili linaendelea. Tumefanya Wilaya 60 tu, kwa hiyo bado tuna kazi kubwa ya kueneza jambo hili katika Wilaya nyingine nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Grace alitaka vilevile Serikali itoe ratiba iliyo wazi kwa maboresho na sisi tunasema, ni kweli kabisa jambo hilo ni la msingi kabisa lakini kama tulivyosema, tulianza na Halmashauri 38 na tunaendelea sasa kueneza

katika Halmashauri nyingine zote ili jambo hili liweze kuenea kwa urahisi zaidi ndani ya mwaka mmoja au miaka miwili ijayo, tuna hakika tutakuwa tumefika mahali pazuri sana.

Kuhusu Mfuko wa Wanawake na Vijana, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Kiwelu kwamba mafunzo kwa maana ya mikopo inayotolewa hivi sasa, kwa kweli yameshaanza kutolewa na yanatolewa chini ya utaratibu wa Afisa Maendeleo ya Jamii. Kabla hujaingizwa katika utaratibu, lazima upite kwenye mafunzo ya wiki moja hivi kukusaidia tu uweze kuona nini kinahitajika, lakini najua inawezekana jambo hili halijaenea kila mahali. Kwa hiyo, bado tunaendelea kulisukuma ili liweze kufika kila sehemu ili kuwezesha mikopo kuchukuliwa zaidi. Kwa maana hiyo hiyo, tutaendelea kwa kweli kama tulivyokwishasema katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwamba ni vizuri kwa kadri tutakavyoweza utaratibu utarekebishwa kidogo ili fedha ziweze kulipwa baada ya kukopwa na tunadhani Mawakala, hasa *Community Banks* au Benki za Wananchi pamoja na *SACCOS* au vikundi vya kijamii ambavyo tunadhani vinaaminika, pengine tunaweza tukasaidiana vizuri zaidi kuliko pengine utaratibu wa sasa ulivyo.

Vilevile, nilitaka niseme kwa yale mawazo aliyoyasema kuhusiana na uwasilishaji wa pendekezo la kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Mfuko huo, yaani kwa maana ya Mfuko wa Wanawake na Vijana na vile vile kuhakikisha kwamba Wabunge tunakuwa na Ofisi zenye hadhi. Yote mawili tumeyakubali na tunaendelea kuyafanyia kazi na ninataka niongeze tu kwamba kwa upande wa Ofisi za Wabunge, nadhani Waheshimiwa Wabunge mnajua hili tayari Ofisi ya Katibu wa Bunge baada ya kushauriana na Serikali wameshakubaliana kwamba wachukue jukumu la kusimamia zoezi hili ili tuweze kuliendesha vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Madiwani kwa ujumla wake, naweza nikasema tu kwamba jambo hili wote tunalijua tumekuwa tunalizungumza sana hapa Bungeni na mimi nina uhakika Waheshimiwa Madiwani wanafarijika sana kusikia namna mnavyojaribu kuwasaidia kuwajengea hoja ambazo zinaweza kuwa ni za msingi. Naomba niseme kwamba bahati nzuri jambo hili sasa hivi liko chini ya usimamizi wa Mwenyekiti Lubeleje, Mbunge wetu ambaye ndiye anayo Kamati inayotazama jambo hili kwa upana wake. Kwa hiyo, ninauhakika jambo litakapo kamilika tutakuwa na mawazo ya kuwasilisha hapa Serikalini kwa lengo ambalo naona Wabunge mnataka tulitazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Tawala za Mikoa Na.17 ya mwaka 1997, Mheshimiwa Grace Kiwelu aliomba litazamwe tena kwa lengo la kujaribu kuona ni namna gani inaweza ikasaidia kufanya Mikoa iweze kufanya kazi vizuri zaidi. Mimi nadhani kwa hili ni jambo la busara tu na tayari tulikwishaanza kulifanyia kazi na tuna hakika mapitio yale yatazaa matunda mazuri.

Kuhusu Ofisi za Wakuu wa Wilaya na nyumba zao, ni kweli tunakiri kwamba lazima si Wakuu wa Wilaya tu, hata baadhi ya nyumba za Mikoa hali zao si nzuri sana. Lakini jambo hili kama mnavyofahamu tumekuwa tunalishughulikia kila mwaka na kwa mwaka huu wa fedha tumetenga kiasi cha Shilingi bilioni 2.2 ambazo zitaelekezwa katika kujaribu kuhakikisha kwamba marekebisho na matengenezo yanafanywa katika maeneo haya ili kuwawezesha Wakuu hawa kufanya kazi zao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko lingine zito hapa la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nafikiri nimwachie Waziri aliseme mwenyewe kwa sababu yeye ndiye mwenye dhamana kubwa zaidi. Lakini kuhusu hili la utafiti wa matukio yaliyojitokeza, tunaweza kusema tu kwamba katika hotuba tumejaribu hata kuainisha ni mapungufu gani au ni uzoefu gani tumeupata wakati tumefanya zoezi hili la uchaguzi. Kwa hiyo, tayari kwa kweli jambo hili linafanyika, lakini kwa dhamira iliyopo tutaendelea kufanya mambo haya mwaka hadi mwaka kwa sababu kazi ni kujenga demokrasia ambayo ni nzuri zaidi. Tunakubali kwamba tuliahidi tungefanya Semina kwa ajili ya *Local Government Reform Program*. Ni kweli hatujafanya, lakini maandalizi yote yameshakamilika na tumeshawasilisha mawazo yetu kwa Katibu wa Bunge ili waweze kututafutia muda muafaka kwa ajili ya kujaribu kusaidia kutoa Semina hiyo kwa kutusaidia kupata uelewa mkubwa zaidi juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la mapato ya Serikali za Mitaa na hili si Mama Kiwelu ambaye amesema, lakini vilevile Mheshimiwa Lwakatare naye vilevile ameligusia. Yako mawazo kwamba baada ya kuondoa vyanzo mbalimbali kwenye Halmashauri zetu, tumewapunguzia uwezo kabisa hata wa kuendesha shughuli zao. Sasa jambo hili nadhani linahitaji maelezo kidogo na tunachosema sisi kama TAMISEMI ni kwamba tulichokifanya tunafidia kile kiwango tu cha ushuru au kodi tuliyokuwa tumeiondoa. Kamwe hatufidii mapungufu yote katika Halmashauri zinazohusika. Sasa Halmashauri nyingine zimeamua kubweteka tu baada ya uamuzi huu na wamefanya kana kwamba zoezi hili litafidiwa kwa kila kitu kutoka Serikali Kuu, hata kidogo! Lazima waendelee kukusanya ushuru na kodi mbalimbali katika maeneo mengine yote yaliyobaki kwa asilimia kubwa kadri inavyowezekana kwa sababu pengo kubwa linaonekana linatokana na wao kutoongeza nguvu katika maeneo ambayo bado yako ndani ya uwezo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa hili tunaliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kweli Serikali imedhamiria, tulianza na Shilingi bilioni 22, tumekuja Shilingi bilioni 25, mwaka huu tumetenga Shilingi bilioni 41 na tunakwenda kwa kulingana na mahesabu ambayo tunadhani yanawiana na kile ambacho tuliahidi kwamba tutakitoa wakati tutakapokuwa tunafidia. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimwa Wabunge wote tusaidiane tuwasukumesukume wenzetu kwenye Halmashauri wasikae wakadhani kila kitu kitatoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Bahati nzuri hili na Kaka yangu Mheshimiwa Mporogomyi alilizungumza licha ya Mheshimiwa Mama Kiwelu na ninaomba niseme tu kwamba ni kweli ziko taarifa mbili ambazo zilitolewa kwa nyakati tofauti. Taarifa ya kwanza ilitolewa mwaka 2003 Mwezi Desemba na Taarifa ya pili imetolewa Oktoba, 2004 na zote mbili Allen Penny alikuwa ni mmoja kati ya watu mashuhuri waliokuwa wamekaa kutengeneza taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi ni kwamba taarifa hizi zote mbili ni mchango wa Serikali kwa kusaidiana na Wahisani hawa kutathmini zoezi hili la Mpango

wa Elimu ya Msingi ili tuweze kuona wapi kuna mapungufu na wapi tufanye nini. Kwa hiyo, sio taarifa ambayo kazi yake au mtazamo wake ni kui-*criticize* Serikali au kuikoa Serikali, hata kidogo! Hata ukisoma utaona kwa kweli kwa sehemu nyingi mambo mengi yameonekana ni mazuri na ni ya kusaidia Serikali ili iweze kufanya kazi zake vizuri.

Naomba tu nitoe mifano miwili tu ya baadhi ya maeneo ambayo wameyasemea na hili ni kuhusiana na mazingira ya Shule za Msingi kwa maana ya ujenzi wa madarasa. Katika ripoti hii ya Desemba, 2003 wataalam hawa wanasema hivi: *"School and Classroom Environment achievements, the team observed new classrooms in all of the school visited in the regions. These classrooms though following different designs, are attractive to the eye, appear reasonably well build, have reduced learner congestion and are a source of immense pride to School Committees, parents, pupils and the communities around the school."* Sasa hii ni *comment* yao hawa waliofanya hii tathmini.

Lakini niseme tu eneo lingine nalo ni *assessment,* lakini hii ni ya Oktoba, 2004. Wanasema: *"Much has been achieved over the past two and a half years, schools are much better places to visit. PEDEP has been successful in ensuring that funding has reached school level in increasing numbers of classrooms constructed textbook procured and teachers trained. It has also been instrumental in developing institution and capacities especially at the school level which are increasingly more responsive to the demands of local stakeholders, whether they supply side institution particular in Central Government are recognized in dis-sufficiently and shaping themselves to respond to these demand is a primary challenge facing PEDEP over the next years." (Makofi)*

Tunachokisema ni nini? Ni kwamba tunakubali kabisa inawezekana yapo mapungufu ya hapa na pale kwa sababu zoezi ni kubwa sana, lakini tusije tukachukua mapungufu ya eneo moja au mawili tuka-*generalize* ikaonekana kama vile mpango mzima kwa kweli hauna maana. Hapana. Mpango kwa kweli kwa sehemu kubwa ni mzuri na ndiyo maana hata wenzetu wanaona hili katika taarifa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nafikiri ni vizuri nalo tukalisema kidogo, ni hili ambalo lilitokana na Kaka yangu Mheshimiwa Kimiti. Najua Mheshimiwa Waziri ataliboresha zaidi la kupandisha hadhi baadhi ya maeneo. Mimi niseme tu kidogo hili la Manispaa ya Sumbawanga.

Waheshimiwa Wabunge, nataka niseme tu kwamba Mheshimiwa Kimiti amejitahidi sana hasa kutubana hasa kwenye suala la Halmashauri hii ya Mji wa Sumbawanga na hatimaye kwa kweli tukasema tujitahidi kufikia mahali ambapo ni muafaka na ndiyo maana tukakubali iwe Manispaa. Lakini ni kwa sababu vilivile sehemu kubwa ya vigezo katika eneo hili kwa kweli vilifikiwa, kwa hiyo hatukuona sababu ya kuendelea kubishana naye juu ya jambo hili.

Kwa masuala ya lami, ninaomba niseme hili vilevile kuhusiana na Halmashauri ya Mji wa Singida. Tunachosema, chini ya *Local Government Support Program,* fedha zimekwishaanza kupangwa kwa ajili ya kwenda katika maeneo fulani fulani na kwa Manispaa ya Sumbawanga tayari tumeshaweka kama Sh.14,500,000/= ambazo

zitatolewa. Hivyo, mfululizo kwa kipindi cha miaka kama mitano na hali kadhalika kwa Mji wetu wa Singida na hivyo hivyo itakuwa kwa Halmashauri nyingine za Miji ambazo zitajitokeza kuundwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Hospitali ya Sumbawanga kuwa na Hospitali yake ya Wilaya, kimsingi Ofisi yetu imelikubali na tutashirikiana na vyombo vinavyohusika na hasa Wizara ya Afya ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukasaidia Mji wa Sumbawanga kuwa na Hospitali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lingine ambalo limejitokeza kuhusiana na Abdulkarim cha Mafia kupitia Mheshimwa Abulkarim Shah. Naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara kwa kweli tutajitahidi, tutazungumza na Wizara ya Ujenzi kwa mara nyingine tena. Rai yako tunaielewa lakini hatuwezi kusema harakaharaka ni kitu gani tutaweza kufanya lakini ni dhahiri unahitaji kwa kweli kutazamwa kwa namna tofauti kidogo. Kwa maana hiyo, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Maria Watondoha na Mheshimiwa Zainab Gama ambao wote niliwaona wanakupigia debe kwa nguvu kweli kweli nadhani wanakupenda sana. *(Kicheko/Makofi)*

Kuhusu Soko la pale Kariakoo kwa upande wa zao la nazi, Mheshimiwa Shah nakuhakikishia tutaliwasilisha ipasavyo na tutatazama tufanye nini. Lakini nataka nikuambie tayari tumeshaanza kuweka baadhi ya miundombinu pale ambayo *specifically* ni kwa ajili ya nazi na tunatazamia vilevile kwamba katika bajeti ya mwaka 2005/2006 tumetenga kiasi fulani cha fedha karibu Shilingi milioni nane kwa ajili hiyo hiyo ili kuhakikisha kwamba zao hili linakuwa katika mazingira mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara zilizopo katika Manispaa ya Morogoro na hasa ile ambayo Mheshimiwa Mloka aliizingumza sana ya kwenda Ikulu, naomba nikuhakikishie kabisa kwamba *TANROAD* wametuthibitishia kwamba jambo hili litatazamwa kwa karibu zaidi ili tuweze kuona kwamba ile aibu inatutoka. Bahati mbaya na mimi nilishapita barabara ile unafika mahali unaona aibu kama Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Kuhusu fedha iliyotolewa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo kile cha Msamvu, naomba niseme kwamba fedha hizi lazima tuzitenganishe. Fedha zile zilikuwa ni hususan kwa ajili ya miundombinu ile ya msingi kama mifereji, barabara pale ndani na vitu vingine vinavyohusiana na namna magari yanavyoweza ku-*park* katika eneo lile. Lakini ujenzi wa vibanda kwa ajili ya kuhakikisha kwamba huduma nyingine za msingi zinakuwepo, tunaomba sana Manispaa ishirikishe Sekta Binafsi kwa sababu nao wana nafasi kubwa sana ya kuweza kuchangia katika eneo hili na tutahakikisha katika maelekezo, tutawaambia hivyo wasitegemee sana kwamba tunaweza kupatikana fedha kutoka Serikalini.

Liko suala ambalo Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alilisema na mimi naomba niseme tu kwamba hili suala sina uhakika kama ni Mheshimiwa Slaa, lakini nadhani ni mmoja kati ya Viongozi wenzetu wa Bunge hapa linalohusiana na kile kitabu cha Mkoa

wa Dar es Salaam cha bajeti juu ya *insertion* ya maneno ya Mheshimiwa Kikwete. Naomba niseme tu kwamba kwa bahati nzuri jambo hili kwenye Kamati lilielezwa na tulikubali kwamba kwa kweli sivyo, ilitakiwa iwe katika taarifa ile, lakini inaonekana aliyeandika alikuwa kidogo amekuwa *carried forward.* Nia yake ilikuwa nzuri kwamba tuandae mazingira mazuri kwa wasaidizi hawa ambao baadaye ndiyo wanakuja kumsaidia Rais Kikwete wakati wa Uongozi wake akiamini kwamba kwa vyovyote vile Rais ni Kikwete. *(Makofi)*

Sasa inawezekana hili hamkulitaka sana, badala yake nikaona kama mnataka kuonyesha kwamba Shilingi milioni 20 zile ni kwa ajili ya kwenda kumfanyia kampeni. Hata kidogo! Haikuwa dhamira ya uandishi ule na hii Shilingi milioni 20 baada ya kugawa kununua vifaa, unapeleka wapi? Kama ni kampeni za mtu mkubwa kama huyu, kwa hiyo nia hasa ilikua ni hiyo lakini bahati mbaya. Naomba niwahakikishie tu kwamba katika kitabu ambacho sisi tuli - *demand* tuletewe, jambo hili lilishafanyiwa marekebisho na hata ukikipata kile sasa hutakuta yale maneno, yamo, lakini kubwa ni yale yaliyojitokeza katika Kamati maana lile hasa ndiyo msingi ambao tunaweza tukautumia. *(Makofi)*

Kuhusu mradi huu wa *Quick Start* ambao Mheshimiwa Dr. Slaa ameuzungumzia. Naomba niseme tu kwamba yako mambo mengi chini ya mradi huu wa *Quick Start* na mimi nataka niseme tu kwamba Mheshimiwa Dr. Slaa jambo hili tumelipokea na tunaomba tukuhakikishie kwamba tutajitahidi kulifuatilia na kulitafutia ufumbuzi na wale wote ambao wataonekana dhahiri kabisa kwamba wame-*mismanage fund* kupitia *Quick Star*t tunakuhakikishia kabisa kwamba hatua zitachukuliwa kali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa vilevile na Mheshimiwa Njelu Kasaka na hata Mheshimiwa Omar Mjaka walizungumza sana juu ya Watendaji wa Vijiji na kwa maana hiyo kujua mishahara yao kwamba pengine wanaona kama inachelewa hivi. Lakini naomba nisema kwamba, tumekuwa tukilieleza jambo hili sana. Ni kwamba kwa kweli Watendaji wa Vijiji ambao tuliwaajiri mpaka hivi sasa ni wale 777,000 na hawa tulihakikisha kwamba kwa bajeti iliyokuwa imetengwa fedha zao zipo na wamekuwa wakilipwa na ndiyo maana mara ya mwisho nilisema kama kuna utata wowote, jambo hilo tutaweza kulitatua bila matatizo yoyote. Sasa wako waliobaki ambao ndiyo hao tumesema kwenye bajeti ya mwaka tumeomba karibu Shilingi bilioni 11 kwa ajili ya Watendaji wa Vijiji wachache waliobaki na Watendaji wa Mitaa ambao endapo Bunge mtapitisha, basi tuna hakika nalo hilo halitakuwa na utata mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lutavi na Mheshimiwa Chilolo na hata Mheshimiwa Lwakatare waliomba kwa kweli tuwe na utaratibu mzuri wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Kamati za Bunge ziwawezeshe kufanya kazi zao vizuri na hasa katika eneo hili la Serikali za Mitaa. Ushauri umepokelewa na tutaufanyia kazi. Nafikiri si jambo ambalo lina utata mkubwa sana, nadhani linaweza likatafutiwa ufumbuzi tuone namna ya kwenda mbele.

Mheshimiwa Major Jesse Makundi alisema kwamba Serikali angependa itoe ufafanuzi ni sheria ipi hasa ambayo imewafanya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya

waweze kuwa vilevile ni Viongozi wa kisiasa. Sasa kwa hili, naomba tu niseme kwamba, unajua wakati mwingine sheria zikipita tunasahau haraka sana, lakini sheria hizi zimepitishwa hapa hapa Bungeni. Kwanza ni Ibara ya 61 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara hii ndiyo inayoweka bayana nafasi ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya na majukumu yake katika kusaidia Uongozi wa nchi hii.

Lakini Sheria Na.3 ya mwaka 1999 ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ambayo ilipitishwa hapa Bungeni, inatamka waziwazi kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni Viongozi wa Kisiasa. Sasa huo ndiyo msingi pekee ambao tunaweza tukautumia katika jambo hili. Sasa kama yapo mapungufu ya hapa na pale ya Mkuu wa Wilaya mmoja mmoja, hilo ni jambo linaloweza kushughulikiwa kwa maana ya mtu mmoja mmoja. Lakini kwa maana ya uhalali wao kama Viongozi wa Kisiasa, sheria ipo na Katiba inawalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwanri, hili naomba niliseme tu kwa sababu nimepewa mimi, lakini nadhani Waziri atalizungumza zaidi. Ulitoa maelezo mazito hapa juu ya kuomba ikiwezekana Hai igawanywe mara mbili tuweze kuwa na Wilaya mbili na kwamba jambo hili lilitokana na ahadi ya Rais alipotembelea huko.

Mimi nasema tu kwamba, jambo hilo linafuatiliwa kwa karibu sana hivi sasa ili tuweze kuhakikisha kwamba kama ahadi hiyo ipo, basi Mheshimiwa Rais aweze kujulishwa na baadaye tujue ataamua nini juu ya jambo hili. Lakini kwa upana wake, kwa maana ya Wilaya, nadhani Waziri ataweza kusaidia vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji kupewa motisha, nia ipo kubwa tu na pengine mahali pazuri kwa kuanzia ni kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa aliyokwishaitoa kwamba asilimia ile 20 ambayo zamani ilikuwa inapatikana kutokana na vyanzo vya mapato, tuhakikishe inarejeshwa pale kwenye ngazi za Vijiji iwe ni sehemu mojawapo ya motisha kwa Wenyeviti hawa na maelekezo tayari yalikuwa yameanza kufanyiwa kazi. Ninaomba kwa hili niseme kwamba, kwa sababu ruzuku inayotolewa kwa kiasi fulani inaweza ikasaidia kuziba pengo hilo bila matatizo makubwa sana. Kwa hiyo tutajitahidi kusukuma jambo hili kwa kadri tutakavyoweza. Maombi ya kuzigawa Tarafa, Kata na Vijiji, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Mgaywa, Mheshimiwa Msafiri na Mheshimiwa Mwananzila, mmeyazungumza. Mimi naomba niseme kidogo tu jambo ambalo tumefanya juu ya jambo hili na Waziri atalifafanua vizuri zaidi.

Jambo hili tumekuwa nalo muda mrefu kidogo. Kama nilivyosema mara ya mwisho katika kutoa ufafanuzi, nilisema uchambuzi umeshafanyika juu ya jambo hili, mawasilisho ya maombi ilikuwa ni Kata mpya 225, zikachambuliwa kitaalam sana. Kata zilizokidhi matarajio zilikuwa ni 71 tu. Wengine wote kwa sababu moja au nyingine kutokuzingatia maelekezo, basi hawakuweza kufanikiwa. Sasa kwa hilo la ujumla wake, nini tunafanya juu ya jambo hili? Nadhani Waziri atasaidia kulimaliza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hati chafu ambazo zimesemekana zipo katika baadhi ya Halmashauri, tunakubali, tutaendelea kuzifanyia kazi kwa uhakika zaidi ili tuweze kuwa na vitu vizuri zaidi. Kuhusu Wahasibu na upungufu wake na wataalam wote kwa ujumla, bahati nzuri jambo hili linashughulikiwa na Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta na tunadhani tutalimaliza polepole kwa kadri uwezo wa Serikali na mafunzo yanavyotolewa.

Lipo suala la Mheshimiwa Kasaka ambalo nadhani alilizungumza kwa uchungu sana na mimi nafikiri ni vizuri tukalisema vizuri kidogo. Kuhusu mbao ambazo Mheshimiwa Mbunge anasema zimepokonywa kutoka kwa mwananchi mmoja na mimi napenda niseme kama ifuatavyo, ni kweli kabisa kwamba mbao zilikamatwa kutoka kwa Bwana Kadu na ni muda mrefu kidogo, nafikiri kwenye mwaka 2001 au mwaka 2002. Jambo hili limekwenda kupitia *process* za Mapolisi, baadaye zikaenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baadaye likarejeshwa sasa kwa maana ya utekelezaji. Mkoa ukaagiza Wilaya itekeleze jambo hili na Mkuu wa Wilaya huyu wa sasa ambaye wakati huo alikuwa ndio kwanza ameingia mwaka 2003, ndiye alianza kusukuma jambo hili kwa maana ya utekelezaji. Lakini linalojitokeza, Mkoa ulisema, *okay,* kwa sababu tumefuta kesi kwa maana ya *nolle, nolle* maana yake ni kwamba, wakati wowote unaweza kukamatwa tena tukakupeleka Mahakamani. Si kwamba ikifutwa ndio mwisho, hata kidogo! Sasa wapo watu watatu ambao wamehusika katika zoezi hili la mbao, lakini Kadu ndiye aliyekuwanazo. Watu wawili ambao ndio Mheshimiwa Mbunge alikuwa amesema mbao zile zimekamatwa pamoja na wao, mmoja anasema anakiri kwamba mbao zile kwa kweli hakuwa na leseni, mbao 405 na amekubali kulipa Shilingi milioni nne na zaidi.

Wa pili ambaye alikuwa na mbao 163 naye halikadhalika amekiri kwamba kwa kweli hakuwa na leseni ya mbao hizo isipokuwa amesema uwezo yeye hana, anaomba Halmashauri iuze. Hiyo ni taarifa *recent* mpaka Mheshimiwa Mbunge alipokuwa amechangia kwenye hoja hii. Mwenzetu Kadu ameandikiwa barua mara mbili njoo uchukue mbao zako, amekwenda mara ya kwanza akakiri kwamba barua ameipata, akasema nitarudi. Amekwenda mara ya pili akawaambiwa sawa barua nimeipata nitarudi, hajaonekana mpaka leo tunavyozungumza. Kwa hiyo, mimi naomba tu Mheshimiwa Kasaka mwambieni Kadu aende kuchukua mbao zake kwa sababu halina ubishi hili. Mahakama imeshaagiza, anaogopa nini? Anajua mwenyewe kwa sababu tumesema ili ukachukue mbao zile, basi si uonyeshe leseni ya uhalali wa mbao hizo basi? Sasa nadhani anapata hata kigugumizi. Lakini kama hana, hata kesho aende, ruhusa atapata hizo mbao zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, .....*(Hapa kengele ya kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji ililia)*

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Ooh, bado nina dakika kidogo?

**NAIBU SPIKA:** Malizia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi niseme haraka haraka mambo mawili, matatu yafuatayo:-

Kwanza, ni hili la Mheshimiwa Makwetta ambalo kwa kweli lazima tukubali kwamba amejitahidi sana katika kutusaidia sana TAMISEMI kuona namna tunavyoweza kukabiliana na tatizo la ukuaji wa Miji. Muda wote akisimama, hii ndio hoja yake kubwa sana na tumemwomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli aje atoe maneno mawili, matatu kuhusiana na jambo hili. Kwa kweli na sisi tunakubali, ipo haja ya kutazama mwelekeo huo kwa sababu suala la ukuaji wa Miji au *urbanization* kwa ujumla ni tatizo na tusipolikabili mapema litatusumbua sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuunda Kamati Maalum kwa ajili ya kukaa Wizarani na kutazama mapendekezo ya maeneo mbalimbali mapya, tumelikubali na tumesema tayari sisi wenyewe tuna huo mkao tayari pale Wizarani na tunafikiri tunakokwenda na watakaokuja wanaweza kuuendeleza vizuri sana ili tuweze kufanya kazi hiyo vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuangalia upya migawanyo ya mipaka, tunalikubali na nadhani halina utata hata kidogo pamoja na muundo wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao nao vile vile utazingatia sana haya mambo ambayo yanakwenda na ukuaji wa Miji ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutoa elimu kwa Maafisa Mipango ili waweze kuharakisha na kubuni vyanzo vingine, hili naomba niliunganishe na lile nililolisema tu kwamba baada ya kuondoa baadhi ya vyanzo, kwa kweli hawa Maafisa Mipango ndio wanatakiwa sasa kuwa Majemedari wakubwa wa kufikiria namna bora zaidi ya kuweza kufanya kazi hiyo ya kuongeza mapato katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, tunakubali kwamba suala hili la Kituo cha Polisi ni la msingi, lakini tutawasiliana na watu wa Mambo ya Ndani tuone namna ya kusaidiana ili kuliharakisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuondoa tatizo la Walimu ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Mporogomyi, nalo tumelikubali. Tumesema tutajitahidi kwa kadri tutakavyoweza kushirikiana na Wizara ya Elimu tuone namna ya kupunguza matatizo haya. Lakini suala la wataalam hawa wa Afya na wengine tutakwenda tunasuasua kidogo kwa sababu hali halisi tuliyonayo ndio hiyo, uwezo mdogo, lakini tuna hakika itafika siku tutalimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la upimaji wa Vijiji na umilikishwaji wa ardhi kwa wananchi, kwanza nilitaka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Nyalandu. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na hasa ukisoma kifungu cha nne, kifungu hicho kinasema waziwazi: "Ardhi yote imewekwa chini ya dhamana ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." Kwa hiyo, yeye ni *custodian* wa ardhi yetu. Lakini ukisoma kifungu hicho hicho kinakwambia: "Ardhi ni za aina tatu; ipo *general*

*land* ambayo nayo inasimamiwa chini ya dhamana ya Rais; ardhi ya Vijiji na kuna ardhi ambayo tunaita ni *reserved land"*. Hakuna namna ambayo mtu anaweza kufika akatumbukia katika eneo hili asijulikane au akaamua kufanya anachotaka kwenye eneo lolote. Hilo ni jambo lisilowezekana.

Suala la Hatimiliki na upimaji wa viwanja, hilo ni jambo lingine na ndio maana Wizara ya Ardhi na sisi tunakwenda sambamba kuhakikisha kwamba jambo hili linazingatiwa kwa sababu lina umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja kwamba Shirika la Masoko litanuliwe ili kuondoa kero. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Lamwai. Tunaikubali na tuna hakika hili tutalifanyia kazi. Tabata tumeshaanza, lakini na Tegeta vile vile kuna eneo ambalo tumeshali-*identify* kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kahumbi alitaka kujua wajibu wa Ofisi ya Rais, kuhusu matatizo ya Walimu. Nadhani hili linaeleweka, tumekuwa tunalisema muda wote. Tunawajibika kikamilifu kabisa kuhakikisha kwamba kero zile zote zinapunguzwa kwa kadri tutakavyoweza na tunapambana na Wakurugenzi ambao kwa kweli ndio wasimamizi wakubwa wa eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum na Kamati zile za UKIMWI tumelipokea, tutalifanyia kazi kwa kadri tutakavyoweza kuhakikisha kwamba tunapata ufumbuzi. Kwa kweli hatuoni mantiki ya kutokuwepo kwa akina mama katika Kamati hizi, kwa hiyo tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba tu niseme kwamba Mheshimiwa Mbawala katika mchango wake wa maandishi alitaka sana mchango wa *Road Fund* ili aweze kumalizia baadhi ya vivuko kule Namtumbo. Kwanza, naomba nimpongeze huyu Mheshimiwa mwenzangu maana yeye na Namtumbo utafikiri ni mtoto na mama yake, kila wakati akisimama ni Namtumbo, Namtumbo, Namtumbo. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini naomba nimhakikishie tu kwamba TAMISEMI katika haya aliyoyataka imeshachangia karibu Shilingi milioni 75 mpaka sasa katika kumwezesha kuhakikisha tunapunguza kero hizo alizozisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa yale ambayo yalipita ya kiujumla jumla, kwa mfano, barabara mpakani mwa Ziwa Tanganyika, ambalo naona Mheshimiwa alilizungumza sana pamoja na Mheshimiwa Mwananzila vile vile. Hili nalo limezingatiwa. Kwa kweli tutajaribu kufanya kazi kwa karibu na Wizara nyingine ili tuweze kuona namna ya kumaliza tatizo au kupunguza kero ile ambayo ipo mwambao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, nimejitahidi kupunguza kadri nilivyoweza, lakini Mheshimiwa Waziri naye atasaidia kumalizia mengine mazito ambayo mimi kama bwana mdogo nafikiri sistahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba na mimi niseme, naunga mkono hoja hii, kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mtoa Hoja, wakati anajiandaa andaa ningependa kuwataarifu na kuwajulisha na pengine kutambua kuwepo kwa yule binti ambaye alikuwa wa kwanza Tanzania nzima katika mitihani ya *Form Six.* Anaitwa Sarah Mhamilawa. Yuko hapa na sisi kwenye *gallery* hii ya kushoto. *(Makofi)*

*(Hapa Ndugu Sarah Mhamilawa Alisimama na Kuonekana kwa Wabunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani hii inaonyesha kwamba akinamama wakipewa nafasi, wanaweza kufanya maajabu sana. *(Makofi)*

Baada ya hayo, sasa namwita Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa na mimi nichukue nafasi hii kutoa maelezo kuhusiana na hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa hapa na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sehemu kubwa sana amezitolea maelezo makubwa sana. Mimi nitaeleza yale ambayo yanahitaji maelezo ya ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo, naomba kama ilivyo kawaida na mimi nitoe shukrani zangu kwanza kwa Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amenisaidia katika kuongoza Wizara yake hii. Mara nyingi sisi ambao ni Wasaidizi wake ndio tumekuwa tunaonekana kana kwamba ndio tunaofanya kazi, lakini kwa kweli tulikuwa tunafanya kazi chini ya maelekezo yake na kila mara tulipokuwa tunajikuta tunakwama ilibidi turudi kwake. Kwa hiyo, kama kuna mambo mazuri yoyote yale ambayo yanaonekana yamefanyika katika Wizara hii, ni kwa sababu Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue nafasi hii kuwashukuru Wasaidizi Wakuu wa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais Dr. Ali Mohammed Shein na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wao kama Viongozi Wakuu wa Serikali yetu hii, wakati mwingine sio lazima twende kwa Rais, bali tumekuwa tukienda kwao ili waweze kutupa miongozo itusaidie katika kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzetu na Manaibu Waziri kwa ushirikiano. Kama ilivyo kawaida, Serikali hii inaendesha kwa *joint responsibility*, ni *joint venture* hii, huwezi kusema wewe mwenyewe katika Wizara ndio ulikuwa unafanya kazi hiyo, daima tumekuwa tukikaa katika vikao vyetu vya Baraza la Mawaziri kuangalia hoja mbalimbali zinazohusu kila Wizara na hususan Wizara yetu hii na wao wamekuwa wakichangia sana kusaidia kutoa mawazo ili tuendeshe Wizara hii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Spika na wewe na Wenyeviti wa Bunge ambao mmesaidia sana kutuongoza na kuhakikisha kwamba

mijadala katika Bunge lako Tukufu ina mielekeo inayohitajika kama sala zetu za asubuhi zinavyoelekeza na daima tumeweza kufikia muafaka ili kuweza kuongoza Wizara hii na nchi yetu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejifunza mengi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Kutoka kwao nimejifunza *Parliamentary Politics*, kwa sababu kuna *politics* za ndani ya Bunge mbali ya *politics* za kule kwenye majukwaa ya siasa. Hapa ni *politics* za kuheshimiana kwa sababu sote tuna jukumu moja la kuijenga nchi yetu. Sidhani kwamba hapa kuna Mheshimiwa Mbunge ana azma ya kubomoa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nisiwasahau Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa. Bahati nzuri wapo pale juu. Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa pamoja na Wasaidizi wao Wakuu wa Wilaya ni Wasaidizi wa Rais na wao ni msingi mkubwa sana, ni nyenzo kubwa sana katika Wizara ya TAMISEMI katika kusimamia yale yote ambayo yanatakiwa kutekelezwa na Wizara hii ya TAMISEMI. Napenda kurudia yale ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kwa kweli wao ni Viongozi wa Kisiasa. Ni Wasaidizi wa Rais kama ambavyo Katiba inasema.

Kwa hiyo, kama Rais na Serikali yake ni wa Chama cha Mapinduzi, hutegemei Mkuu wa Mkoa wala wa Wilaya azungumze mambo ya Vyama vya Upinzani. Tunategemea kwamba kama Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani walivyosema kwamba mwakani wakiingia madarakani, kama wataingia madarakani, nao tunategemea watateua Wakuu wao wa Mikoa. Lakini kwa sasa hawa ni wa CCM!

Isipokuwa kama ilivyo kawaida, Wakuu wa Mikoa hawa wamekula kiapo cha kuitumikia na kuilinda Tanzania bila kuzingatia itikadi za yupi ni yuko upande gani. Kwa hiyo, tunataka kuthibitisha kwamba Chama Tawala daima kipo makini katika kuteua watu ambao watatekeleza wajibu wao kulingana na Katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, naomba niwashukuru wale wote ambao wamechangia katika hoja hii tuliyoitoa hapa Bungeni kama ilivyowasilishwa ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia ndani ya Ukumbi huu kwa kusema na wengine wamechangia kwa maandishi na wapo wengine walichangia wakati wa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Naomba niwataje wale ambao wamechangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. Wa kwanza, ni Mheshimiwa George Lubeleje - Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Grace Kiwelu - Msemaji wa Upinzani kwa Wizara hii; Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Major Jesse Makundi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshmiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Ruth

Msafiri, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Khadija Kusaga, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. Hao jumla yao ni thelathini na moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wale ambao wamechangia kwa maandishi, naomba vile vile niwataje. Hawa jumla yao wapo 33. Wa kwanza, Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Pius Mbawala, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Juma Kapuya, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Christopher Wegga. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Ali Karavina, Mheshimiwa Edga Maokola-Majogo, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Ramadhani Khalifan na Mheshimiwa Paul Ntwina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya hao Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni thelathini na tatu na vile vile wapo Waheshimiwa waliochangia kupitia hotuba ya Waziri Mkuu. Hawa wapo kumi na tano, nao ni Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Khadija Kusaga, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Raphael Mlolwa na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wote hawa napenda kutoa shukrani zetu za dhati za Wizara kwamba michango yao hii waliyochangia hapa imetusaidia sana katika kuhakikisha kwamba tunaboresha hotuba ambayo tumeitoa hapa Bungeni ili kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi yanafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda nichukue nafasi hii kueleza kwamba kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema, Wizara hii ni kubwa, inagusa kila upande wa maisha ya Mtanzania. Ni wazi kwamba, pamoja na mafanikio tuliyonayo, vile

vile yapo matatizo mengi na mafanikio tuliyoyafikia ukweli ni kwamba wote sisi pamoja na Waheshimiwa Wabunge tumechangia katika mafanikio haya.

Mara nyingi huwa tunasahau, wale ambao tunatenda nao kazi hizi tunadhani kwamba ni sisi wenyewe tu ndio tunaojua kuzitenda, lakini tunasahau michango ya wale wote ambao ni wadau na wadau wakubwa sana katika uendeshaji wa Serikali ya Tanzania ni Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, kwa hilo nashukuru sana. Hoja za Waheshimiwa Wabunge zimesaidia sana katika kuonyesha wapi matatizo yapo na wapi panahitaji juhudi za ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yale ambayo bado hayajatekelezwa ukiachilia mbali makosa na mapungufu ya kibinadamu, kwa kweli kama hayajatekelezwa ni kwa sababu ya uwezo wa Serikali hususan uwezo wa kifedha, sio kwa sababu kuna mtu kakaa chini anapanga mipango ya jinsi gani ya kufanya malengo yaliyowekwa yasifikiwe. Naamini jinsi uchumi wetu unavyozidi kukua, ndivyo utekelezaji wetu utazidi kuimarika na kufikia malengo tuliyokwishajiwekea.

Kama nilivyosema, hoja nyingi zimejitokeza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Pinda amezijibu hapa na ametoa maelezo na hoja nyingi, tumesema tunakubaliana nazo, hizi zitatekelezwa. Tunasema hivyo kwa sababu ndio ukweli wenyewe. Yale Waheshimiwa mliyoyaona kwamba ni mapungufu na sisi ndio hayo hayo tunayoyaona. Kwa hiyo, kinachohitajika sio tena kutoa visababu na visingizio na kuweka mikwara bali ni kukubali ili twende kutekeleza kazi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nieleze sasa mambo machache ambayo yanahitaji maelezo kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyozungumza. Kwanza, nizungumzie suala la Mfuko wa Pembejeo. Nikiri kwamba ni kweli Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mwaka jana ilielekeza Serikali kwamba Mfuko wa Pembejeo uhamishwe kutoka Wizara ya Kilimo uje Wizara ya TAMISEMI. Napenda kusema kwamba, suala hili limezingatiwa na Serikali. Kama tunavyojua masuala ya Mfuko huu ni masuala ya kisheria, lakini kwa bahati nzuri katika mawasiliano yetu na wenzetu wa Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amekubali kwamba kesho Wizara yake ndio inaingia katika kuwasilisha makadirio yao, atalitolea maelezo kamili.

Kwa hiyo, katika hili, Waheshimiwa Wabunge naomba mniridhie kwamba tusubiri Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atalieleza vizuri zaidi kwa sababu yeye ndiye mwenye Mfuko huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maagizo mengine matano ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Hayo tutayafanyia kazi, tumeyapokea na mimi naahidi kwamba, Wizara itahakikisha kwamba mwakani Bunge litakapokuwa linajadili utekelezaji, basi pamoja na kwamba wengine inawezekana hatutakuwepo katika Wizara hii, lakini wapo Watendaji wanasimamia masuala hayo, maelekezo hayo mengine matano nayo yatakuwa yametekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hoja za Msemaji wa Kambi ya Upinzani yote aliyoyasema tumeyazingatia na Mheshimiwa Naibu Waziri amejaribu kuyaeleza. Ila napenda nichukue nafasi hii kuelezea machache kwa kuongeza yafuatayo: Kwamba hivi sasa Serikali za Mitaa zipo katika maboresho ambayo msingi wake mkubwa ni kupeleka madaraka kwa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupeleka madaraka kwa Umma ni pamoja na kupeleka nyenzo kwa Umma. Katika kutekeleza hii, mara nyingi kinachoonekana ni majukumu na wajibu wa Serikali Kuu kupeleka madaraka hayo na nyenzo hizo kwa Serikali za Mitaa. Lakini upo upande wa pili kwa wale wanaopokea madaraka na nyenzo hizo. Madaraka hayo na nyenzo hizo zinapokabidhiwa kwa Halmashauri, dhana iliyopo ni kwamba chochote kile kinachopokelewa ndani ya Halmashauri zile ni mali ya wananchi wote wa Halmashauri ile chini ya usimamizi wa Waheshimiwa Madiwani.

Kwa msingi huo, mali zote za Halmashauri zinazosimamiwa na Waheshimiwa Madiwani kwa kweli zinatakiwa Waheshimiwa Madiwani wawajibike kwa wananchi. Serikali Kuu kazi yake ni kusimamia kuhakikisha kwamba nyenzo hizo kweli zinatumika kwa makusudi yaliyowekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, msingi mkubwa wa maboresho ni kupeleka madaraka, lakini vile vile Halmashauri zetu zinao wajibu wa kuhakikisha kwamba madaraka yale haziyahodhi bali zinayafikisha kwa wananchi.

Tunalo tatizo hapa kati, ambalo naamini kila mmoja wetu analijua kwamba, sawa na ambavyo wakati mwingine imekuwa ikizungumzwa kwamba Serikali Kuu inahodhi madaraka, sasa vile vile inajitokeza kwamba madaraka yale yanapopelekwa kwa Halmashauri yakifika pale Wilayani, Halmashauri nayo inahodhi, haitaki kuyapeleka kwenye Kata na Vijiji.

Napenda kuchukua nafasi hii kuziagiza Halmashauri zote kwamba lazima nazo zihakikishe kwamba zinafanya *decentralization by devolution,* kupeleka madaraka na nyenzo zile na ndio maana hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumzia kwamba sasa tutahakikisha hata fedha za Vijiji huko tunakoelekea zitakuwa zinakwenda moja kwa moja kutoka Hazina kwenda huko Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba tunapeleka madaraka kwenye Serikali za Mitaa, hii ni pamoja na nyenzo iwe ni fedha, magari au wafanyakazi, wote wanatakiwa wasimamiwe na waajiriwe na Halmashauri. Hii ndio dhana ya maboresho. Hivi sasa Halmashauri zote zimepewa mamlaka ya kuajiri watu wao mpaka Wakuu wa Idara, bado tumebakiza Wakurugenzi na zipo sababu kwamba sasa hivi tupo katika kipindi cha mpito. Kuna fedha nyingi sana za Serikali Kuu zinapelekwa kule, tunahitaji uwepo usimamizi wa karibu mpaka hapo tutakapoona kwamba kila fedha zinapokwenda kule kweli zinakwenda kufikishwa pale panapotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo sababu ya pili kwa nini Wakurugenzi wanaendelea kushikiliwa kutoka *Centre*. Tanzania tunasifiwa kwamba tumefanikiwa kuua ukabila. Tusingependa sasa hivi katika kipindi hiki cha mpito tujikute kwamba tunaachia Halmashauri ziajiri kila mtu mpaka Mkurugenzi kwa kuhofia kwamba tusije kujikuta tunajenga Ukabila. Kwa sababu mara nyingi huko tulikotoka hasa katika Halmashauri zile za kabla ya Ukoloni, Halmashauri zetu zilikuwa zimejengwa katika misingi ya Ukabila.

Kwa hiyo, tusipoangalia tunaweza kujikuta mimi natoka Halmashauri ya eneo langu, basi sikubali mtu kutoka mahali pengine. Kwa bahati nzuri juzi wakati natoa hotuba yangu tulisema kwamba ipo ile siku ya Serikali za Mitaa na inayo kauli mbiu kwamba, Serikali za Mitaa ni kielelezo cha Utaifa wetu. Ukweli ndio huo kwa sababu leo hii ukienda katika Halmashauri yoyote aghalabu utakuta wafanyakazi wakuu katika Halmashauri ile sio watu kutoka eneo lile. Kwa hiyo, Halmashauri zetu ni kielelezo cha Utaifa wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niligusia suala la Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Napenda kusisitiza kwamba, wapo pale Kikatiba. Sheria Na.19 ya Mwaka 1997 na Sheria Na.7 na Na.8 ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 zinaeleza wazi kwamba hawa ni wasaidizi wa Rais na ni wahimili wakubwa katika masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo yao.

Ni kweli zipo hoja kwamba sasa kwa vile labda tuna-*devolve* madaraka, basi ziachiwe Serikali za Mitaa. Lakini tunasema kwamba wao wapo pale kwa *eyes on hands off, as long as* mambo yakiwa yamekwenda kwa amani, basi wanaachia Halmashauri zijiendeshe. Lakini kama kuna tishio la amani, tusisahau kwamba kiapo cha kila Kiongozi ikiwa ni pamoja na sisi tuliomo humu ndani, kwanza ni kuhakikisha kwamba tunailinda Katiba na Viongozi hawa wanaomwakilisha Mheshimiwa Rais katika maeneo yao, basi wanawajibika kuhakikisha kwamba amani na utulivu katika maeneo hayo vinadumishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba, tunaelekea kwenye uchaguzi. Pamoja na kwamba sasa tunakwenda kwenye kipindi cha kampeni, tusisahau kwamba dola ipo. Ipo pale kuhakikisha kwamba amani na utulivu katika nchi hii vinaendelea kudumishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie maeneo ya utawala ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea kwamba nitaeleza kwa ufasaha zaidi. Ni kweli yapo maombi mengi sana ya kuanzishwa kwa Wilaya.

Nataka kusema kwamba suala hili liko Mezani panapohusika na upo uwezekano kabla hatujakwenda kwenye uchaguzi tutakuwa tumepewa maelekezo ya aina fulani na Mheshimiwa Rais hasa tukizingatia kwamba yeye ndiye mwenye mamlaka ya Kikatiba ya kugawa maeneo ya Utawala.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri usipoteze *hope* na Waheshimiwa Wabunge wote mlioomba Wilaya siyo zote zitakazopatikana, naamini kuna baadhi zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile yamekuwepo maombi mengi ya Kata nayo yamezingatiwa, lakini kama tunavyoelewa, tunakwenda kwenye uchaguzi, lazima Tume ya Uchaguzi sasa hivi iendelee na mipango, hatuwezi ku-*create* Kata hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba suala hili na Kata hizo zitaangaliwa baada ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kuzungumzia suala la kupandisha Miji hadhi. Nini dhana yetu iliyopo? Dhana iliyopo ni kwamba sasa hivi *trend* ya dunia ni watu kutoka Vijijini kuja Mijini. Hakuna njia utawazuia binadamu kutoka Vijijini kuja Mijini, ndivyo ilivyo huko Marekani, Ulaya na Asia. Hata kwa makisio ya UN *habitat* wanatueleza kwamba katika mwaka 2030 watu asilimia 51 watakuwa wanaishi Mijini Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kwa hiyo, tujitayarishe kwamba Miji itakuwa na wakazi wengi zaidi jinsi siku zinavyoendelea. Kilichopo kinachotakiwa ni kujitayarisha, ndiyo maana kwa kuanzia, mwaka jana tuliweza kutenga Miji Midogo 50 na tutaendelea kutangaza Miji mingine ambayo inawiva kuwa Miji Midogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tumesema sasa Makao Mkuu yote ya Wilaya katika nchi hii yatakuwa ni Miji. Tutakwenda hatua kwa hatua, lakini kila Wilaya ijue kwamba Makao Makuu ya Wilaya ilipo, *eventually* itakuwa ni Mji na mingine tutaanza kuitangaza. Naamini kabla Bunge hili halijakwisha tutangaza Miji isiyopungua 25 ikiwa ni pamoja na Njombe Kusini kwa Mheshimiwa Anna Makinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumesema dhana hapa ni kwamba Makao Makuu yote ya Mikoa itakuwa ni Manispaa. Kwa hiyo, sasa hivi tunazo Manispaa tisa, bahati nzuri tuna-*create* Majiji matatu lile la Mbeya, Tanga na Arusha. Hapa napenda nifafanue Arusha, Arumeru ilikuwa ni Halmashauri ya Wilaya sasa nayo inapandishwa kuwa Manispaa. Arumeru pamoja na Manispaa ya Arusha ndizo zitakazounda Jiji la Arusha. Sababu ni ndogo tu, kwa sababu sasa hivi Manispaa ya Arusha haiwezi kupanuka, watu wanaendeleza ujenzi ndani ya Arumeru, ni lazima tu- *capture development* ndani ya Arumeru. Kwa hiyo, sasa hivi Mji ule ukishapata hati yake, utakuwa ukienda Arusha maana yake unakwenda Manispaa ya Arusha na Manispaa ya Arumeru. Manispaa nyingine zitapandishwa hadhi kuwa Majiji kwa jinsi ambavyo hali inajitokeza na inaruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuelezea masuala ya mipaka kwamba tumeyashughulikia. Lakini napenda kusisitiza hapa kwamba wakati tunazungumzia mipaka, daima sasa wapimaji wetu lazima wafikirie kuweka mipaka kufuata *physical features*. Hii habari ya kuchukua mpaka unakatisha katika mapori

halafu unamwambia mwananchi wewe uko katika Kijiji hiki, ataelewa saa ngapi? Kwa mwananchi ni lazima zaidi kujua kwamba ukivuka bonde lile, ukienda upande wa pili wa mlima ndiyo unaingia katika eneo fulani. Kwa hiyo, tujaribu kuzingatia *physical features* katika kutengeneza mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda hapa kukiri kwamba katika kupandisha hadhi Majiji na Manispaa tumezingatia kwamba hakuna mpaka wa Jimbo lolote la uchaguzi litaingiliwa na hakuna mpaka wa Kata yoyote itabidi ugawanywe. Kwa hiyo, kazi hiyo yote inafanyika tukijua kwamba tunaingia kwenye uchaguzi. Madiwani watakuwa katika maeneo yao kama yalivyopitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi ya Vijijini Mheshimiwa Naibu Waziri amelieleza hapa vizuri. Ningependa niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna Mwongozo wa Ushirikishwaji katika Mipango ya Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini kama ulivyotolewa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Hiyo ndiyo inayoweka utaratibu mzima na hatua zote ambazo zinatakiwa kuchukuliwa katika kumiliki ardhi ya Kijiji. Karibu mambo mengi tumeyaeleza hapa. Mapungufu bado yapo, nadhani ndiyo maana tuko kazini sote ili kuweza kukabiliana na mapungufu yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa msaada ambao wameweza kuipatia Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Wizara halafu tutakwenda kwenye Mikoa. Tunaanza na vifungu vya Wizara kwa sababu ndiyo vinalinda na Mikoa pia. Kwa hiyo, tutaanza na Wizara halafu tutakwenda kwenye Mikoa.

### Fungu 56 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Kif. 1001 – *Administration and General* … Shs. 3,248,323,300/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba msimame ili tuweze kuwaandika majina.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nijaribu kuuliza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2000 bahati nzuri Mji wetu wa Shinyanga ulibahatika kuwa Manispaa. Wakati ule Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru alikuwa Waziri, Mji wetu ulikuwa Manispaa. Mwaka 2001/2002, 2002/2003, 2003/2004 nilitegemea kwamba Mji wetu vilevile utawekwa katika Mipango ya Serikali katika kuboresha barabara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, kazi hiyo sijaiona mpaka sasa na kwa bahati nzuri kwenye bajeti ya mwaka jana tarehe 25 Juni, 2004 Mheshimiwa Waziri nilimwuliza kwamba kuna tatizo gani Mji wetu mpaka sasa pamoja na kwamba umekuwa ni Manispaa haujawekwa katika hadhi hasa kama Miji mingine? Mheshimiwa Waziri aliniahidi na kwa bahati nzuri ninayo *Hansard* na akasema kwamba: "Kazi hiyo ingelifanyika kwenye bajeti ya mwaka 2004/2005." Kazi hiyo haikufanyika na bahati nzuri niliandika barua haikujibiwa. Ndiyo kusema kwamba Mheshimiwa Waziri alilidanganya Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo, vinginevyo kwa kweli pamoja na kwamba niliandika kule kwamba ninaunga mkono, lakini kama hiyo haikuwekwa, nipate maelezo *because* haiwezekani miaka yote hii mimi wananitania tu. Hivi ama mimi sipendezi! *No*, naomba wanieleze! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi ufuatao:- Ni kweli mwaka jana tuliahidi, lakini fedha hizo zilikuwa zitoke kwenye mradi, bahati mbaya fedha hizo hazikupatikana. Sasa hivi kinachofanyika ni kwamba umeanzishwa mradi mwingine wa *Local Government Support Programme* ambao utahusisha Halmashauri hizi. Tunaamini kwamba sasa itawezekana kusimamia au kushughulikia suala la barabara za Manispaa ya Shinyanga.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** *I hope it will be done.*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu. Wakati nilipokuwa nachangia katika hotuba ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha nilizungumzia suala la harufu mbaya pale Ikulu na leo nimelirudia. Sasa bahati mbaya sikujibiwa na mimi sitanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunajua kwamba hata ukimaliza kula samaki lazima unawe kwa sabuni, huwezi kwenda unatembea nazo unasema rafiki zangu mjue. Sasa huyu Mheshimiwa Waziri ambaye anahusika na Serikali za Mitaa, yale Majiji yanapanga pale samaki na Mheshimiwa Waziri Mkuu bahati nzuri yupo hapa kama wao hawasikii harufu ile, wageni wanasikia. Mimi nilikwenda pale nikaumwa tumbo, shahidi ni Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, nilimwambia kwamba naumwa tumbo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kujua, hao wanaocheka, wacheke, lakini mimi najua harufu ile ipo. Sasa tunataka kujua kama wengine kule wanakataa

madampu, kwamba madampu yapelekwe mahali fulani na samaki ni kitu kizuri, lakini pale ni uchafu kwa Ikulu yetu siyo ya mtu mmoja. Tunataka kujua kama Mheshimiwa Rais anafurahia ambaye ndiye Rais wa Nchi na Waziri Mkuu anafurahia? Tunataka kujua. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nikiri kwamba pale *Ferry* ni soko la samaki na daima samaki wana harufu ya kisamaki. Manispaa ya Ilala imejitahidi kutengeneza mazingira ya pale yawe safi na hatua zinaendelea kuchukuliwa. Naamini jinsi tunavyoendelea hali itatengemaa na itakuwa nzuri tu. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui! Tunavyoelewa, pale kuna upepo wa bahari na samaki wanavuliwa pale bado wakiwa ni wabichi. Mimi sijasema hawasafishi pale, sijasema hakuna mifereji ya maji, sijasema hicho. Mimi ninachosema ni kwamba eneo lile kwa heshima ya nchi yetu, mnajua mimi ninashangaa hiyo kukwepa ukweli, unakuwa unaukwepa uende wapi? Ukweli uliopo ni kwamba samaki wale wangewekwa kwenye eneo lingine siyo pale. Sasa kama Mheshimiwa Waziri anasema wao wananenepa kwa kusikia harufu ile, basi mimi nanyamazawaendelee kunenepa lakini panatuaibisha. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, nadhani huhitaji maelezo maana umesema basi.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kupata ufafanuzi kidogo tu kwamba Mheshimiwa Waziri kwa tangazo lake la 2004/352 alipandisha hadhi Miji mitatu, Babati, Korogwe na Kibaha. Sasa katika mchango wangu kwa maandishi nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Waziri anieleze kidogo kuhusu bajeti ya Halmashauri hizi.

Nilivyoangalia kwenye mpango huu wa bajeti ya Maendeleo kwa Mikoa, Halmashauri za Miji na Wilaya nimeona Halmashauri ya Mji wa Babati imepangia fedha kidogo sana kwenye jedwali Na. 4. Sasa unapoanzisha Halmashauri ya Mji, kuna mambo mengi ambayo yanatakiwa yatekelezwe ndani ya Mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua: Je, kuna mipango mingine au fedha ndiyo hiyo kidogo inayoonekana hapo? Kwa sababu hizo fedha kwa kweli hazina hata sababu ya kutamkwa, ni kidogo sana ukiangalia Jedwali Na.4. Nataka kupata hayo maelezo tu. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo kwa sababu limejitokeza sasa hivi, tutakwenda kuliangalia.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nina maelezo mafupi tu. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake na kweli nililizungumza hili jambo jana kwa uchungu na maelezo aliyoyatoa

ninayafahamu. Tatizo lililotokea ni kwamba *process* nzima ina utata walichukua mbao kwa Bwana Ramadhani Kadu zaidi ya 700 halafu wakamrudishia mbao 400. Nyingine wanatafuta watu wengine kwamba waje wachukue zile mbao ndipo panapotokea utata.

Zile mbao zilikuwa zimegongwa. Mbao zikigongwa zinachukuliwa kwamba ni halali na zimechukuliwa kwake mbao 700. Inapofika wakati wa kumrudishia, unasema aje achukue mbao 400 na nyingine watachukua watu wengine? Ndiyo maana nikalizungumzia hapa. Nadhani tatizo ni *procedure* na ndiyo maana hata yeye mwenyewe anasita kwenda kuzichukua kwa sababu mbao zilizochukuliwa kwake zilikuwa 700, sasa anaambiwa akachukue mbao 400 ambazo ni pungufu. Ndiyo tatizo lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikutaka iwe mvutano kati ya mimi na Mheshimiwa Waziri au Wizara, nilitaka tu kumweleza Mheshimiwa Waziri kwamba kuna huu utata ambao nilifikiri yeye angekuwa amechukulia maanani kwamba nini kimefanyika. Maelezo haya mimi ninayafahamu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ulitaka afahamu tu utata huo au unataka ujibiwe kwa maelezo?

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka afahamu suala hilo na jinsi ya kuchukua hatua.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa ufafanuzi walioutoa kuhusiana na fedha iliyokuwa imetengwa kupitia Mkoa wa Dar es Salaam kwenda kumsaidia mgombea wa Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Maelezo yamefafanuliwa vizuri na kwa bahati nzuri vitabu vilivyorekebishwa vimewekwa kule kwenye *pigeon hole* tumeviona. Naamini kazi hiyo ingeweza kuwa imefanyika hata kabla ya kuwasilisha hotuba ya bajeti humu Bungeni. Nampongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo ningemwomba Mheshimiwa Waziri kupitia Bunge hili kuwahakikishia Watanzania ambao naamini wanatusikiliza hivi sasa, kama siyo kutuona kwamba ile dhamira ambayo amezungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu, kwamba wakati mwingine dhamira inamjia mtu na kujisahau na akajikuta ameweka *figure* hizo na maneno hayo kwamba taswira hiyo na dhamira hiyo haitajitokeza wakati wa uchaguzi kwa kuyakuta magari ya Halmashauri, magari ya Taasisi ya Serikali na magari ya Wakuu wa Wilaya yakienda kusaidia katika kampeni za baadhi ya Wagombea na kwamba Wagombea wote watakuwa *treated* sawa na magari ya Taasisi hizi na dhana nyingine za Taasisi hizi hazitahusika.

Iwapo hali hiyo itatokea: Je, atakuwa tayari kutoa Waraka wa kusisitiza jambo hilo ili jambo hili lisiweze kujitokeza. Naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani inafahamika kwamba vipo vyombo vya dola ambavyo lazima viendelee kufanya kazi zake. Kwa mfano, huwezi kusema Polisi wasiwepo, huwezi ukasema Mkuu wa Wilaya ama Mkuu wa Mkoa asizunguke kuangalia na kwa vyovyote vile Mkurugenzi wa Halmashauri ndiye msimamizi wa uchaguzi, lazima atatumia gari la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile napenda kusisitiza kwamba, yaliyoandikwa na kusahihishwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala hayakuashiria kwamba ni kweli kuna fedha Shilingi milioni 20 zilizotengwa kwa makusudi kwa ajili ya Mgombea wa CCM. Kwanza, kifungu kinachosema zimetengwa, kweli unatenga milioni 20 kwa ajili ya *furniture;* Mgombea wa CCM anachukua *furniture* apeleke wapi?

**MBUNGE FULANI:** Hapo sasa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Pili, kampeni za CCM hazitegemei Shilingi milioni 20, tunatumia mabilioni. Kwa hiyo, katika zoezi hilo tunajua kwamba kuna suala la kupata nafasi ya kisiasa, ukipatia hapo hapo shika papo hapo. Lakini tunaamini kwamba hakukuwa na nia mbaya yoyote ya kusema fedha zitengwe kwa ajili ya kumsaidia Mgombea wa CCM. Serikali fedha zote ilizotenga imezipeleka Tume ya Uchaguzi kusimamia uchaguzi huo siyo kitu kingine. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapolieleza hili, mimi siyo mwehu kwamba sielewi ninachozungumza. Kauli aliyoitoa Mheshimiwa Waziri ninapozungumzia dhamira, sizungumzii suala la magari ya Polisi kwenda kufanya kazi yao kama Polisi katika shughuli za Ulinzi na Usalama, sizungumzii suala la Ma-*DC* kuhakikisha usalama upo katika maeneo ambapo shughuli za uchaguzi zitakuwa zinafanyika, sizungumzii suala la wasimamizi wasaidizi kwenda kuzungukia Vituo na kuweka taratibu nzuri za uchaguzi. Suala linalozungumza hapa iwapo itabainika, maana yake tuko huko kwenye *grass root*, magari hayo wakati mwingine yanatumika kuwazungusha watu wa Chama cha Mapinduzi kwenda kufanya kampeni. Sasa hilo ndilo ninalolitaka.

**MBUNGE FULANI:** Omba radhi!

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani ya Bunge hatupitishi bajeti kwa kuapishana kwa Misahafu au Biblia, tunapitisha kwa *principle* na *logic.* Mimi nilichotaka ni *principle* na *logic:* Je, mambo haya hayatajitokeza? Yakijitokeza, wananchi wawafanyaje hao watakaofanya hivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba Kanuni na Sheria za Uchaguzi zinasimamiwa na Tume ya Uchaguzi na taratibu zote zimewekwa kama yapo malalamiko hatua gani zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba kama hilo likijitokeza tutaiachia Tume ya Uchaguzi ifanye kazi yake. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ndiyo kwanza tunaanza hii *process* ya kupitisha Matumizi ya Wizara kwa Wizara, ningependa tu kuwakumbusha ile Kanuni ya 81(6) inayozungumzia muda ukiisha suala la *guillotine* kwamba tunaweza tukajadili, lakini hata kama kitabu kizima kitakuwa kimebaki na bado dakika 10 tu, basi tutasimamisha watu kuchangia zaidi, tutahoji kifungu bila majadiliano. Kwa hiyo, naomba hilo mlikumbuke. *(Makofi)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … … .. Shs. 223,814,600/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning Division* … … …Shs. 474,782,900/=

Kif. 1004 - *Management Information System Division* ... ... ... ... ... ... ... ... ..Shs. 438,147,000/=

Kif. 1005 – *Legal Services Division*… … … … Shs. 186,849,900/=

Kif. 2001 - *Regional Administration Coordination Division* … … … … … … Shs.2,714,636,800/=

*(Vifungu viliyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 -*Local Government Coordination Division* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 16,036,243,100/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hii *Local Government Coordination Division* 2002, nimeangalia pale 270200 kuna mambo ya *Technical Equipment, Fumigation and Cleaning,* nameangalia pale mwisho *Mobile Vehicles and Self propelled Equipments* ni fedha nyingi. Sasa nilipokuwa nazungumza hapa nilisema kuhusu soko la Tandale. Majiji yale ya Dar es Salaam na Manispaa za Kinondoni zinahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde. Kuna watu wengine sijui wanafurahia uchafu! Maana yake mimi sikai Tandale, lakini nina maana kwa sababu ule ni Mji watakuwepo watu wa Karagwe wako pale. Sasa ninaomba nielewe kwamba ule uchafu ulioko pale na watu wanatozwa ushuru, ndiyo sera ya Serikali kwamba watu walipe ushuru halafu pakae pachafu na wale wanaoishi pale wakae kwenye uchafu ili watu wakifa kwa kipindupindu tuanze kusikitika hapa na kulia machozi ya mamba? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niseme hapa kwamba Serikali yetu haipendi uchafu ndiyo maana tunatumia mamilioni ya fedha kuweka hali ya usafi. *(Makofi)*

Pili, hapa tunazungumzia *Local Government Coordination Division* Wizarani, kwa vile amezungumzia Tandale labda angesubiri wakati tukizungumza Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu una bajeti yake, pale upo uwezekano kwamba tutajibu vizuri zaidi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kitabu hiki kipo kuahirisha tatizo siyo tatizo, kwa hiyo, mimi nakubali. Kwa hiyo na wale wanao-*shout* nadhani wasubiri. *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 – *Sector Coordination Division*… … Shs. 25,024,385,600/=

Kif. 3001 - *Organizational Development Division* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 4,983,016,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MIKOA**

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha … … … … Shs. 21,794,195,000/=

Fungu 71 - Mkoa wa Pwani … … … … … Shs. 17, 828,373,600/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma … Shs. 24,977,725,100/=
Fungu 73 - Mkoa wa Iringa… … Shs. 26,186,949,300/=
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma … … Shs. 22,190,709,800/=
Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro…Shs. 31,327,178,700/=
Fungu 76 - Mkoa wa Lindi … Shs. 14,052,762,400/=
Fungu 77 - Mkoa wa Mara .. Shs. 22,463,021,200/=
Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya… … Shs. 32,652,377,200/=
Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro … Shs.26,863,152,200/=
Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara … Shs.17,507,877,200/=
Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza … Shs.39,940,170,900/=
Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma … Shs.19,364,408,600/=
Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga … Shs.37,312,207,900/=

Fungu 84 - Mkoa wa Singida … Shs.17,602,388,600/=
Fungu 85 - Mkoa wa Tabora… Shs.24,402,368,000/=
Fungu 86 - Mkoa wa Tanga … Shs.28,624,037,000/=
Fungu 87 - Mkoa wa Kagera … Shs.28,956,844,800/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam… Shs. 33,691,368,100/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa hoja nilikwishaisema, nilisubiri hapa kwamba Mheshimiwa Waziri atuambie kama pale Tandale wanapotoza ushuru, wanatoza kwa ajili gani na kama wamepasafisha ni lini au wana utaratibu gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii kuna programu ya Dar es Salaam *upgrading* ambayo itahusisha masoko ya Manzese na Tandale. Kwa hiyo, naamini kwamba suala hili litashughulikiwa.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa… … Shs.17,689,002,400/=
Fungu 95 - Mkoa wa Manyara … Shs.16,513,117,800/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Kifungu 1001 – *Administration & General ...* Shs.50,000,000/=

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii.

Nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Waziri kwamba Kibara hivi sasa ni Mji ambao kwa kweli unajitegemea, hauhitaji kuongezewa hata tofali kuitwa Mji mdogo na hapa anaposema Mheshimiwa Waziri kuna watu huko Kibara wanasubiri. Huenda wasilale wanasubiri kutangaziwa kwamba hivi sasa ni Mji mdogo na naamini haitakuchukua sekunde mbili kutamka Kibara ni Mji mdogo. Sasa kwa hilo basi

ninamwomba Mheshimiwa Waziri atupatie jibu kwamba kuanzia sasa Kibara ni Mji mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara itaandaa utaratibu ikaangalie Kijiji hicho cha Kibara tuone kama kiko tayari kuwa Mji mdogo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 – *Local Government Coordination Nation Division* ... ... ... ... ... Shs.100,395,724,400/=
Kifungu 2003 – *Sector Coordination Division*… Shs. 7,545,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Organizational Development Division*... ... ... ... ... ... ... ... .. Shs. 45,273,760,000/=

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nilimwuliza Mheshimiwa Mtoa Hoja, kwa nini baadhi ya watu waliokuwa watumishi wa Halmashauri kwa kada ya Makatibu Kata na ambao hawakuchukuliwa na Halmashauri kwa kada ya Watendaji wa Kata mpaka sasa bado hawajalipwa mafao yao wakiwemo Watendaji wanne wa Jimbo la Buyungu? Kwa nini mpaka sasa hawajalipwa na watalipwa lini na nani anawajibika kuwalipa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri unaweza, kujibu lakini hili ni fungu la Matumizi ya Kawaida. Hii ni maendeleo. Lakini Mheshimiwa Waziri kwa sababu anataka kujibu vizuri jibu tu kama una jibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama ulivyosema tukalifanyie kazi suala hili.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili nilishalipeleka Wizarani tangu mwezi Juni, 2003 na mpaka hivi sasa sijapata majibu. Nilitegemea kwamba hapa watakuwa wameshapata majibu. Naomba majibu Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nilikuwa nasema kwamba tukalifanyie kazi kwa sababu lazima tuangalie watu hawa walipokuwa katika ajira ilikuwa ni ajira ya Halmashauri kwa sababu Serikali Kuu imeanza kuchukua

*responsibility* ya Watendaji mwaka 2004. Sasa kama ni huko nyuma itabidi tuangalie kwa nini Halmashauri imekuwa haiwalipi. Ndiyo maana nasema ngoja tukalifanyie kazi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha… … .... … ... Shs. 417,199,800/=

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilikuwa nimezungumzia suala la maji yaliyokuwa yapelekwe kwenye Hospitali ya Wilaya ya Karatu ambayo yamekwama kwa zaidi ya mwaka mmoja. Taarifa hizo zilipelekwa ngazi zote husika mpaka Ofisi ya Rais na kwenye mchango wangu niliuliza nini kinaweza kufanyika kwa sababu athari ya mradi huo kukwama ni kukwamisha mradi mwingine wa Shilingi milioni 300 ambazo zinatolewa na wafadhili wetu kupitia *Saint Joseph's Hospital,* Marekani.

Mheshimiwa Waziri hakugusia japo *informally,* Mkuu wa Mkoa ameniambia kwamba linafuatiliwa. Sasa ningependa nipate ufafanuzi wa kina ili iingie kwenye rekodi kama kweli itashughulikiwa au vipi na taratibu za kawaida zitafuatwa za Serikali kuona kilichokwamisha sasa haitakwamishwa tena na kwamba wafadhili wanakuja tarehe 6 mwezi Julai, 2005 kwa lengo la kuondoa Shilingi milioni 300 za mradi mwingine nilioutaja. Sasa ili fedha hizo ziokoke, ningependa Serikali itoe kauli yake hapa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haikusudii kukwamisha chochote. Kama Mkuu wa Mkoa alivyoahidi na mimi vile vile amenieleza hivyo kwamba atakwenda kulisimamia suala hili. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 71 - Mkoa wa Pwani … … … ... Shs.7,987,687,000/=
Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma … … ... Shs.4,964,000,000/=
Fungu 73 - Mkoa wa Iringa … … … Shs.5,679,876,300/=
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma … … Shs 577,000,000/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro … … ... Shs.1,086,800,200/=

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote* 1001 *sub-vote* ndogo 6298 *Self Help Projects.*

Katika mchango wangu wa maandishi nimemwarifu Mheshimiwa Waziri kwamba kumekuwa na mgogoro wa nyumba ambazo Kijiji cha Makidi kinadai ni zake na ambazo ziliuzwa katika mkumbo wa kuuza nyumba za Serikali. Jambo hili nililisema mwaka jana 2004 nikaahidiwa kwamba litashughulikiwa. Pia, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika Rombo Madiwani wakalalamika juu ya hizo nyumba na akaahidi hatua zitachukuliwa. Lakini ilipotokea katika Kamati katika kipindi hiki tulipata maelezo tofauti kwamba nyumba zile zimeuzwa na *Building Agency* na sio Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba hizo zimekuwa kwenye mgogoro na jinsi ninavyoongea, sasa zimekamatwa kwa amri ya Mahakama kutekeleza hukumu iliyotolewa dhidi ya Kijiji cha Makidi. Kijiji kimekuwa kinafanya jitihada kukomboa zile nyumba. Serikali imekaa kimya, lakini wakaamua kuuza wakati Kijiji kinazipigania. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko la Serikali kuhusiana na hizo nyumba: Je, ni Serikali imeziuza na kama haikuziuza anatoa agizo gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naamini kama ilivyosemwa suala hili liko Mahakamani. Kama haliko Mahakamani, basi nitamwomba Mheshimiwa Mbunge labda tuwasiliane na Wizara ya Ujenzi kwa sababu *Building Agency* iko kwenye Wizara ya Ujenzi ili tuweze kufikia muafaka. Hata sisi tuna *interest* kama kuna dhuluma imefanyika dhidi ya nyumba za Kijiji, basi tusaidie tuweze ku-*retrip* hali hiyo.

**MHE. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili Serikali ina habari nalo na kuna barua zimeandikwa zaidi ya 10 Serikalini katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa *Regional Commissioner* na *DC*. Kwa hiyo, sio kwamba Serikali haina habari. Inayo habari, lakini wanatupiana mpira. Sasa nani abebe lawama na hatua gani zichukuliwe?

**MWENYEKITI:** Nani abebe lawama? Ungependa Waziri aseme nani abebe lawama? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha tunapata *solution* ya suala hilo. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 76 - Mkoa wa Lindi … … … ... ... Shs.892,000,000/=

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji *clarification* kwa *vote* 1001 *sub-vote Rehabilitation of DC's House*. Ipo ya kwanza 6214

*Rehabilitation of DC's House* Kilwa, halafu nyingine *Rehabilitation of DC's House* wapi? Hiyo hiyo Kilwa au?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika sio Kilwa. Inawezekana tutaangalia na Mkoa tuone walimaanisha wapi.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 77 - Mkoa wa Mara .. … … ... Shs. 1,980,000,000/=
Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya… … … Shs. 3,510,572,000/=
Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro … … Shs. 2,617,618,400/=
Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara … … Shs. 949,000,000/=
Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza … … Shs. 6,079,623,900/=
Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma … … Shs. 839,207,300/=
Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga … … Shs. 770,148,200/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 84 - Mkoa wa Singida... ... … … ... ... Shs.773,336,400/=

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa tarehe 4 Novemba, 2001 tulimwandikia barua kuwa kuna watumishi fulani katika Halmashauri ya Iramba ambao utumishi wao umekuwa na kasoro. Wamezamia zaidi katika biashara zao kwa sababu wamekaa sana pale, wameleta mazoea. Tulimwomba awahamishe au awastaafishe kwa manufaa ya Umma, mpaka leo hajafanya lolote. Naomba maelezo ? (*Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya watumishi hawa walihamishwa. Lakini napenda tu kukumbusha kwamba sasa hivi ajira ya watumishi wote wako chini ya Halmashauri yenyewe. Halmashauri inatakiwa iwachukulie hatua za kinidhamu. Kwa hiyo, uwezekano wa kuwahamisha sasa haupo tena.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 85 - Mkoa wa Tabora… … … Shs. 646,000,000/=
Fungu 86 - Mkoa wa Tanga … … … Shs.3,206,440,600/=
Fungu 87 - Mkoa wa Kagera … … Shs.3,088,482,000/=
Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam… Shs 1,806,000,000/=
Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa… … Shs. 519,000,000/=
Fungu 95 - Mkoa wa Manyara … … Shs.3,198,913,600/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati ya Matumizi kuwa imekamilisha shughuli zake za kufikiria Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri zake kwa mwaka wa fedha 2005/2006 sasa naomba kutoa hoja kwamba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yamepitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo tumefikia mwisho wa shughuli za leo.

Lakini ningependa tu kuwakumbusha kwamba katika hatua hii ya Kamati, unapotaka kutoa hoja yoyote katika Kamati tafadhali sema kifungu gani au kifungu kidogo gani unachozungumzia, kwa sababu kama mlivyoona hapa masuala ya Matumizi ya Kawaida yameulizwa kwenye Maendeleo na Matumizi ya Maendeleo yameulizwa kwenye Matumizi ya Kawaida.

Hili nililiachia kwa sababu ndio tumeanza na hii ni awamu ya mwisho mwisho sio vizuri kukatisha katisha watu. Kwa hiyo, naomba tuzingatie hili katika siku zijazo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.51 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 23 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*